RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2011

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.
Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)211515/8, Nukushi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na.CA.4/01/2010/11 Tarehe: 26 Machi, 2012

Kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 9120,
Ikulu,
Dar es Salaam.

Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti iliyotajwa hapo juu.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.

www.JamiiForums.com

YALIYOMO

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ix
Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ix
Dira ix
Dhima xi
Vifupisho xxi
DIBAJI xiiivii
Shukrani xvii
Muhtasari wa mambo muhimu katika ripoti ya ukaguzi wa Taarifa za fedha za Serikali Kuu Kwa mwaka 2010/2011 xix

A: UTANGULIZI xix
SURA YA 1 1
1.0 Utangulizi 1
1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Umma 1
1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa 2
1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi Ndani ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi 2
1.4 Ukaguzi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa 3
1.5 Mawanda na viwango vya Ukaguzi vinavyotumika 3
1.6 Sera ya Kiuhasibu 4
1.7 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa 5
1.8 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani 5
1.9 Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi 6
SURA YA 2 9
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YATOKANAYO NA HOJA ZA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA 9
2.0 Utangulizi 9
2.1 Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ripoti ya Serikali Kuu kwa miaka ya nyuma 10
2.2 Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli /Wakuu wa vitengo yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabuza Serikali. 13
2.3 Mamlaka ya Mapato Tanzania 15
2.4 Majibu ya hoja zitokanazo na ukaguzi wa Taarifa

www.JamiiForums.com

Jumuifu za Taifa. 15

SURA YA 3 21
MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA 21
ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO 21
3.1 Utangulizi 21
3.2 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi ya Kawaida katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa 21
3.3 Ulinganisho wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya Wizara na Idara za Serikali kwa kipindi cha 2009/2010 na 2010/2011 22
3.4 Uwiano wa bajeti dhidi ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara 24
3.5 Mamlaka ya Mapato Tanzania 25

SURA YA 4 35
MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI 35
4.0 Utangulizi 35
4.1 Madhumuni ya ukaguzi wa awali 35
4.2 Mawanda ya ukaguzi wa awali 36
4.3 Changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi 36
4.4 Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo 36

SURA YA 5 443
MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA WIZARA, IDARA, WAKALA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA 443
5.1 Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo hazijarudishwa Serikalini 443
5.2 Matengezezo ya magari katika karakana zisizoidhinishwa na TEMESA 44
5.3 Malipo ya mishahara kwa wastaafu wasiokuwa kazini na maafisa wasio nastahili 45
5.4 Malipo yenye nyaraka pungufu 47
5.5 Mali na vifaa visivyopokelewa 48
5.6 Malipo yaliyofanyika kutoka katika vifungu visivyohusika Sh.340,756,700.80 49
5.7 Malipo yenye shaka 49
5.8 Kuongezeka kwa malipo ya posho 50
5.9 Hesabu za Vyama vya Siasa zilizokaguliwa kutowasilishwa kwa Msajili 51

www.JamiiForums.com

5.10 Mishahara isiyolipwa kutowasilishwa Hazina 51
5.11 Mali ambazo hazikuandikwa katika daftari la mali zisizohamishika…. 52
5.12 Madeni na Mihadi 53
5.13 Ukaguzi wa Usimamizi wa Manunuzi 55
5.14 Taarifa ya Idara ya Usimamizi mali za Serikali kuhusu usimamizi wa vifaa na mali……. 60

SURA YA 6 63
UCHAMBUZI WA HESABU JUMUIFU ZA TAIFA 63
Utangulizi 62
6.1 Masuala yaliyojitokeza mwaka huu na mapendekezo 63
6.2 Madeni ya Mikopo yanayodaiwa na Serikali 66
6.3 Taarifa ya Madeni yasiyolipwa 66
6.4 Taarifa ya deni la Taifa 67
6.5 Taarifa ya malimbikizo ya Maduhuli Taarifainaonyesha kuwa, kuinua ukusanyaji wa mapato. 67
6.6 Taarifa ya mali na vifaa vingine Taarifa fedha zilizopangwa katika bajeti ya mwaka husika zinatumika 68
6.7 Taarifa ya upotevu Sh.11,152,048,065 68
6.8 Madeni ya Serikali ambayo hayakuonyeshwa katika hesabu 68
6.9 Amana za Serikali ambazo hazikuonyeshwa katika katika taarifa 70
6.10 Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa na Serikali 72

SURA YA 7 73
7.O UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI. 73
7.1. Utangulizi 73
7.2 Aina ya hati za ukaguzi 74
7.3 Hati inayoridhisha isiyokuwa na masuala ya msisitizo..... 78
7.4 Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo 78

7.5 Hati yenye shaka 78
7.6 Hati isiyoridhisha 78
7.8 Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo 79
7.9 Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa zilizopata hati zenye shaka 121

www.JamiiForums.com

SURA YA 8 140
MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO 140
8.1 Majumuisho 140
8.2 Mapendekezo 140
9.0 Viambatisho 156

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano
Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Dira
Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

Dhima
Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

1) **Uadilifu:** sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.

2) **Ubora:** sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi

3) **Uaminifu:** tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.

4) **Mtazamo wa watu:** tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.

5) **Uvumbuzi:** sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.

6) **Matumizi bora ya rasilimali**: sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

Vifupisho

A/C	Akaunti
ACGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
Act	Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CDTI	Taasisi ya Maendeleo ya Jamii na Mafunzo
CFS	Taarifa Jumuifu za Fedha
CPO	Ofisi Kuu ya Malipo
FDCS	Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi
HIV	Upungufu wa Kinga Mwilini
IFMS	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha
INTOSAI	Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi kuu za Ukaguzi wa Hesabu
ISA	Viwango vya Ukaguzi wa Hesabu vya Kimataifa
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
LART	Mfuko wa Kusimamia Mikopo na Ufuatiliaji wa Madeni
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
NAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu
PFA	Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya 2001
PFMRP	Programu ya Marekebisho ya Usimamiaji Fedha za Umma
PFR	Kanuni za Fedha za Umma
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
PPA	Sheria ya Manunuzi wa Umma Na. 21 ya 2004
RAS	Sekretarieti za Tawala za Mikoa
RCCB	Daftari la Kukusanyia Maduhuli
Reg.	Kanuni
Sect.	Kifungu
SUMA	Shirika la Uchumi na Maendeleo
TANSORT	Shirika la Kuchambua Almasi la Serikali ya Tanzania
TCAA	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania
UNESCO	Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa
URT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
USD	Dola za Kimarekani
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden
PAA	Sheria ya Ukaguzi wa Umma

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

DIBAJI

Kwa kipindi cha miaka mitano, jamii imeanza kuona maboresho katika mchakato wa uwajibikaji nchini. Sio tu kwamba maboresho haya yametokana na ripoti zangu za ukaguzi za kila mwaka, lakini pia ni kwa sababu ya utashi wa kisiasa uliowekwa na uongozi wa awamu ya nne ya serikali chini uongozi wa Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete na michango ya kimaendeleo inayotolewa na Bunge la Jamhuri wa Tanzania kupitia kamati zake za kudumu ambazo zimesimamia na kuhimiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Ninapenda kutoa shukrani zangu kwa wale wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kuniwezesha kutimiza majukumu yangu ya kikatiba na hatimaye kutoa ripoti hii kwa wakati.

Ripoti hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu 34(1)(c) cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Kwa mujibu wa Ibara 143 (2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila ripoti anayotoa chini ya Ibara 143 (2). Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais ataagiza wanaohusika waziwasilishwe ripoti hizo mbele ya Kikao cha kwanza cha Bunge ikiwezekana ndani ya siku saba baada ya kuanza kwa kikao.

Uhuru wa kiutendaji wa ofisi yangu kwa kiasi kikubwa umeimarika baada ya kuanza kutumia sheria ya Ukaguzi wa Umma Na 11 ya mwaka 2008. hata hivyo kulingana na viwango vya kimataifa maboresho zaidi yanahitajika hasa kwa upande wa kupanga mishahara na ajira za watumishi wa ofisi yangu ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba kwa ufanisi zaidi.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kumeongeza mawanda ya ukaguzi wangu kwa kunipa madaraka ya

www.JamiiForums.com

kufanya kaguzi nyingine zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha. Kwa mujibu wa sheria hii natakiwa kufanya ukaguzi wa ufanisi, utambuzi na mazingira na kaguzi mbalimbali maalum kama zinavyojitokeza. Ni matumaini yangu kwamba, kwa kuanzishwa kwa sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma, Ofisi yangu itaweza kuimarisha udhibiti wa fedha na kuisaidia Serikali kuimarisha uwajibikaji. Sheria hii pia itaniwezesha kuwa huru katika kulithibitishia Bunge masuala yanayohusu uwajibikaji, uwazi na matumizi bora ya rasilimali hasa kuona kwamba rasilimali hizo zimetumika vizuri kwa kuzingatia uchumi, ufanisi na kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge.

Ni vyema kutambua kuwa wakati ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za Umma na hasa Serikali Kuu, lakini wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Bunge na watanzania kwa ujumla wanatarajia kuona kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika Serikali Kuu kuhusiana na ufanisi na ubora na usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo kuhusu uimarishaji na uboreshaji wa sekta ya Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu na Ofisi yangu zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma.

Ingawa majukumu ya ofisi yangu na yale ya taasisi za umma yanatofautiana, hata hivyo matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma wa Tanzania kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia maendeleo katika sekta ya Umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tutaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya Umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

www.JamiiForums.com

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC), moja kati ya kamati za Kudumu za Bunge, imefanya kazi kubwa ya kuboresha utendaji wa Maafisa Masuuli wa Serikali Kuu ambao utendaji wao haukufikia matarajio ya Kamati hiyo. Pamoja na jitihada hizo, ninaamini kuwa Serikali Kuu ina jukumu muhimu katika kuboresha usimamizi wa fedha za Umma.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa utaalamu juhudi kubwa walioonyesha katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, mishahara duni na upungufu wa watumishi, na wakati mwingine kufanya kazi maeneo ya vijijini ambayo sio rahisi kufikika.

Napenda pia kutambua kazi iliyofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali na Msajili wa Hazina kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za kiutendaji za Taasisi zilizoko chini yao kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 na kuonyesha mambo mengi ambayo kwa kiasi kikubwa yalijitokeza kwenye ripoti yangu ya mwaka uliopita. Nipenda kuzitambua kazi zilizofanywa na Taasisi hizi ambazo nimeona ni vyema nikazijumuisha kwenye ripoti yangu.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu kwa siku zijazo.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
Dar es Salaam.

Machi, 2011

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Kwa mara nyingine, napenda kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wote wa Ofisi yangu kwa kuniwezesha kutoa ripoti hii kwa wakati. Ninawajibika kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa kutuvumilia kwa kutokuwa nao kwa muda mrefu wakati tukikamilisha majukumu haya ya kikatiba.

Vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la Maendeleo la Sweden, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP) na wote wenye mapenzi mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha Ofisi yangu. Mchango wao umekuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza na kukuza raslimali watu, nyezo za kazi (magari), mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na vitendea kazi. Hata hivyo, bado misaada zaidi inahitajika kwa ajili ya kuboresha kazi za ukaguzi katika sekta ya umma kwa kuzifanya kuwa za kisasa zaidi. Jambo hili lingeweza kwenda haraka endapo angepatikana mfadhili wa kugharamia ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Ukaguzi kitakachojengwa Gezaulole katika Manispaa ya Temeke.

Aidha, natoa shukrani zangu kwa Hazina, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma, Mhakiki Mali Mkuu na wadau wote kwa taarifa mbalimbali muhimu walizonipatia ili kukamilisha kazi hii. Pia namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuniwezesha kutoa ripoti kwa wakati.

Kwa kumalizia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Umma popote pale walipo Tanzania Bara, wawe ni wa Serikali Kuu au Halmashauri bila ya kuwasahau walipa kodi ambao ndio walengwa wa ripoti hii. Michango yao imekuwa msaada mkubwa katika ujenzi wa Taifa ambao hauwezi kupuuzwa hata kidogo.

Naomba Mungu awabariki wote kwa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2010/2011

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihusuyo Taarifa za Fedha za Serikali Kuu imelenga maeneo yafuatayo:

(A) Utangulizi
(B) Mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa
(C) Udhaifu niliogundua katika mifumo wa udhibiti wa ndani
(D) Mapungufu katika mchakato wa manunuzi
(E) Masuala ya kodi
(F) Masuala yahusuyo malipo ya wastaafu
(G) Hitimisho na mapendekezo

A: Utangulizi

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa Taarifa za Fedha katika Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Mawanda ya ukaguzi katika Serikali Kuu yanajumuisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa. Hata hivyo, taarifa za ukaguzi wa Ofisi za Balozi zitawasilishwa katika taarifa inayojitegemea kutokana na kuchelewa kwa zoezi la ukaguzi lililosababishwa na kutopatikana fedha mapema kutoka Hazina kwa ajili ya ukaguzi huo.

B: Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa

Matokeo ya ukaguzi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 yanaonyesha kuboreka kwa hati zilizotolewa kwa Serikali Kuu na Taasisi zake ikilinganishwa na mwaka uliopita kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Aina	Hati za kuridhisha			Hati zenye shaka			Hati zisizoridhisha			Hati chafu			Jumla		
Mwaka wa fedha	2008/ 2009	2009/ 2010	2010/ 2011	2008/ 2009	2009/ 2010	2010/ 2011	2008/ 2009	2009/ 2010	2010/ 2011	2008/ 2009	2009/ 2010	2010/ 2011	2008/ 2009	2009/ 2010	2010/ 2011
MDAs	45	43	50	7	13	10	1	1	0	-	-	-	53	57	60
RAS	18	12	19	2	7	2	1	1	0	-	1	-	21	21	21
Jumla	63	55	69	9	20	12	2	2	0	-	1	-	74	78	81
Asilimia	85	71	85	12	26	15	3	2	0	0	1	0	100	100	100

Jedwali linaonyesha kwamba hati za kuridhisha zimeongezeka kutoka asilimia 71 mwaka 2009/2010 hadi asilimia 85 mwaka 2010/2011 wakati hati zenye shaka zimepungua kutoka asilimia 26 mwaka 2009/2010 hadi asilimia 15 mwaka 2010/2011.

www.JamiiForums.com

Matokeo ya ukaguzi kwa mwaka huu yamebaini kutokuwepo kwa hati isiyoridhisha ilihali hati 2 zilizotolewa mwaka 2009/2010. Vilevile, matokeo ya ukaguzi yanaonyesha kutowepo kwa hati mbaya ikilinganishwa na hati 1 iliyotolewa mwaka 2009/2010.

Kwa kuwa mwelekeo wa hati za ukaguzi umeonyesha kuboreka ikilinganishwa na mwaka jana, natoa ushauri kwa uongozi katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa pamoja kutorejea katika hali ya miaka ya nyuma na badala yake kuendeleza mafanikio yaliyokwishapatikana katika usimamizi wa fedha na mali za umma.

C: Dosari tulizozikuta wakati wa ukaguzi

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu tumeendelea kukutana na dosari mbalimbali ambazo maelezo ya kina yametolewa katika sura husika. Dosari hizo ni pamoja na kufotuatwa sheria mbalimbali, kutokuwepo kwa mifumo ya udhibiti ya ndani madhubuti, aidha kama mifumo ipo kutozingatiwa kwa mifumo hiyo. Masuala muhimu yanayohusiana na dosari hizo ambayo yako katika taarifa yangu ni haya yafuatayo:

- Kutofuatwa kikamilifu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS)
- Kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za 2005
- Kutotekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi niliyoyatoa katika miaka iliyopita.
- Malipo ya zaidi ya Sh.8,076,574,791 yalifanywa bila nyaraka sahihi na bila kuwa na maelezo ya kuthibitisha uhalali wake.
- Bidhaa zilizonunuliwa na kulipwa lakini hazijapokelewa hadi wakati wa kuandika taarifa hii Sh.31,027,797,820
- Mishahara ya jumla ya Sh.142,715,828 ililipwa kwa watumishi ambao hawako kwenye utumishi wa Umma.
- Madai mara mbili ya malipo ya uzeeni (pensheni na mafao ya mikataba) kinyume na sheria za pensheni.

www.JamiForums.com

- Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 38 kutoka Sh.10,503,806,011,885 mwaka 2009/2010 hadi Sh.14,441,617,939,770 mwaka 2010/2011
- Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, Hesabu Jumuifu za Taifa zilionyesha Sh.461,586,713,035 (Mkopo Sh 579,280,687,763) kama dhamana za Serikali. Kwa wastani, kiasi hiki cha dhamana ni sawa na asilimia 96.8% ya mikopo yote iliyotolewa. Huu ni ukiukaji wa Kifungu cha.13 (1) (b) cha sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali ya 1974 (iliyorekebishwa 2004), ambayo inaeleza dhamana zisizidi 70% ya fedha zote zilizokopwa.
- Hadi tarehe 30 Juni 2011 kiasi cha Sh.17,589,570,021 ikiwa ni fedha za msaada kwa wanaoagiza bidhaa nje zilikuwa bado hazijarudishwa na waliozichukua. Kwa maoni yangu, taratibu na mbinu zinazotumiwa na Serikali katika kukusanya fedha hizi zinaonekana kutokuzaa matunda yoyote pamoja na kuingia mkataba na M/s Msolopa Investment tangu tarehe 17 Novemba 2008 kwa ajili ya kukusanya fedha hizo.
- Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2011 wizara, idara za serikali, na sekretariati za mikoa zilikuwa na madeni na miadi inayofikia jumla ya Sh.1,327,139,369,086
- Matokeo ya uhakiki wa madai ya wazabuni na watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi uliofanyika kuanzia 04/05/2010 hadi 06/06/2010 ilionyesha kwamba kati ya kiasi cha Sh.26,899,351,638 kilichowasilishwa, madeni ya Sh.23,471,015,604 yalikubaliwa na kiasi kilichobaki cha Sh.3,428,336,033 hakikukubalika kwa sababu mbalimbali.
- Taarifa za fedha za wizara, idara za serikali na wakala wa serikali saba (7) zinazoishia 30 Juni 2011 zinaonyesha vifaa vya kudumu vyenye thamani ya Sh.70,854,983,288 havijaingizwa kwenye daftari la vifaa.
- Kiasi cha Sh.577,537,084,848 kilionyeshwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kikiwa ni madeni yasiyolipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011. Kiasi hiki kinawakilisha ongezeko la asilimia 259% ikilinganishwa na kiwango cha mwaka uliopita cha Sh.107,063,198,140. Kwa hiyo,

www.JamiiForums.com

matumizi ya jumla kwa mwaka yalionyeshwa pungufu kwa kiasi sawa na madeni hayo. Huu ni ukiukwaji wa msingi wa uhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu.

D: Dosari zilizobainika katika mchakato wa manunuzi

Matokeo ya ukaguzi uliofanya na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) umeonyesha wastani wa kiwango cha uzingativu wa sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 kufikia asilimia 64. Kiwango hiki kimekokotolewa kutokana na vigezo 13 vya uzingativu ambavyo maelezo yake yako katika sura ya 5 ya taarifa hii.

Uzingativu wa Sheria ya Manunuzi katika Taasisi za manunuzi (PEs) zilizokaguliwa na PPRA kilikuwa chini ya wastani (chini ya 50%) katika Wizara, Idara na Wakala wa serikali zote zilizokaguliwa. Matokeo haya yanatokana na vigezo vitano vilivyoangaliwa ambavyo ni: Kuwepo kwa Kitengo cha Manunuzi na uwiano wa wataalam wenye sifa stahiki; Kuandaliwa kwa mipango ya mwaka ya manunuzi; Kutangazwa kwa zabuni zilizotolewa; Utunzaji nyaraka na Udhibiti wa ubora. Kwa upande mwingine, kiwango cha uzingatifu kilikuwa juu ya wastani (50% na zaidi) katika vigezo nane vifuatavyo: Kuanzishwa kwa bodi za zabuni na muundo wake; Utendaji wa Maafisa wahasibu, Bodi za Zabuni na Vitengo vya Manunuzi; uzingatifu wa viwango vya uidhinishaji wa manunuzi; Utangazaji wa Zabuni; Muda wa kuandaa tangazo la zabuni; Utumiaji njia sahihi ya kufanya manunuzi; Matumizi ya nyaraka sahihi za zabuni kama zilivyoelezwa katika Kanuni za Manunuzi za mwaka 2005; na Utekelezaji wa mikataba.

E: Masuala ya Kodi

Matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania yamejumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa katika Sura ya 3 ya taarifa hii. Mambo muhimu yaliyojitokeza kuhusiana na ukusanyaji wa kodi ni kama ifuatavyo:

www.JamiiForums.com

- Kumekuwepo na masuala ya taarifa za ukaguzi za miaka ya nyuma ambayo hayajashughulikiwa yenye thamani ya kiasi cha Sh.236,459,698,078 na Dola za Kimarekani 50,565,602.
- Hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania Bara zimeonyesha makusanyo ya kiasi cha Sh.5,550,205,244,378 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.5,849,093,700,000 na kusababisha makusanyo pungufu ya Sh.298,888,455,622

- Taarifa za mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania zilionyesha misamaha iliyotolewa kwa Taasisi mbalimbali yenye thamani ya Sh.1,016,320,300,000 sawa na asilimia 18 ya makusanyo yote. Katika hali halisi, kama kiasi cha Sh.1,016,320,300,000 kisingesamehewa, Mamlaka ya Mapato Tanzania ingekusanya Sh.6,566,525,544,378 ambazo ni sawa na Sh. Sh.717,431,844,378 zaidi ya kiasi kilichokadiriwa kukusanywa.

  Kwa upande wa Hesabu Jumuifu za Taifa, matokeo muhimu yalijumuisha masuala yafuatayo:

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Kuongezeka kwa Deni la Taifa	3,937,811,927,885
Mikopo iliyotolewa na serikali ambayo haijarejehswa	480,229,660,682.00
Mihadi isiyolipwa	79,113,403,430
Madeni yamkini	30,408,060,580
Madeni yasiyolipwa	577,537,084,848
Dhamana za serikali	461,586,713,035
Uwekezaji wa Serikali	11,410,408,210,579
Malimbikizo ya potevu za serikali	7,998,801,086
Fedha zilizolipwa zaidi kaitika mfuko wa serikali mpaka tarehe 30 Juni, 2011	548,332,614,000

Aidha, pamekuwepo na udhaifu katika kuhifadhi taarifa zinazohusiana na uwekezaji na dhamana za Serikali.

www.JamiiForums.com

F: Masuala yahusuyo malipo ya mafao ya uzeeni

Kwa vile udhibiti wangu unanitaka kufanya ukaguzi wa mafao ya wastaafu, sura ya nne ya taarifa hii inaonyesha matokeo muhimu ya ukaguzi wa awali niliyofanya katika kipindi husika. Ukaguzi ulibaini kwamba:-

- Kiasi cha malipo kwa wastaafu kingelipwa zaidi ya kile kinachostahili kwa Sh.539,201,733 kama malipo hayo yasingehakikiwa.
- Wastaafu wangepunjwa malipo ya kustaafu kwa kiasi cha Sh.106,007,774 kama madai yao hayangehakikiwa.

Matatizo makubwa yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa mafao ya wastaafu ni kama ifuatavyo:

(i) Matatizo ya kiuendeshaji
(ii) Kutoa tafsiri isiyokuwa sahihi ya sheria za pensheni, kanuni zake na sheria nyingine
(iii) Matatizo ya kiutawala

Masuala muhimu yaliyojitokeza kutokana na ukaguzi huo ni haya yafuatayo:

- Kutotumia viwango sahihi katika ukokotoaji wa mafao ya wastaafu.
- Kudai mara mbili malipo ya kiinua mgongo.
- Kuchanganya masharti ya ajira za kudumu na za mikataba
- Kuchelewa kuwasilisha karatasi za mafao ya uzeeni kwa ukaguzi.
- Maamuzi yanayokinzana kwa baadhi ya watumishi yasiyoendana na sheria za pensheni.
- Kutozingatiwa kwa sheria za pensheni
- Ucheleweshaji wa kuwasilisha madai ya pensheni kwa ajili ya ukaguzi
- Kuwasiliha nyaraka zisizokamilika
- Kutokuwa na stahili za kulipwa mafao ya uzeeni
- Utoaji maamuzi yenye utata (unaokinzana)

www.JamiiForums.com

G: Hitimisho na mapendekezo

Mwisho, kwa mujibu wa madaraka niliyopewa chini ya Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, nimetoa mapendekezo kadhaa katika Sura ya 8 ya taarifa hii ambayo kama yatatekelezwa yatasaidia kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Umma katika nchi yetu. Mapendekezo hayo yanajumuisha:-

- Utekelezaji wa mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma haujazingatiwa ipasavyo na serikali. Hivyo napendekeza utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa wakati ili kuleta ufanisi na uwajibikaji. Nashauri Maafisa masuuli wazingatie sheria pamoja na uandaaji wa taarifa mbalimbali ili kuweka uwazi na uwajibikaji ndani ya serikali.
- Madeni ya jumla ya Sh.1,327,139,369,086 yatambuliwe na kuingizwa katika Taarifa Jumuifu za Fedha.
- Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuboresha nidhamu katika matumizi ya Serikali.
- Maafisa Masuuli waimarishe michakato ya manunuzi, ikiwa ni pamoja na kuingia na kusimamia mikataba yenye tija kwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi ili kupata thamani ya fedha.
- Serikali iboreshe utaratibu za malipo ya mwisho ya wastaafu ili yalipwe haraka na kwa ufasini.

www.JamiiForums.com

SURA YA 1

1.0 Utangulizi

Taarifa hii inatolewa kufuatia ukaguzi wa hesabu na kumbukumbu nyingine za Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozi kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34(1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011.

1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Umma

Kutokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapaswa kukagua kumbukumbu za taarifa zote za hesabu za fedha katika Ofisi zote za Umma, Mahakama na Mamlaka zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania na kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais ambaye atahakikisha zinawasilishwa mbele ya Bunge.

Katika kutimiza wajibu huu, kutokana na Kifungu Na. 10 cha Sheria Na 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ninatakiwa kujiridhisha kwamba:-

- Tahadhari inachukuliwa ili kuhakikisha kwamba fedha za Umma zinakusanywa na kutunzwa kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa.

- Fedha zote kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimeidhinishwa na kutolewa kufuatana na Sheria ya Matumizi ya Bunge ya mwaka husika.

- fedha zote zimetolewa chini ya mamlaka sahihi na kuwa zimetumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na mamlaka hiyo na, kanuni zipo za kutosha kwa ajili ya kuwaongoza watunza vifaa namna ya kuweka vitabu sahihi. Aidha, nina wajibu, kwa mujibu wa kifungu hicho cha sheria kumjulisha Rais na Bunge juu ya

www.JamiiForums.com

uwepo wa matumizi mabaya ya fedha na mali za Umma.

1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Wajibu wa kisheria wa Ofisi yangu katika kukagua hesabu za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa umebainishwa chini ya Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Kutokana na Sheria hiyo, ninawajibika kuchunguza, kukagua na kutoa taarifa juu ya hesabu za Wizara na Idara za Serikali na Maafisa Masuuli, na watu wote waliokabidhiwa jukumu la kukusanya, kupokea, kutunza, kutoa au kuuza, kuhamisha na kutoa stakabadhi, dhamana, vifaa au mali nyingine za Umma. Pia, jukumu langu linahusu Mashirika yote ya Umma na Taasisi nyingine, Mamlaka yoyote au Taasisi inayopokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, au Taasisi yoyote ambayo imeruhusiwa kisheria kukaguliwa na Ofisi yangu.

1.3 Muundo wa Kazi za Ukagui Ndani ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi, ambao ulifanywa na Ofisi yangu nchini kote katika mwaka husika

Taarifa hii inatoa kwa muhtasari matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi ambalo lilifanywa na Ofisi yangu nchini kote kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2011. Ili ofisi yangu iweze kushughulikia kwa ufanisi zaidi kazi hii kubwa ya kukagua Wizara zote, Wakala na Sekretarieti za Mikoa nchini, nimeweka ofisi katika kila Wizara na Mikoa ya Tanzania Bara kwa madhumuni ya usimamizi mzuri wa kazi.

www.JamiiForums.com

Ofisi hizi za Mikoa na Wizara zinasimamiwa na Wakaguzi wa Hesabu Wakazi ambao wanawajibika kwa Wakaguzi wa Hesabu wa Kanda.

Tumeona ni vyema kugawa wakaguliwa wetu katika Kanda ambazo zinaongozwa na Wakaguzi wa Kanda ili kurahisisha usimamizi wa kaguzi zinazofanywa chini yao. Ili kuhakikisha ufanisi katika ukaguzi, wizara na taasisi zimegawanywa katika Kanda 11, na kila kanda inaongozwa na Mkaguzi wa Kanda.

1.4 Ukaguzi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa

Mwezi Disemba mwaka jana (2011), Mkutano Mkuu Maalumu wa Umoja wa Mataifa uliiteua Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Tanzania kujiunga na Bodi ya Ukaguzi wa Hesabu ya Umoja huo (United Nations Board of Auditors - UNBOA) kujaza nafasi itakayoachwa wazi wakati Afrika ya Kusini itakapomaliza muda wake tarehe 30 Juni , 2012.

Nimeteua maafisa wawili kutoka ofisi yangu kufanya kazi katika ofisi ya Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa iliyoko New York, na wengine kadhaa watakuwa Tanzania ambao watakagua taasisi za Umoja wa Mataifa zilizopo duniani kote kama zilivyogawanywa kati ya wanachama watatu wa Bodi hiyo ambao ni Tanzania, China na Uingereza.

Napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa msaada niliopewa mimi binafsi na ofisi yangu wakati wa mchakato mzima ambao umetufanya kuteuliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kazi hii muhimu ambayo italiweka jina la Tanzania katika medani ya Kimataifa.

1.5 Mawanda na viwango vya Ukaguzi vinavyotumika

1.5.1 Mawanda ya ukaguzi

Mawanda ya ukaguzi kwa kifupi yanahusisha ukusanyaji wa maduhuli, uidhinishaji wa matumizi kwa kufuata

www.JamiiForums.com

sheria ya Bunge, utekelezaji wa miradi, utendaji wa Hazina na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ukaguzi ulifanyika ili kujiridhisha kwamba kulikuwepo na uzingatiaji wa kanuni zilizopo, kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji na kubainisha baadhi ya kasoro zilizojitokeza, kupitia ripoti mbalimbali.
Wakati wa ukaguzi, hoja zote zilizojitokeza ziliwasilishwa kwa menejimenti za Wizara, Mikoa na Miradi iliyokuwa inakaguliwa kwa ajili ya kutolea maelezo. Maafisa Masuuli wanapewa fursa ya kuzitolea ufafanuzi hoja na mapendekezo ya ukaguzi kabla ya kuingizwa kwenye ripoti.

1.4.2 Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI) na Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi Kanda ya Africa kwa nchi zinazoongea kingereza (AFROSAI-E). Hivyo basi inatumia viwango vya ukaguzi vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) na vile vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC) ambalo Tanzania ni mwanachama kupitia Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu. Pia ninayo furaha kueleza kwamba Tanzania (kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu) kwa sasa ndiye Mwenyekiti wa AFROSAI-E kuanzia Aprili 2011 kwa kipindi cha miaka mitatu. AFROSAI-E inajumuisha wanachama kutoka nchi 24 za Afrika.

1.6 Sera ya Kiuhasibu

Kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004), Serikali imeweka taratibu za kihasibu ili kuhakikisha kwamba raslimali zinazoidhinishwa na Bunge zinatumika kwa usahihi. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004), Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikiksha kwamba mapato yote ya

www.JamiForums.com

Umma yanaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia malipo kutoka kwenye Mfuko huo yataidhinishwa kwa Sheria ya Bunge ya Matumizi kwa mwaka husika.

Huu ni mwaka wa nne tangu serikali ianze kuandaa Taarifa za Fedha kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa mising ya fedha taslimu [(IPSAS) -cash basis of accounting]. Chini ya msingi huu mapato ya Serikali hayatambuliwi mpaka zitakapopokelewa fedha taslimu. Hali kadhalika matumizi hutambulika pale tu malipo yanapofanyika.
Kifungu cha 25(i) hadi (j) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inatoa ufafanuzi wa wa hesabu na taarifa zinazotakiwa kuandaliwa na Maafisa Wahasibu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

1.7 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na Sekretareti za Mikoa wana majukumu ya kusimamia rasilimali za Umma kwenye maeneo yao ya kazi. Kazi na majukumu ya Maafisa Masuuli kama ilivyoainishwa chini ya kifungu Na 8 cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ni kuwajibika na kulinda mali za umma zilizoko chini ya maeneo yao. Katika kulinda rasilimali zilizoko chini yao, ni muhimu kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mifumo ya udhibiti wa ndani madhubuti na inayofuatwa muda wote kufanya kazi.

1.8 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Udhibiti wa ndani unalenga jinsi rasilimali za Serikali zinavyoelekezwa, kusimamiwa na kupimwa. Kwa maana nyingi mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani unayo nafasi kubwa katika kuzuia na kugundua ubadhirifu/matumizi mabaya na kulinda rasilimali za Umma zinazogusika na zisizogusika.

www.JamiiForums.com

Uwekaji wa mfumo wa ndani madhubuti ni muhimu na niwajibu wa menejimenti ya taasisi husika.

1.9 Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi

Jukumu la kutayarisha na kuwasilisha hesabu za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni wajibu wa Maafisa Masuuli wa Serikali Kuu (Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa). Kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004); inataja aina ya hesabu mbalimbali anazotakiwa kutengeneza Mhasibu Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli na Maafisa wengine wa Serikali waliokasimiwa Mifuko Maalumu iliyoanzishwa kisheria. Pia, Kifungu cha 25(4) cha sheria hiyo hiyo kinataka taarifa za fedha ziandaliwe kulingana na mifumo ya kihasibu iliyokubalika kimataifa na ni lazima misingi ya kihasibu iliyotumika iwekwe bayana. Kwa mwaka wa pili katika historia, taarifa za fedha za Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma ambayo inalandana na matakwa ya kanuni Na. 53 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). Aidha, utaratibu huo umeanza katika Balozi kwa mara ya kwanza mwaka huu wa fedha.

Kanuni ya 8 (5) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) inataka kila Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kutengeneza na kutoa kwa Umma taarifa ya utekelezaji ya mwaka inayoeleza mikakati ya bajeti, aina na malengo ya kila mpango/programu, tathmini ya matokeo na mafanikio yakilinganishwa na malengo yaliyowekwa. Pia, Maafisa Masuuli wanatakiwa kutengeneza muhtasari wa matokeo ya matumizi ya fedha, kwa mwaka wa fedha unaohusika na kwa mfumo ulioidhinishwa na Mhasibu

www.jamii-forums.com

Mkuu wa Serikali, mipango ya mwaka ujao kama ilivyoidhinishwa na Bunge na mipango ya muda wa miaka miwili inayofuata. Baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikutimiza wajibu huu.

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

SURA YA 2

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YATOKANAYO NA HOJA ZA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

2.0 Utangulizi

Sura hii inaonyesha matokeo ya tathmini iliyofanyika katika kipindi cha ukaguzi na ni jinsi gani Serikali imetekeleza mapendekezo yatokanayo na hoja za ukaguzi kwa miaka iliyopita yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia ripoti jumuifu na za kina kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa.

Matokeo ya tathmini yalikuwa katika maeneo yafuatayo:

i. Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa katika ripoti jumuifu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

ii. Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa masuuli /Wakuu wa vitengo yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

iii. Majibu ya taarifa za Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) yaliyowasilishwa kwenye ripoti jumuifu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

iv. Majibu ya hoja zitokanazo na ukaguzi wa taarifa jumuifu za hesabu za Serikali.

www.JamiiForums.com

2.1 Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ripoti za Serikali Kuu kwa miaka ya nyuma

(a) Mapendekezo mengi yaliyotolewa katika ripoti ya Serikali Kuu kwa miaka iliyopita hayakutekelezwa na Serikali. Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali hayazingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Nazidi kusisitiza kwa Serikali kutekeleza mapendekezo ambayo yalilenga kuboresha moja kwa moja mifumo na michakato mbalimbali pamoja na kuepusha madhara kwa mambo ambayo yana yanayoendelea kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:-

2008/2009	Maelezo
10.2 (i)	**Mapitio ya utaratibu wa kubakiza maduhuli yaliyokusanywa** • Mapitio ya utaratibu wa kubakiza maduhuli yaliyokusanywa ili kuhakikisha kwamba Balozi zinawasilisha salio la maduhuli katika Mfuko Mkuu wa Hazina akaunti Na.14:50 ili kufidia pengo litokanalo na upungufu wa bajeti zake hayakutekelezwa kulingana na mapendekezo yaliyotolewa kipindi kilichopita. • Uhamisho wa fedha kutoka katika Ofisi Ndogo za Ubalozi kwenda katika Balozi nyingine udhibitiwe na Wizara ya Fedha na Uchumi.
10.2(iii)	**Usimamizi mbaya wa mali za Serikali** Matatizo ambayo yanasababisha mashine za

www.JamiiForums.com

	kuchapisha Visa zisitumike kikamilifu katika balozi nyingi ambayo hayakupatiwa ufumbuzi ni kama yafuatayo: a) Ukiritimba katika kupata haki ya kufanyia matengenezo ya mashine za kuchapisha Visa b) Ugumu wa matengenezo pale zinapoharibika c) Uwezo mdogo wa kutumia mashine za kuchapisha Visa
10.2(v)	**Kufanyiwa marekebisho kanuni za utumishi za 1979 balozini** Mapendekezo ya kufanyia marekebisho Kanuni za Utumishi za mwaka 1979 katika Balozi za Tanzania nchi za nje ili ziendane na wakati uliopo hayakutekelezwa.
10.2(vi)	**Umiliki wa ardhi na majengo** Hati miliki ya ardhi na majengo yanayomilikiwa na Balozi za Tanzania London, Nairobi na Maputo mpaka sasa hazijapatikana pamoja na mapendekezo kutolewa katika ukaguzi kwa miaka iliyopita.
10.2(xi)	**Masuala ya Kodi** • Matokeo ya ushauri kwa uongozi wa Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji Mkuu kuhusiana na kesi au rufaa zote za kodi kushughulikiwa na Bodi ya Rufaa za Kodi kama zinavyoonyeshwa katika sheria ya rufaa ya kodi namba. 15 ya mwaka 2000 hayajatekelezwa kama nilivyopendekeza na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. • Sijawahi kuridhishwa na hatua zinazochukuliwa

www.JamiiForums.com

	na Serikali katika kuimarishwa Mfumo wa uangalizi na udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuhakikisha kuwa marejesho ya mapato na malipo ya kodi vinapitiwa kwa makini ili kubaini udanganyifu na mianya ya ukwepaji kodi kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na kodi na kuzuia matumizi mabaya ya fedha za Serikali. • Serikali haijaweza kuchunguza kwa umakini sababu zilizofanya Mamlaka ya Mapato Tanzania ishindwe kukusanya kiasi kilichokadiriwa katika bajeti yake, na kwa kushauriana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ije na hatua madhubuti zitakazoondoa tatizo hilo la kutofikia malengo katika ukusanyaji mapato.
2009/2010	Ukaguzi wa orodha za malipo ya mishahara mwaka huu umeonyesha kuwa Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa nane (8) zililipa jumla ya Sh.1,842,607,565.29 kama mishahara kwa wastaafu, wasiokuwa kazini na wasiokuwa na stahili kwa vile hawakuwa tena kazini.
5.2	**Matengezezo ya magari katika karakana zisizoidhinishwa na TEMESA Sh.176,722,089** Hakuna hatua zilizochukuliwa kurekebisha udhaifu ulioripotiwa katika ukaguzi uliopita ambapo matengenezo ya magari ya Serikali yanafanyika katika karakana binafsi za magari ambazo hazijaidhinishwa na TEMESA Hata hivyo, karakana binafsi za magari ambazo hazijaidhinishwa na TEMESA zimeendelea kufanya matengenezo ya magari kinyume na taratibu za manunuzi ya umma.
5.4	**Ununuzi wa samani kwa maafisa wasiokuwa na stahili**

www.JamiiForums.com

	Serikali haijatoa waraka wowote wala kuchukua hatua zozote kwa uongozi wa Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa ambazo zilifanya manunuzi ya samani kwa maafisa wasiokuwa na stahili ya kiasi cha Sh.650,714,800 kwa ajili ya nyumba binafsi badala ya zile za Serikali kinyume na matakwa ya waraka wa UTUMISHI,(Waraka namba C/CA/134/213/01/G/69 wa 30/01/2006
5.7	**Malipo yaliyofanyika kutoka katika vifungu visivyohusika Sh.5,296,243,598** Hakuna hatua zilizochukuliwa kuzuia Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na balozi kwa kufanya malipo ya kiasi cha sh.5,296,243,598 kutoka katika vifungu visivyohusika kinyume na sheria ya fedha za umma.
	Maamuzi ya upendeleo ya kutoa kiwango cha chini cha mrabaha wa mazao ya misitu kuliko kiwango cha sheria ya misitu (CAP 323) na Kanuni za misitu za mwaka 2007 bila kibali cha mamlaka husika hayajapatiwa ufafanuzi na Wizara ya Maliasili tangu kufanyika kwa ukaguzi uliopita.

2.2 Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli /Wakuu wa vitengo yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ofisi za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zimekuwa na maendeleo mazuri katika utekelezaji wa masuala ya kaguzi za nyuma.Hata hivyo, katika mwaka huu wa ukaguzi, Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa 58 zilikuwa hazijashughulikia masuala ya miaka ya nyuma yenye jumla ya, Sh.543,364,747,075.99 JPY 16,351,520,096.94 and Dola za Kimarekani 91,580. Kati ya kiasi hicho, Hazina inaongoza kwa kiasi kikubwa cha JPY16,351,520,096.94 ikifuatiwa na Wizara ya Ujenzi yenye Sh.390,447,292,901 wakati Idara ya

www.JamiiForums.com

Huduma za Magereza ikiwa ya tatu yenye Sh.34,836,336,257.**(Kiambatisho Na.I)**
Lengo la kuwasilisha matokeo ya ukaguzi pamoja na mapendekezo kwa mkaguliwa ni kumsaidia mkaguliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika usimamizi wa fedha na udhibiti wa mali katika Wizara, Idara,Wakala na Sekretarieti za Mikoa . Kutojibiwa kwa hoja na mapendekezo ya ukaguzi kutokufanyiwa kazi kama inavyoonekana katika Wizara, Idara,Wakala na Sekretarieti za Mikoa ni kosa kubwa kwa Maafisa Wahasibu wa taasisi hizo na uongozi wa Wizara, Idara,Wakala na Sekretarieti za Mikoa husika**.**

Kutoshughulikiwa kwa hoja na mapendekezo ya ukaguzi kunasababisha kasoro zilizojitokeza wakati wa ukaguzi kujirudia katika miaka inayofuata. Pia, hii inaonyesha kutowajibika kikamilifu kwa Maafisa Wahasibu na uongozi wa taasisi husika.

Mchanganuo huu unaonyesha kwamba Menejimenti za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikufanya jitihada za kutosha kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi. **Kiambatisho Na.I** katika ripoti hii ni orodha ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa na thamani ya masuala ya nyuma yasiyoshughulikiwa.

Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo zilikuwa hazijashughulikia masuala ya miaka ya nyuma zimeongezeka kutoka 46 mpaka 58 zenye jumla ya Sh.543,364,747,075.99 JPY 16,351,520,096.94 na Dola za Kimarekani 91,580 ukilinganisha na Sh.468,627,883,842 katika mwaka 2009/2010.

Mchanganuo huu unaonyesha kwamba Menejimenti za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikufanya jitihada za kutosha kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi. Orodha ya masuala ya miaka ya nyuma

www.jamiiforums.com

yasiyojibiwa yako kwenye Kiambatisho Na. I katika ripoti hii.

2.3 Mamlaka ya Mapato Tanzania

Hadi kufikia wakati wa kutoa taarifa yangu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (Disemba 31, 2011); Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa na masuala mbalimbali ya ukaguzi yaliyoripotiwa katika taarifa zilizopita yaliyofikia kiasi cha Sh.236,459,698,078 na Dola za Kimarekani 50,565,602 kama yalivyoainishwa hapa chini hayakuwa yameshughulikiwa kikamilifu.

Idara	Kiasi(Sh.)	Kiasi (Dola za Kimarekani)
(i) Maduhuli		
Ushuru wa Forodha	25,962,179,237	699,541
Idara ya Kodi za ndani	17,834,418,929	-
Idara ya walipa kodi wakubwa	192,367,017,620	49,866,061
Jumla	**236,163,615,786**	**50,565,602**
(ii) Matumizi	296,082,292	-
Jumla	**236,459,698,078**	**50,565,602**

Baadhi ya masuala yaliyoainishwa kwenye jedwali hayakujibiwa kikamilifu tangu mwaka 2001/2002 na baadhi yake yanasubiri maamuzi ya Mahakama.

2.4 Majibu ya hoja zitokanazo na ukaguzi wa Taarifa Jumuifu za Taifa za Taifa.

Namba	Maelezo
1	**Maduhuli yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Sh.13,475,072,714**

www.JamiiForums.com

	Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ulitakiwa kuonyesha tofauti kiasi cha fedha kilichohamishwa ili kuweza kuhakiki na kufuatilia mapendekezo kwa urahisi na kuhakikisha kiasi cha fedha kilichohamishwa kimewekwa katika akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hakuna ripoti iliyowasilishwa na Hazina kuonyesha kwamba kiasi hicho kimewekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina.
2	**Vitega Uchumi vya Serikali** Msajili wa Hazina alitakiwa kurekodi mtaji wa kuanzia mwanzoni mwa mwaka wa fedha kama kitega uchumi cha Serikali na mabadiliko yoyote kufanyika mwishoni mwa mwaka wa fedha.Serikali haijatathmini raslimali zake za nje na pale inapobidi kuzifuta raslimali zisizofanya vizuri kama nilivyopendekeza katika ripoti ya mwaka uliopita.
3	**Mapungufu katika kusimamia mali za Serikali** Ripoti ya Hesabu Jumuifu za Taifa zinaonyesha mali za Serikali kiasi cha Sh.7,981,954,338,324. Ingawa Serikali ilikubaliana na mapendekezo yangu, lakini bado hakuna daftari au kumbukumbu zinazoonyesha uandikishwaji wa mali za Serikali.
4	**Fedha ambayo haikutumika kutorudishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali Sh.31,821,562,811** Hesabu Jumuifu za Taifa zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh.16,186,322,742 kati ya Sh.31,821,562,811 kilichobaki bila kutumika katika miaka ya fedha 2008/2009 and 2009/2010 hakikurejeshwa katika mfuko mkuu wa Serikali na kuingizwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kama nilivyopendekeza.
9.0	**Usimamizi wa madeni yanayotarajiwa kutokana na ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi (PPP)**
9.1	**Udhaifu katika mfumo wa kusimamia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi** Mapitio ya makubaliano yaliyofanywa kati ya Serikali na sekta binafsi kwa baadhi ya wawekezaji binafsi

www.tam...ms.com

	imeonekana kuwa na mafanikio kidogo yenye mapungufu makubwa. Mazungumzo hayo ni kati ya Serikali na SONGAS Ltd, IPTL Ltd, ARTUMAS, TRL Ltd, ATCL Ltd, Kiwira Coal Mines (TANPOWER Ltd), City Water na TICTS. Pamoja na mapendekezo yetu kwa Wizara ya Fedha kuandaa orodha ya kina ya adhari katika mfumo wa bajeti, ikiwa ni pamoja na uwazi na uthabiti wa madeni yanayotarajiwa kutokana na ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kupima gharama za madeni yanayotarajiwa ili kushawishi maamuzi ya kufanya au kutokufanya mradi; Serikali kufanya uchambuzi wa kina wa gharama na manufaa pamoja na thamani ya fedha, baadhi ya rasilmali au vitega uchumi vimeonekana kutokuwa endelevu kiuchumi; Mapendekezo ya ubia kati ya Sekta ya Umma na binafsi yawe yanapitiwa na watu wenye utaalamu katika maswala ya ubia kati ya Sekta ya Umma na binafsi na usimamizi wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha kabla ya kusaini mkataba; Serikali kufuatilia kwa makini miradi inayotekelezwa kwa ubia kati yake na sekta binafsi (miradi iliyopo na inayotarajiwa kuanza baadaye) ili kuchukua hatua za tahadhari na kupunguza uwezekano wa hatari ya kuwa na madeni yasiyotarajiwa na matukio kama hayo; Serikali kuangalia uwezekano wa kupitia mikataba iliyopo ili kuangalia kama kuna mapungufu ambayo yanaweza kurekebishwa na kuhakikisha kwamba Serikali inanufaika na shughuli hizo na kuzuia uwezekano wa athari zinazoweza kutokea kutokana na makubaliano hayo;Serikali kumpatia Mshauri kazi ya kukagua utendaji wa uongozi katika kuendesha makampuni yote; Serikali kupata ushari wa kisheria katika mchakato wa kuzingatia uvunjaji wa mikataba yote na makampuni binafsi ambayo yameshindwa kuzingatia sheria na masharti ya mikataba. Hakuna kilichotekelezwa kama nilipendekaza.

www.iamit-forums.com

9.2	**Usimamizi wa madeni yamkini kutokana na ubia kati ya Serikali na sekta binafsi mali na amana zake** Mara nyingi makubaliano ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP) yameonekana kutokuwa na mpangilio mzuri wa uwendeshaji kwani ni dhahiri kwamba mwisho wa ubia husababisha Serikali kuwa na madeni makubwa ambayo haikuyatarajia. Ingawa nilipendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuzuia kutoa mikopo na kudhamini sekta binafsi au wawekezaji wasio na uwezo kifedha na baadaye mzigo wote hubebwa na Serikali, lakini mapendekezo yangu hayajatekelezwa. Pamoja na hayo, mapendekezo yangu kwa Serikali kurekebisha Sheria ya Mikopo, Udhamini na Misaada ya mwaka 1974 (iliyorekibishwa mwaka 2004) yanayoongelea rehani kwa mikopo na dhamana inayotolewa na mashirika ya umma bado hayajazingatiwa.
9.3	**Kutojihusisha kikamilifu kwa Serikali katika makubaliano ya kutayarisha mikataba na kujenga kama vile Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) na vingine kama hivyo.** Serikali iliingia makubaliano ya mikataba na Mifuko wa hifadhi ya jamii katika kutayarisha mikataba na kujenga Mabibo hosteli ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam; Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na NSSF, PPF, PSPF, LAPF and NHIF na Ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela-Africa na PPF. Ukaguzi umebaini kuwa hakuna vielelezo vinavyoonyesha ushiriki wa Serikali katika kubuni na kujenga miradi hiyo na hivyo basi kunaweza kuisababishia Serikali kubeba gharama kubwa kwa wakandarasi kutumia bei za juu kwa gharama za

www.JamiiForums.com

	ujenzi. Ingawa nilitoa mapendekezo yangu kwa Wizara ya Fedha kumpatia mshauri kazi ya ukaguzi wa dhamani ya fedha katika miradi hiyo mitatu ili kugundua gharama halisi zilizotumika, stahili na uhalali wa madeni kutoka Mifuko ya hifadhi ya jamii; na kuwasilisha mikataba husika inayoonyesha masharti katika ubunifu, ujenzi na makubaliano ya namna ya kufanya malipo kwa ajili ya ukaguzi, hakuna kilichotekelezwa na Wizara.

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

SURA YA 3

MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO

3.1 Utangulizi

Sehemu hii inatoa mchanganuo wa kina wa ugharimiaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka 2009/2010 na 2010/2011. Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa kiasi kikubwa zinapata fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia Hazina.

3.2 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi ya Kawaida katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, jumla ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2009/2010 zilikuwa Sh.6,251,629,581,428 wakati matumizi halisi yalikuwa Sh.6,237,494,869,945. Kwa upande mwingine, fedha zilizotolewa na Hazina kwenda Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa katika mwaka wa fedha 2010/2011 zilikuwa Sh. 7,587,424,923,903 wakati matumizi halisi yalikuwa ni Sh. 7,581,154,383,395 **(Kiambatanisho II)**

Muhtassari wa mchanganuo huu ni kama ifuatavyo:

	2009/2010	**2010/2011**
Fedha zilizotolewa (Sh)	6,251,629,581,428	7,587,424,923,903
Matumizi halisi (Sh)	6,237,494,869,945	7,581,154,383,395
Tofauti (Sh)	**14,134,711,483**	**6,270,540,508**

www.JamiiForums.com

Pia taarifa hiyo hapo juu imeonyeshwa katikaa chati mhimili hapa chini:



3.3 Ulinganisho wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya Wizara na Idara za Serikali kwa kipindi cha 2009/2010 na 2010/2011

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba jumla ya fedha zilizotolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2009/2010 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Sh 6,251,629,581,428 na matumizi ya maendeleo yalikuwa Sh. 2,299,010,652,135 na kufanya jumla ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kuwa sh.8,550,640,233,563. Halikadhalika, mchnganuo unaonyesha kuwa kiasi kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni asilimia 27 na matumizi ya kawaida yalikuwa asilimia 73

Kwa upande mwingine, fedha zilizotolewa kwa ya matumizi ya kwaida kwa mwaka 2010/2011 ni Sh.7,587,424,923,903 na matumizi ya maendeleo zilikuwa Sh.2,223,684,150,465 na kufanya jumla ya

www.JamiiForums.com

fedha zote zilizotolewa kufikia Sh 9,811,109,074,368 . Mchanganuo huu pia unaonyesha kuwa asilimia 77 ya fedha zote zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 23 kwa matumizi ya maendeleo.

Mchanganuo huo umewekwa katika jedwali lifuatalo:-

Fungu	2009/2010	%	2010/2011	%
Fedha za matumizi ya kawaida (Sh)	6,251,629,581,428	73	7,587,424,923,903	77
Fedha za matumizi ya maendeleo (Sh)	2,299,010,652,135	27	2,223,684,150,465	23
Jumla	**8,550,640,233,563**	**100**	**9,811,109,074,368**	**100**

Pia taarifa hiyo hapo juu imeonyeshwa kwenye chati mhimili kama ifuatayo:



www.JamiiForums.com

3.4 Uwiano wa bajeti dhidi ya fedha zilizotolewa na **Hazina** kwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara

Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Wizara na Idara kwa mwaka 2009/2010 ilikuwa Sh. 2,825,431,400,000 ambapo kiasi cha Sh.2,299,010,652,135 kilitolewa na Hazina ikiwa ni pungufu kwa Sh. 526,420,747,865 sawa na asilimia 19.

Aidha, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara na Idara katika mwaka 2010/2011 ilikuwa Sh. 3,750,684,569,000 ambapo fedha zilizotolewa na Hazina zilikuwa Sh. 2,223,684,150,465 ikiwa ni pungufu kwa Sh. 1,527,000,418,535 sawa na asilimia 41 ya fedha zilizoidhinishwa.
Muhtasari wa bajeti na fedha zilizotolewa kwa Wizara na Idara kwa kipindi cha miaka miwili ni kama ifuatavyo:

Mwaka	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Fedha halisi zilizotolewa (Sh.)	Tofauti (Sh.)	%
2009/2010	2,825,431,400,000	2,299,010,652,135	526,420,747,865	19
2010/2011	3,750,684,569,000	2,223,684,150,465	1,527,000,418,535	41

Kutokana na jedwali hapo juu, shuguli za maendeleo za jumla ya Sh.1,527,000,418,535 au asilimia 41 ya fedha zilizoidhinishwa hazikutekelezwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 ikilinganishwa na Sh.526,420,747,865 au asilimia 19 ambazo hazikutolewa katika mwaka 2009/2010. Hii inamaanisha kwamba, shughuli za maendeleo za kiasi hicho cha fedha hazikutekelezwa kwa miaka husika.

Taarifa kwenye jedwali hilo hapo juu pia imeonyeshwa kwenye chati mhimili kama ifuatavyo:

www.jamiiforums.com



Kutokana na uchambuzi na chati mhimili hapo juu, ni dhahiri kuwa kuna tatizo kubwa katika utoaji wa fedha za shughuli za maendeleo ambapo fedha zinazotolewa na Hazina kugharamia miradi ya maendeleo zimeendelea kupungua ikilinganishwa na bajeti iliyopitishwa na bunge. Mwelekeo unaonyesha kuwa kwa kipindi cha miaka miwili mapungufu ya ugharimiaji wa shughuli za maendeleo yanazidi kuongezeka kutoka asilimia 19 kwa mwaka 2009/2010 hadi asilimia 41 mwaka 2010/2011.

3.5 Mamlaka ya Mapato Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia ukusanyaji wa kodi za Serikali kuu pamoja na ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Serikali. Tangu kuanzishwa kwake, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikitayarisha hesabu zilizokuwa zikionesha Mapato na Matumizi. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kutayarisha aina mbili za Taarifa za Hesabu ambazo ni zile za Mapato na Taarifa ya Hesabu za Matumizi.

www.JamiiForums.com

3.5.1 Masuala ya miaka iliyopita yasiyojibiwa

Hadi kufikia wakati wa kutoa taarifa yangu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (Disemba 31, 2011), Mamlaka ilikuwa na masuala mbalimbali ya ukaguzi yaliyoripotiwa katika taarifa zilizopita yaliyofikia kiasi cha sh 236,459,698,078 na Dola za Kimarekani 50,565,602 ambayo yalikuwa hayajashughulikiwa kikamilifu kama yalivyoainishwa hapa chini.

Idara	Kiasi (Sh.)	Kiasi (Dola za Kimarekani)
(i) Maduhuli		
Ushuru wa Forodha	25,962,179,237	699,541
Idara ya Kodi za ndani	17,834,418,929	-
Idara ya walipa kodi wakubwa	192,367,017,620	49,866,061
Jumla ndogo	**236,163,615,786**	**50,565,602**
(ii) Matumizi	296,082,292	-
Jumla kuu	**236,459,698,078**	**50,565,602**

Baadhi ya masuala yaliyoainishwa hapo juu yamekuwepo tangu mwaka 2001/2002 na baadhi yake yanasubiri maamuzi ya Mahakama.

Ukusanyaji wa Mapato

Hesabu za Mapato zinaonyesha kuwa kiasi cha Sh 5,550,205,244,378 kilikusanywa kwa Tanzania Bara ikilinganishwa na makisio ya Sh.5,849,093,700,000 ikiwa ni makusanyo pungufu kwa Sh.298,888,455,622 sawa na asilimia 5.11% ya Makisio ya Mapato ya Mwaka.

Kwa upande wa Zanzibar, makusanyo yalikuwa Sh. 76,357,574,602 ikilinganishwa na Makisio ya Sh.69,240,800,000; na kufanya makusanyo ya ziada ya kiasi cha Sh.7,116,774,602 sawa na asilimia 10.27 ya makisio ya Mapato ya mwaka.

www.JamiiForums.com

Mchanganuo wa makusanyo ya mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa idara ni kama ifuatavyo:-

Tanzania Bara

Idara (a)	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b) Sh.	Ziada/pungufu ya makusanyo (c) = (b-a) Sh.	& (c/a)
Idara ya Kodi za Ndani	1,047,547,100,000	1,004,147,527,178	43,399,572,822	4.14
Idara ya Walipa kodi Wakubwa	2,336,419,100,000	2,111,110,359,085	225,308,740,915	9.64
Ushuru wa Forodha	2,421,450,700,000	2,405,263,556,329	16,187,143,671	0.67
Jumla ndogo	**5,805,416,900,000**	**5,520,521,442,592**	**284,895,457,408**	**4.91**
Ongeza: Vocha za Hazina	43,676,800,000	29,683,801,786	13,992,998,214	32.04
Jumla Kuu	**5,849,093,700,000**	**5,550,205,244,378**	**298,888,455,622**	**5.11**

Zanzibar

Idara	**Lengo (a) Sh.**	**Makuanyo halisi (c) Sh.**	**Ziada/Pungufu ya Makusanyo (c) = (b-a) Sh.**	**% (c/a)**
Idara ya Kodi za ndani	29,733,000,000	27,672,570,440	-2,060,429,560	(6.93)
Ushuru wa Forodha	39,507,800,000	48,685,004,162	9,177,204,162	23.23
Jumla	**69,240,800,000**	**76,357,574,602**	**7,116,774,602**	**10.28**

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa pande mbili za Serikali – yaani Tanzania Bara na Zanzibar kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:-

www.JamiiForums.com

Tanzania Bara

Mwaka	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b)Sh.	Tofauti (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
2008/2009	4,600,849,900,000	4,174,371,105,259	(426,478,794,741)	(9.27)
2009/2010	5,028,922,100,000	4,637,686,999,618	(391,235,100,382)	(7.78)
2010/2011	5,849,093,700,000	5,550,205,244,378	(298,888,455,622)	(5.11)

Mwelekeo huo wa makusanyo unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:



www.jamii.ms.com

Zanzibar

Mwaka	Lengo (a) Sh.	Makusanyo Halisi (b) Sh.	Tofauti (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
2008/2009	49,220,900,000	53,877,284,997	4,656,384,997	9.46
2009/2010	63,234,200,000	59,998,034,392	(3,236,165,608)	(5.12)
2010/2011	69,240,800,000	76,357,574,602	7,116,774,602	10.28

Mwelekeo huo wa makusanyo kwa upande wa Zanzibar unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:



Matokeo ya makusanyo ya Mapato kwa miaka mitatu iliyopita kwa upande wa Tanzania Bara yanaonyesha ongezeko la makisio na makusanyo mwaka hadi mwaka. Hata hivyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 makusanyo ya mapato yamekuwa chini ya makisio kwa asilimia 5. Mchanganuo zaidi wa mwenendo wa makisio kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2008/10 hadi

www.jamii.com

2009/11 unaonyesha ongezeko chanya kutoka ongezeko la asilimia 9 hadi asilimia 19. Kwa upande mwingine, kiwango cha ongezeko la makusanyo halisi kilikua kutoka asilimia 11 kipindi cha 2008/10 hadi asilimia 20 kwa kipindi cha 2009/11.

Kwa upande mwingine, makusanyo ya mapato Zanzibar yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, katika mwaka 2010/201011 kulikuwa na ongezeko kidogo la makadirio ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita na kufanya makusanyo kuwa juu ya makisio kwa asilimia 10.

Zaidi ya yote, ukaguzi umebaini kuwa maduhuli yote yaliyokusanywa Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 hayakuhamishiwa kwenye akaunti ya Kamishina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato iliyoko Benki Kuu japo ni jukumu la Mamlaka kufanya hivyo.

3.5.2 Misamaha ya Kodi Sh.1,016,320,300,000

Taarifa za Mapato kwa mwaka unaoishia tarehe 30, Juni 2011 zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh.1,016,320,300,000 kilikuwa ni misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Taasisi mbali mbali na watu binafsi kama inavyoonekana hapa chini:

Taasisi	Idara ya Forodha (Sh)	Idara ya Kodi za ndani (Sh)	Jumla (Sh) 2010/2011	Jumla (Sh) 2009/2010
Taasisi za Serikali	52,743,800,000	-	35,867,200,000	52,743,800,000
Mashirika ya Umma	8,758,700,000	-	8,131,200,000	8,758,700,000
Taasisi za Kidini	281,200,000	-	1,569,300,000	281,200,000
Taasisi zisizo za Kiserikali	22,147,100,000	-	25,462,600,000	22,147,100,000
Miradi ya Wafadhili	72,458,100,000	-	115,758,100,000	72,458,100,000
Makampuni na watu binafsi	36,174,600,000	-	182,706,100,000	36,174,600,000

www.JamiiForums.com

Sekta ya Madini	48,738,600,000	-	109,885,900,000	48,738,600,000
Kituo cha Uwekezaji Tanzania	268,002,300,000	-	239,667,300,000	268,002,300,000
Misamaha ya kodi za Ongezeko la Thamani	-	168,671,900,000	279,845,200,000	168,671,900,000
Misamaha ya Kodi katika Maduka yasitozwa kodi	-	- 2,691,600,000	17,427,400,000	2,691,600,000
Jumla	**509,304,400,000**	**171,363,500,000**	**1,016,320,300,000**	**680,667,900,000**

Mwenendo wa misamaha unaonyesha ongezeko la sh 335,652,400,000 sawa na asilimia 49 kutoka Sh.680,667,900,000 zilizosamehewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 hadi Sh.1,016,320,300,000 mwaka 2010/2011.

Endapo kiasi hiki cha Sh.1,016,320,300,000 ambacho ni sawa na asilimia 18 ya makusanyo yote kingekusanywa, ni dhahiri kuwa kiasi cha Sh.298,888,455,622 kilichokusanywa pungufu kwa Tanzania Bara kisingekuwepo na badala yake kungekuwepo ziada ya Sh.717,431,844,378.

Kwa ujumla, misamaha ya kodi kwa Tanzania Bara imeongezeka kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June 2011 ikilinganishwa na mwaka uliopita na kuathiri ufanisi katika makusanyo kama ifuatavyo:

Maelezo	**2011/2010 (Sh)**	**2009/2010 (Sh)**
Makusanyo Halisi	5,550,205,244,378	4,637,686,999,618
Misamaha	1,016,320,300,000	680,667,900,000
Asilimia ya Misamaha kwa makusanyo Halisi	18%	15%
Pungufu la Makusanyo	298,888,455,622	391,235,100,382
Ziada kama misamaha isingetolewa	717,431,844,378	289,432,799,618

www.JamiiForums.com

3.5.3 Usitishwaji wa Mita zinazotumika Kupima Ujazo wa Mafuta Bandarini

Kabla ya mwaka 2005 njia iliyokuwa inatumika kupata ujazo wa mafuta yanayoingizwa nchini moja tu ya kuzamisha fimbo (stick dipping) kwenye meli na matangi kabla na baada ya kupakua mafuta. Hata hivyo, miaka ilivyoenda, njia hii ilionyesha mapungufu mengi ambayo yamekuwa yakitumiwa na wafanya biashara wa mafuta kukwepa kodi na kuikosesha serikali mapato.

Ili kurekebisha mapungufu haya mwaka 2005, serikali, kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania iliamua kununua mita ambazo ziliidhinishwa na Wakala wa Vipimo (Weights and Measures Agency) kwa barua yenye kumb. Na HB.111/597/01/111 ya tarehe 27 Desemba, 2004 kwa ajili ya kuhakiki mafuta yanapopakuliwa melini kabla hayajaingia kwenye matangi ya wafanya biashara.

Hata hivyo, mwezi February, 2011 wakala wa vipimo ambao awali waliidhinisha mita hizo waliwaandikia Mamlaka ya Bandari barua yenye kum. Na BA/84/221/01/26 ya tarehe 02/02/2011ikiwataka kuacha mara moja utumiaji wa mita hizo kwa madai yafuatayo:

(i) Ilidaiwa kuwa Mita hizo zilikuwa zikitoa vipimo visivyo sahihi ikilinganishwa na ujazo halisi unaopatikana kwa njia ya kutumia fimbo kabla na baada ya kupakua mafuta.

(ii) Pia ilidaiwa kuwa mita hizo zilitengenezwa mahsusi kwa ajili ya kupima mafuta wakati wa kupakia melini, hivyo basi, kuzitumia wakati wakupakua kunasababisha matatizo mengi yanayotokana na ufanisi mdogo wa mita hizo na kuongeza msongamano wa meli bandarini.

www.JamiiForums.com

Hii inaashiria kwamba mita hizo zilinunuliwa bila ya uchambuzi yakinifu ili kujua aina na ubora wa mita zinazohitajika. Zaidi ya hayo, kutotumia mita hizo zilizonunuliwa kwa gharama kubwa inamaanisha kuwa madhumuni ya kununua mita hizo hayakufikiwa licha ya kuingia kwenye matumizi makubwa yasiyokuwa na faida.

Serikali kwa upande wake haijaonyesha jitihada katika suala hili ili kupata njia ambayo ni sahihi na ya kuaminika kupata ujazo halisi wa mafuta yanayoingizwa nchini au hata kuhoji maamuzi ya Wakala wa Vipimo.

Kwa mtazamo wetu, njia ya kupima ujazo wa mafuta kwa kutumia mita za kisasa ni sahihi zaidi kuliko kutumia fimbo ambayo imepitwa na wakati na ni rahisi kuhujumiwa na wafanya biashara. Utafiti zaidi unahitajika ili kupata njia sahihi na ya kuaminika kupima ujazo wa mafuta ili kupata kodi sahihi itokanayo na mafuta yanayoingizwa nchini.

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

SURA YA 4

MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI

4.0 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu unafanywa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 5 (a) cha Sheria hiyo hiyo ya Ukaguzi kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, matumizi yake yawe yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 136 ya Katiba, na iwapo ataridhika kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe. Kutokana na ukweli kuwa malipo ya pensheni hulipwa bila makadirio yake kuidhinishwa na Bunge, ni vyema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu akafanya ukaguzi wa awali kwa malipo hayo ya mafao ya wastaafu ambayo si rahisi kukadiriwa kwa uhakika na kutengewa fedha.

4.1 Madhumuni ya ukaguzi wa awali

Lengo la kufanya ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu ni kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuweza kuhakiki usahihi wa malipo hayo na kuzuia au kubaini makosa mapema kwa nia ya kulinda fedha za Serikali na wakati huo huo, kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa kile wanachostahili. Ukaguzi wa awali ni muhimu kwa kuwa malipo yasiyo sahihi yakifanywa kwa wastaafu inakuwa vigumu kwa Serikali kuyarejesha kutoka kwa wastaafu hao.

Kwa upande mwingine, ukaguzi wa awali unalenga kuhakikisha kuwa sheria za malipo ya uzeeni pamoja na

www.JamiiForums.com

kanuni na sera za utmishi wa umma, miuondo ya utumishi na mifumo ya mishahara vinafuatwa na kuzingatiwa wakati wa kutendgeneza malipo ya wastaafu.

4.2 Mawanda ya ukaguzi wa awali

Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyomo katika ripoti hii hayawahusu watumishi ambao mafao yao ya uzeeni yanashughulikiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (PSPF). Ukaguzi wa awali wa mafao ya uzeeni unahusisha makundi yafuatayo:

- Maafisa wa Jeshi, Walimu na Maafisa Usalama.
- Malipo ya Mikataba kwa Viongozi wa Kisiasa, wasiokuwa raia na wastaafu walioko kwenye ajira ya mkataba.
- Watumishi wa Serikali wasio na stahili ya pensheni ambao hulipwa fidia ya kiinua mgogo
- Mafao ya askari Polisi wa ngazi za chini

4.3 Changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi

Wakati wa ukaguzi zilijitokeza changamoto ambazo zinaweza kuainishwa katika makundi matatu yafuatayo:

(i) Matatizo ya utendaji,

(ii) Tafsiri zisizo sahihi za Sheria za Penseni na Kanuni zake,

(iii) Kasoro za kiutawala

4.4 Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo

4.4.1 Matokeo

Katika mwaka 2010/2011 Ofisi yangu ilianza na majalada 32 ya pensheni ikiwa ni bakaa kutoka mwaka 2009/2010. Jumla ya majalada 4,788 ya wastaafu yaliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kufanya idadi ya majalada yote katika kipindi husika kuwa 4,960. Kati ya majalada yote yaliyokuwepo, majalada 4,412 yalikaguliwa, 361 yalirudishwa kwa Maafisa Masuuli kwa marekebisho na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 majalada 47 yalikuwa

www.JamiiForums.com

yakiendelea kukaguliwa kama inavyoonyeshwa kwa ufupi hapa chini:

Mchanganuo	**Majalada**
Salio la nyuma 1 Julai, 2010	32
Majalada yaliyopokelewa katika mwaka	4,788
Majalada yaliyokuwepo kwa ajili ya ukaguzi	4,820
Majalada yaliyokaguliwa	4,412
Salio la majalada tarehe 30 Juni, 2011	361

4.4.2 Ukokotoaji zaidi au pungufu wa mafao ya wastaafu

Majalada yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi yameonyesha kuwepo kwa makosa katika ukokotoaji wa mafao ya baadhi ya wastaafu. Makosa hayo yangesababisha mafao kulipwa zaidi au pungufu ya stahili ya mstaafu. Kwa mfano, kati ya majalada 4,788 ya pensheni yaliyokaguliwa, 282 yangelipwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 539,201,733.63 wakati majalada 79 yangelipwa pungufu kwa kiasi cha Sh.106,007,774.81 kama yalivyoonyeshwa hapa chini:-

(i) Fedha zilizozidishwa Sh.539,201,733.63

Na.	**Maelezo**	**Idadi ya kadhia**	**Kiasi (Sh.)**
1.	Muda uliozidishwa	154	427,425,562.50
2.	Makosa katika ukokotoaji	90	48,236,335.20
3.	Mishahara iliyozidishwa	38	63,539,835.93
	Jumla	**282**	**539,201,733.63**

www.JamiiForums.com

(ii) Kiasi kilichopunjwa Sh.106,007,774.81

Na.	Maelezo	Idadi ya watumishi	Kiasi (Sh.)
1.	Kipindi kilicho punjwa	33	68,287,785.44
2.	Makosa katika ukokotoaji	27	20,434,310.49
3.	Mishahara iliyopunjwa	19	17,285,678.88
	Jumla Sh.	**79**	**106,007,774.81**

Kutokana na mchanganuo huo hapo juu, endapo malipo ya uzeeni yasingekaguliwa kabla ya kulipwa, Serikali ingepata hasara ya Sh. 539,201,733.63 wakati wastaafu wangepata malipo pungufu ya jumla ya Sh.106,007,774.81.

4.4.3 Utumiaji wa mishahara isiyosahihi wakati wa kuandaa mafao ya mwisho

Sheria ya Pensheni inaelekeza kutumia mshahara wa mwisho wa mtumishi akiwa kwenye ajira ya Umma katika kuandaa mafao ya mstaafu. Hata hivyo, imeonekana kuwa baadhi ya watumishi waliokuwa Serikalini waliteuliwa katika nafasi mbalimbali katika Mashirika ya Umma au uongozi wa kisiasa na hivyo kupokea mishahara iliyoko katika vyeo hivyo. Sio sahihi kisheria mishahara hiyo ya uteuzi katika mashirika na siasa kutumika kukokotoa mafao ya pensheni kwa wastaafu badala ya ile ya mwisho katika utumishi wa Umma.

Baadhi ya wastaafu wamekuwa wakishinikiza waajiri wao kukokotoa mafao yao kwa kutumia mishahara ya mwisho kwenye taasisi walizokuwa wakifanya kazi kabla ya kustaafu. Hii ni kinyume na sheria ya pensheni ambayo inataka ukokotoaji na ulipaji wa pensheni uzingatie mishahara inayokubalika kulingana na sheria husika.

4.4.4 Madai mara mbili ya mafao ya kustaafu (pensheni na ajira ya mikataba)

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa maafisa wa jeshi waliokuwa wameteuliwa katika nyadhifa za uongozi wa kisiasa waliendelea kuwa na nyadhifa zao za kijeshi kinyume na maagizo yaliyotolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Katibu Mkuu Kiongozi yaliyowataka kujiuzulu

www.JamiiForums.com

vyeo vyao vya kijeshi mara tu baada ya uteuzi katika nyadhifa za kisiasa. Suala muhimu hapa ni kuhakikisha kuwa muda wa utumishi katika jeshi unalipwa pensheni na muda ambao mstaafu ametumikia uongozi wa kisiasa unalipwa tuzo ya mkataba. Hata hivyo, uzoefu umeonyesha kuwa utaratibu huo haufuatwi na hivyo kusababisha malipo mara mbili kwa maafisa wahusika; kwa mfano:

(i) Maafisa wa jeshi wanaopata ajira za kisiasa hawaachi utumishi wao jeshini hadi wanapofikia umri wa kustaafu katika jeshi na hivyo kusababisha ukokotoaji wa mafao yao ya kustaafu kujumuisha muda ambao wametumikia vyeo katika siasa kinyume na sheria za pensheni

(ii) Imeonekana pia kuwa baadhi ya maafisa wastaafu wamerejeshwa tena kazini na hivyo kulazimika kurudisha barua zao za kustaafu. Hali hii inampa mstaafu husika haki ya kunufaika na sheria za pensheni zilizopo na hivyo kufanya pawepo na ongezeko la mafao ya uzeeni na malipo ya malimbikizo ya mishahara. Hii ni kinyume na sheria za pensheni ambazo zinataka mstaafu alipwe kulingana na masharti ya ajira yake na sheria za pensheni zilizopo kwa wakati huo.

4.4.5 Baadhi ya Watumishi walioajiriwa kwa Mikataba Wanachangia na Kulipwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)

Baadhi ya watumishi walioajiriwa kwa masharti ya mikataba wamebainika kusajiliwa na kuchangia kwenye Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF). Kulingana na sheria na kanuni za pensheni, wtumishi wanaofanywa kazi kwa mikataba hawastahili kuchangia wala kulipwa mafao yao kupitia mfuko huu.

4.4.6 Kuchelewa kuwasilisha majalada kwa ajili ya ukaguzi

Sheria ya Pensheni inataka mchakato wa kulipa mafao ya wastaafu kuanza miezi 6 kabla ya mtumishi kustaafu. Utaratibu huu unalenga kukamilisha maandalizi ya malipo mapema na kulipwa kwa wakati. Kinyume na hivyo, baadhi ya majalada yanaletwa ukaguzi baada ya miezi kadhaa au mwaka baada mtumishi kustaafu.

www.JamiiForums.com

Zaidi ya hayo, majalada mengi ya wastaafu huletwa kwa ajili ya ukaguzi wa awali yakiwa na nyaraka pungufu na hivyo kulazimu kuitisha nyaraka hizo jambo ambalo huchangia kucheleweshe machakato mzima wa ulipaji wa mafao kwa wastaafu.

4.4.7 Mkanganyiko kuhusu sheria ipi itumike kulipa mafao

Imeonekana kuwa uongozi wa baadhi ya taasisi umekuwa ukiomba idhini ya kulipa mafao ya uzeeni bila kuzingatia sheria za pensheni ilivyoainishwa hapo chini:

(i) Utumiaji mishahara banafsi (Salary Personal to Oneself) kukokotoa malipo ya pensheni

Katika nyakati tofauti idhini imekuwa ikitolewa na mamlaka husika kuruhusu kuandaa malipo ya wastaafu kwa kutumia mishahara binafsi (Salary personal) kwa watumishi walioajiriwa kwa mikataba wakitokea Mashirika ya kimataifa na ya Umma kulingana na Aya ya 47(a), (b) na (c) ya Kanuni za Kudumu na Kifungu cha 14 cha Sheria ya Pensheni kama ilivyorekebishwa tarehe 20 Machi, 1978. Hata hivyo Sheria na Kanuni zilizotajwa zinatumika kwa watumishi wa masharti ya kudumu na pensheni wanapohamishwa toka mashirika ya umma kwenda serikalini au kinyume chake.

(ii) Madai ya Wastaafu Waliopitia Ajira za Aina Tofauti

Pia, imeonekana kuwa baadhi ya maafisa walioacha kuwa viongozi wa kisiasa kwa namna ambayo sheria za pensheni zilizopo ziliruhusu wao kulipwa mafao lakini malipo yao hayakutayarishwa kwa wakati kwa madai kuwa maafisa wahusika hawakuomba kulipwa mafao hayo.

Aidha, waajiri wao hawakushughulikia stahili zao za mafao kwa vile maafisa hawa waliendelea kuteuliwa katika nafasi ambazo mafao yake ya pensheni yanatawaliwa na sheria nyingine. Wakati maafisa hawa wanapostaafu katika ajira yao ya mwisho, huomba kibali cha kuunganisha muda wote wa ajira ili walipwe pensheni kwa sheria inayowapa manufaa zaidi kimapato. Hili linaathiri zaid wastaafu kwa, sheria haitoi mwanya kwa mstaafu kunufaika kwa kutumia sheria inayosimamia ajira yake ya mwisho katika mashirika ya kimataifa au taasisi nyingine.

www.JamiiForums.com

4.4.8 Kutokuwa na stahili ya kulipwa pensheni

Watumishi wa ngazi ya chini Serikalini waliokuwa wameajiriwa chini ya masharti ya muda na baadae wakaingizwa katika masharti ya kudumu na pensheni, mafao yao ya uzeeni yalikokotolewa kama vile bado walikuwa chini ya masharti ya muda kinyume na sheria za pensheni ambazo zinataka kipindi alichotumikia mstaafu chini ya masharti ya muda kupata kibali cha Katibu Mkuu Hazina ili kihesabiwe katika masharti ya kudumu kwa madhumuni ya kulipa pensheni

4.4.9 kuzidisha muda wa ajira ya pensheni kwa watumishi wa jeshi

Ukaguzi wa awali wa nyaraka za maombi ya pensheni umebaini kuwa baadhi ya maafisa wa jeshi wamekuwa wakiendelea na ajira hadi miaka mitano (5) zaidi ya umri wao wa kustaafu kwa mujibu wa sheria baada ya kupata idhini ya waajiri wao. Kuzidisha muda wa kufanya kazi ni kinyume na sheria ya Jeshi La Wananchi wa Tanzania inayotaka ajira ya masharti ya pensheni kukoma baada ya umri wa kustaafu kwa mujibu wa sheria isipokuwa kwa mazingira maalum. Imebainika kuwa kuna nyakati maafisa hawa hupandishwa na kupata nyazifa za juu wakati wameshapitisha umri wa kufanya kazi.

Ukiukwaji huu wa sheria unapelekea ulipaji wa mishahara na pensheni kwa watumishi wa jeshi visivyo halali.

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

SURA YA 5

MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA WIZARA, IDARA, WAKALA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA

5.1 Fedha JPY 16,699,499,858 zilizotolewa kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo hazijarudishwa Serikalini

Mikakati mbalimbali iliyofanywa na Serikali kukusanya kiasi cha JPY 16,699,499,858 kikilichotolewa kwa wafanyabiashara kwa ajili ya kuagiza bidhaa nje ya nchi na ambacho kimebakia bila kulipwa kwa muda mrefu haikufanikiwa. Licha ya kazi ya kukusanya madeni hayo kupewa Kampuni ya Msolopa Investment tangu tarehe 17 Novemba, 2008, kiasi kinachokusanywa kila mwaka kimezidi kupungua. Hali hii imetokana na kuwepo ushirikiano mdogo kati ya vyombo vinavyosimamia sheria na wafanyabiashara walionufaika na mikopo hiyo kuwa mafichoni.
Ufuatao ni muhtaasari usioridhisha wa jitihada za kukomboa kiasi hicho cha fedha za Serikali kutoka kwa wadaiwa hao sugu kwa nyakati mbalimbali:

Kipindi	**Kiasi kichokombolewa (Sh.)**
Hadi mwezi Aprili 2010	4,512,304,045.60
mwezi Mei hadi 2010	309,783,936.30
Mwezi Disemba hadi 2010 hadi Disemba 2011	2,137,507,236.36

- Kipindi cha kwanza cha mkataba wa ukusanyaji kilifikia ukomo tarehe 25/01/2012

- Chanagamoto zinazolikumba zoezi la ukusanyaji ni kubwa. Ukichukuliwa mfano mmoja tu wa

www.JamiiForums.com

wanufaika 38 waliokopeshwa kiasi cha JPY 390,000,000, katika kipindi cha hadi mwezi Disemba, 2011, ni wadaiwa watano (5) tu waliopatikana kutoka mafichoni na kulipa kiasi cha JPY 124,374,775. Kati ya hao waliolipa, ni mdaiwa mmoja tu aliyemaliza deni lake na wadaiwa 33 kati ya 38 hawajulikani walipo.

Kutokana na hali iliyoelezwa hapo juu, Serikali inapaswa kuchukua hatua za dhati ili kukomboa kiasi hiki kikubwa cha fedha kilichotolewa kwa wafanyabiashara kwa nia njema ya kukwamua mwenendo wa biashara zao. Zipo hatua kadhaa zinazoweza kuchukuliwa kushughulikia tatizo hili. Kwa sasa, ufutwaji wa madeni hayo sio hatua muafaka bali hatua zifuatazo zinapendekezwa:

i) Serikali ifikirie kutumia tovuti au njia nyinginezo za mawasiliano kwa kuweka majina ya wadaiwa hadharani na kuuomba umma kusaidia kufichua waliko
ii) Kuwashitaki wadaiwa hao sugu
iii) Kuzitambua mali zao popote zilipo na kuzitaifisha ili zifidie kiasi wanachodaiwa
iv) Kuweka majina yao hadharani kama wadaiwa wasiofaa kukopeshwa na taasisi yoyote ya fedha
v) Kuwatambua na kuwachukulia hatua maafisa wote ambao wakati wa kushughulikia mikopo hii, hawakuwataka wadaiwa hao kutoa taarifa kamili ya sehemu biashara zao zilipo pamoja na nyaraka muhimu, jambo lililosababisha upatikanaji wao kuwa mgumu wakati wa msako wa kuwatafuta.

5.2 Matengezezo ya magari katika karakana zisizoidhinishwa na TEMESA Sh.77,318,833

Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa zinatakiwa kutengeneza magari yake kupitia TEMESA au kupeleka

www.JamiiForums.com

katika karakana zilizoidhinishwa na TEMESA. Hii ni mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Mali, kazi, huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali ya umma kwa zabuni) ya mwaka 2005.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, imebainika kuwa Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa zipatazo 5 zililipa jumla ya Sh. 77,318,833 katika karakana binafsi za magari ambazo hazijaidhinishwa na TEMESA kama gharama za matengenezo ya magari. Hakuna kibali kilichoombwa kutoka TEMESA kabla ya kupeleka magari katika karakana hizo.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1.	55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	16,110,643
2.	59	Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	13,554,201
3.	77	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	6,927,000
4.	83	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	6,569,797
5.	79	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	34,157,192
		Jumla	**77,318,833**

5.3 Malipo ya mishahara kwa wastaafu wasiokuwa kazini na maafisa wasio na stahili Sh. 142,715,827.99

Ukaguzi wa orodha za malipo ya mishahara mwaka huu umeonyesha kuwa Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa zilizoorodheshwa hapa chini zililipa jumla ya Shs. 142,715,827.99 kama mishahara kwa wastaafu, wasiokuwa kazini na wasiokuwa na stahili.

www.JamiiForums.com

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	18	Mahakama Kuu ya Tanzania	18,018,540.00
2	19	Mahakama za Wilaya na Mwanzo	56,705,420.00
3	42	Ofisi ya Bunge	11,078,420.00
4	44	Wizara ya Viwanda na Biashara	27,099,393.30
5	48	Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Mkakazi	8,596,167.26
6	58	Wizara ya Nishati na Madini	8,177,716.16
7	96	Wizara ya Habari	13,040,171.27
Jumla			**142,715,827.99**

Ufuatao ni muhtasari wa malipo ya mishahara kwa wastaafu, walioacha kazi na wasiokuwa na stahili kwa mwaka 2009/2010 na 2010/2011 kwa ajili ya ulinganisho:

Mwaka	Kiasi(Sh.)	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa
2009/2010	1,842,607,565.29	8
2010/2011	142,715,827.99	7

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mapokezi ya kiasi cha Sh. 465,655,201 kama ilivyoonyeshwa katika hati ya kupokelea fedha, ikiwa ni malipo zaidi ya mishahara. Kiasi hiki kililipwa katika akaunti ya Amana ya Mkuu wa Majeshi (Fungu 38 – Ngome). Hata hivyo, hakuna uthibitisho wowote uliowasilishwa ukaguzi unaoonyesha kama kiasi hicho kilichowekwa katika akaunti ya Amana kilihamishiwa Hazina ilipofika tarehe 30 Juni, 2011. Kutohamishiwa fedha hizo Hazina ni kinyume na Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004).

Jedwali hilo hapo juu linaonyesha kuwa bado kuna matatizo makubwa katika mfumo ya udhibiti wa ndani katika eneo hili la usimamizi wa mishahara.

www.JamiiForums.com

5.4 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 8,076,574,791.42

Malipo ya jumla ya Sh. 8,076,574,791.42 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (zilizorekebishwa 2004). Kwa hali hiyo, uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/ Wakala/ Sekretarieti za Mikoa	Matumizi ya Fungu kwa mwaka (Sh.)	% ya matumizi ya fungu	Nyaraka pungufu (Shs)
1	18	Mhakama Kuu ya Tanzania	14,319,428,524.00	0.19	27,359,720
2	19	Mahakama za Wilaya na Mwanzo	16,746,115,793.00	0.05	8,903,500
3	42	Ofisi ya Bunge	67,865,995,668.00	0.25	170,858,030
4	58	Wizara ya Nishati na Madini	226,973,672,295.54	0.02	35,000,000
5	58	Wizara ya Nishati na Madini	226,973,672,295.54	0.06	141,937,228
6	60	Mahakama ya Kazi	2,376,522,717.00	1.85	44,019,728.00
7	39	Jeshi la Kujenga Taifa	100,359,353,340.00	0.01	9,920,000
8	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS)	13,773,266,215.00	0.04	6,172,790
9	93	Idara ya Uhamiaji	45,087,636,012.50	0.14	64,360,099
10	78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	159,455,748,944.00	0.00	4,545,366
11	61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	64,611,466,648.00	0.66	427,906,854
12	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	468,598,860,119.00	0.02	77,332,806
13	32	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi nwa Umma	38,011,398,802.70	3.55	1,350,611,387.20
14	24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika (CDC)	5,761,422,704.00	0.75	43,035,000
15	43	Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika	273,649,747,143.00	0.04	97,080,000
16	88	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar Es Salaam	151,608,671,550.00	0.02	24,910,500
17	94	Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma	8,157,525,607.00	0.07	5,940,000

www.JamiiForums.com

18	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	105,499,070,798.00	0.01	14,573,608
19	29	Idara ya Magereza	109,889,084,181.00	0.01	8,887,000.22
20	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	585,289,097,821.00	0.90	5,254,436,695
21	84	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida	72,321,179,681.00	0.04	29,120,000
22	95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	5,862,230,917.00	1.43	84,073,500
23	72	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	115,492,915,646.00	0.09	104,711,330
24	79	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	138,089,937,640.39	0.03	40,879,650
Jumla					**8,076,574,791.42**

5.5 Mali na vifaa visivyopokelewa Sh.31,027,797,820

Mali na vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh. 31,027,797,820 vililipiwa lakini havikupokelewa au vilipokelewa pungufu kwenye Wizara/Idara na Wakala kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini. Hali hii ni kinyume na Kanuni ya 122 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Mali, kazi, huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali ya umma kwa zabuni) ya mwaka 2005.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	49	Wizara ya Maji	132,598,919.00
2	57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	30,865,918,901.00
3	99	Wizara ya mifugo na Maendeleo ya Uvuvi	9,000,000
4	84	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida	19, 000,000
5	95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	1,280,000
Jumla			**31,027,797,820**

www.JamiiForums.com

5.6 Malipo yaliyofanyika kutoka katika vifungu visivyohusika Sh.340,756,700.80

Katika mwaka 2009/2010, ukaguzi wa majaribio ulibaini kuwa baadhi ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikuzingatia bajeti ya Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha za Umma (MTEF) na hivyo kufanya malipo ya kiasi cha Shs. 340,756,700.80 kutoka katika vifungu vingine ambavyo havikukasimiwa matumizi hayo bila kibali cha Hazina kinyume na Kanuni ya 51(1-8) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (zilizorekebishwa 2004).

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1.	38	Jeshi la Ulinzi (Ngome)	152,267,812
2.	38	Jeshi la Ulinzi (Ngome)	467,480,778
3.	42	Ofisi ya Bunge	94,000,000
4.	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	38,655,268
5.	59	Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	101,516,410
6.	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS)	5,949,460
7.	33	Tume ya Maadili	45, 026,737.00
8.	12	Tume ya Ajira ya Mahakama	6,473,770
9.	91	Tume ya Kudhibiti Madawa	5,546,276.80
10.	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	73,956,552
11.	27	Msajili wa Vyama vya siasa	134,356,708
12.	69	Wizara ya Maliasili nna Utalii	37,124,900
13.	29	Idara ya Magereza	57,147,108
14.	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	26,151,386
Jumla			**340,756,700.80**

5.7 Malipo yenye shaka Sh.1,471,933,333

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa mitatu zilifanya malipo yenye shaka yanayofikia Sh. 1,471,933,333 Malipo hayo

www.JamiiForums.com

yalionekana kukosa viambatanisho ambavyo vingeonyesha taarifa za kina pasipo kuacha mashaka yoyote kuhusiana na usahihi wa malipo hayo.

Mchanganuo wa malipo yenye shaka ni huu ufuatao:

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/ Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1.	Ofisi ya Waziri Mkuu	37	1,326,002,959
2.	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	85	40,643,265
3.	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	95	105,287,109.00
Jumla			**1,471,933,333**

Muhtasari wa malipo yenye shaka kwa mwaka 2009/2010 na 2010/2011 upo kwenye jedwali lifuatalo kwa ajili ya ulinganisho:-

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa
2009/2010	15,711,104,612	3
2010/2011	1,471,933,333	3

5.8 Kuongezeka kwa malipo ya posho

Serikali inaweza kuboresha zaidi mishahara inayolipwa kwa watumishi endapo utaratibu wa sasa wa kulipa posho utadhibitiwa na fedha hizo kutumika katika kuongeza viwango vya mishahara. Ongezeko la posho mbalimbali lilesababisha kupanda kwa kasma ya mishahara kutoka asilimia 41 (2009/10) hadi 57% (2010/11) bila hatua zozote kuchukuliwa na Serikalimkudhibiti mwelekeo huu. Mwelekeo wa ongezeko la malipo ya posho kwa miaka 2009/2010 na 2010/2011 imeonyeshwa katika jedwali hapa chini kwa ajili ya ulinganisho.

www.JamiForums.com

Sura ya Kasma ya Mishahara	2010/11 (Sh.)	%	2009/10(Sh.)	%
Mishahara -Ajira za Pensheni	569,330,942,721		282,053,778,510.00	
Mishahara - Ajira zisizo za Pensheni	30,728,169,877		256,200,212,613.00	
Michango katika Mifuko ya Pensheni	15,449,433,768		191,161,378,266.00	
Mishahara pekee	**615,508,546,366**	**43**	**729,415,369,389**	**59**
Posho za ajira	292,588,263,901		263,561,362,940.00	
Posho za mavazi	274,971,423		16,397,662,012.00	
Posho za Kujikimu	518,833,236,062		220,523,429,636.00	
Posho	**811,696,471,386**	**57**	**500,482,454,588**	**41**
Jumla	**1,427,205,017,752**	100	**1,229,897,823,977**	100

5.9 Hesabu za Vyama vya Siasa zilizokaguliwa kutowasilishwa kwa Msajili

Kifungu cha 14 (1 – 3) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 kinataka kila Chama cha Siasa kilichosajiliwa kutayarisha hesabu za fedha na mali za Chama na kuziwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Aidha, Sheria hiyo hiyo inamtaka Msajili kutangaza katika Gazeti la Serikali, hesabu za kila Chama cha Siasa kuhusu matumizi ya fedha, rasilmali na mali.

Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011, kiasi cha Sh. 17,202,999,991 kililipwa kama ruzuku kwa Vyama mbalimbali vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni. Hata hivyo, Hesabu za Vyama hivyo hazikuthibitishwa kuwasilishwa kwa Msajili wa Vyama wala kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kama inavyotakiwa kisheria.

5.10 Mishahara isiyolipwa kutowasilishwa Hazina Shs. 110,100,451.12

Ukaguzi wa mishahara kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 umebaini kuwa mishahara ya jumla ya Sh. 110,100,451.12 iliyotakiwa kulipwa watumishi ambao kwa sababu mbalimbali zikiwepo vifo au kustaafu, hawapo tena katika ajira katika Wizara, Idara, Wakala

www.JamiiForums.com

na Sekretarieti za Mikoa husika. Maelezo ya mishahara hiyo iliyokuwa bado kuwasilishwa Hazina ni kama ifuatavyo:

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/ Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1.	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	8,029,579.82
2.	80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	2,320,488.30
3.	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	10,639,600
4.	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS)	51,897,465
5.	74	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	22,091,007
6.	72	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	15,122,311
Jumla			**110,100,451.12**

5.11 Mali ambazo hazikuandikwa katika daftari la mali zisizohamishika

Uchunguzi wa Taarifa za Fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi umebaini kuwa mali zenye thamani ya Sh. 70,854,983,287.92 katika Wizara, Idara na Wakala mbalimbali hazikuandikwa katika daftari la mali zisizohamishika kama ifuatavyo:

Na.	Wizara, Idara na Wakala	Fungu	Kiasi(Shs)
1.	Jeshi la Kujenga Taifa	39	5,518,115,791
2.	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	14	5,903,313,042
3.	Ofisi ya Makamu wa Rais	31	13,661,411
4.	Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi	99	3,870,000,000
5.	Jeshi la Ulinzi (Ngome)	38	2,266,596,621.92
6.	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	57	53,063,606,800
7.	Mahakama Kuu ya Tanzania	18	219,689,622
Jumla			**70,854,983,287.92**

www.JamiiForums.com

5.12 Madeni na Mihadi1,330,599,248,033.19

Kifungu cha 17 (3) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inakataza Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kufanya malipo, kukubali malipo katika akaunti, kufanya matumizi bila kibali cha kufanya hivyo. Hata hivyo, katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2011, Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zilikuwa na madeni na mihadi ya kiasi cha Sh. 1,330,599,248,033.19 bila kibali cha kufanya hivyo. Hali ya madeni na mihadi ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Na.	Fungu	**Wizara, Idara na Wakala** na RAS	Bakaa ya fedha	Mihadi/Madeni	Nakisi isiyotengewa fedha (Shs)
1	16	Mwanasheria Mkuu wa Serukali	19,992,348.41	614,706,995.30	-594,714,646.89
2	18	Mahakama Kuu ya Tanzania	0	1,957,172,757.05	-1,957,172,757.05
3	19	Mahakama za Wilaya na Mwanzo	40,632,195.41	2,332,219,386.77	-2,291,587,191.36
4	35	Mkurugenzi wa Mashtaka	18,862,099	187,844,586.01	-168,982,487.01
5	38	Jeshi la Ulinzi (Ngome)	0	11,851,654,049	-11,851,654,049
6	42	Ofisi ya Bunge	40,631,595.40	582,566,072.49	-541,934,477.09
7	44	Wizara ya Viwanda na Biashara	52,458,048	734,596,925	-682,138,877
8	48	Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi	140,069,195	308,038,512.21	-167,969,317.21
9	49	Wizara ya Maji	381,381	3,839,569,053	-3,839,187,672
10	55	Tume ya Haki za Binadamu	1,595,325	157,852,999	-156,257,674
11	57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	1,324,349	738,245,005,177	-738,243,680,828
12	58	Wizara ya Nishati na Madini	4,112,553.04	139,326,254	-135,213,700.96
13	60	Mahakama ya Kazi	3,188.85	142,464,390	-142,461,201.15
14	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	675,741	593,536,574	-592,860,833
15	83	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	217,637	59,600,154	-59,382,517
16	90	Mahakama ya Ardhi	3,192,788.08	24,790,590	-21,597,801.92
17	96	Wizara ya Habari	233,014.69	3,615,777,165	-3,615,544,150.31
18	16	Mwanasheria Mkuu wa Serukali	19,992,348.41	614,706,995.30	-594,714,646.89

www.JamiiForums.com

19	19	Mahakama za Wilaya na Mwanzo	40,632,195.41	2,332,219,386.77	-2,291,587,191.36
20	35	Mkurugenzi wa Mashtaka	18,862,099	187,844,586.01	-168,982,487.01
21	55	Tume ya Haki za Binadamu	1,595,325	157,852,999	-156,257,674
22	60	Mahakama ya Kazi	3,188.85	142,464,390	-142,461,201.15
23	90	Mahakama ya Ardhi	3,192,788.08	24,790,590	-21,597,801.92
24	39	Jeshi la Kujenga Taifa	29,880,118.50	1,770,734,739.62	-1,740,854,621.12
25	33	Tume ya Maadili	232,447,933.62	268,138,440.00	-35,690,506.38
26	91	Tume ya Kudhibiti Madawa	6,045,818	12,106,738	-6,060,920
27	14	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	14,693,591.75	572,364,139.09	-557,670,547.34
28	78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	4,007,371	363,854,203	-359,846,832
29	66	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango	32,808,844	527,578,797.85	-494,769,953.85
30	61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	41	2,905,761,848	-2,905,761,807
31	53	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, jinsia na	8,602,468	2,034,032,772	-2,025,430,304
32	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	737,668,009	47,246,895,443	-46,509,227,434
33	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	2,208,602.35	690,950,856	-688,742,253.65
34	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	7,577,395	1,569,149,421	-1,561,572,026
35	27	Msajili wa Vyama vya Siasa	5,683,899.14	545,821,725.54	-540,137,826.40
36	26	Ofisi ya Makamu wa Rais	12,339,648	291,298,811.46	-278,959,163.46
37	25	Ofisi ya Waziri Mkuu	404,314.00	140,922,760	-140,518,446.00
38	31	Ofisi ya Makamu wa Rais	40,776,936	283,807,788.36	-243,030,852.36
39	43	Wizara ya Kilimo, Chakula na Maendeleo	4,635,173,807	5,528,060,214.68	-892,886,407.68
40	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	126,884,499.42	1,186,780,590.97	-1,059,896,091.55
41	64	Mahakama ya Biashara	511,663	438,998,136.44	-438,486,473.44
42	56	PMO - RALG	87,926	147,821,065	-147,733,139
43	88	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam	90,615,299	437,849,688	-347,234,389
44	40	Idara ya Mahakama	65,369,974.66	5,812,594,360.15	-5,747,224,385.49
45	94	Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma	6,008,513.98	70,869,317	-64,860,803.02
46	76	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	151,684,078	587,191,190	-435,507,112

www.JamiiForums.com

47	65	Wizara ya Kazi na Ajira	312,287,415.35	615,775,222.65	-303,487,807.30
48	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	1,053,118.43	356,211,696.41	-355,158,577.98
49	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	32,069,695.20	590,122,117.80	-558,052,422.60
50	71	Sekretarieti ya Mkoa wa Coast	14,821	599,884,021	-599,869,200
51	29	Idara ya Magereza	4,288,498	9,760,295,229	-9,756,006,731
52	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	7,610,970	193,565,755	-185,954,785
53	73	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	4,153,502	246,032,877	-241,879,375
54	46	Wizara ya Elimu na Maendeleo ya Ufundi	187,215,915	5,063,267,729	-4,876,051,814
55	86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	701,560	1,052,067,752.50	-1,051,366,192.50
56	87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	246,565	892,603,136.90	-892,356,571.66
57	98	Wizara ya miundombinu	2,313,841.00	422,299,119,935	-422,296,806,094.00
58	34	Wizara ya Mambo ya nje na Uhusiano wa	6,869,392.43	8,268,990,786.12	-8,262,121,393.69
59	28	Idara ya Jeshi la Polisi	203,460,779	35,155,973,446	-34,952,512,667
60	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	126,601.90	851,096,823.18	-850,970,221.3
61	72	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	12,448,313.00	1,254,135,620	-1,241,687,307
62	74	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	10495747	65,102,015	-54,606,268
63	79	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	698594.45	1,054,820,238.56	-1,054,121,644
Jumla				1,330,599,248,033.19	-1,323,193,052,550.

5.13 Ukaguzi wa Usimamizi wa Manunuzi

5.13.1 Utangulizi

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) iliwasilisha taarifa ya mwenendo wa manunuzi katika Taasisi mbalimbali ambayo imeonyesha kwa kiwango kikubwa mapungufu yaliyojitokeza katika taarifa ya mwaka uliopita. Kwa kutambua kazi nzuri iliyofanywa na Mamlaka hii, nimeamua kujumuisha masuala yaliyobainishwa na Mamlaka hii kwenye taarifa yangu.

Lengo la ukaguzi uliofanywa na PPRA ni kubaini kiwango cha uzingativu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004; Kanuni zake za 2005 na Tangazo la Serikali Na. 177 la 2007 na

www.JamiiForums.com

kwamba manunuzi yaliyofanywa yanawakilisha thamani halisi ya fedha zilizotumiwa na taasisi husika. Muhtasari wa matokeo na mapungufu yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo:

5.13.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Manunuzi

Kati ya Taasisi za Manunuzi 106 zilizokaguliwa, 36 zilikuwa ni Wizara, Idara na Wakala. Matokeo ya ukaguzi uliofanywa na PPRA umeonyesha wastani wa kiwango cha uzingativu cha asilimia 64. Utendaji wa wastani ulikuwa chini ya 50% katika viashiria viwili, yaani: Uchapishaji wa tuzo za mikataba (42%) na Ubora na kudhibiti (42%). Utendaji ulikuwa juu ya wastani (50% na zaidi) katika viashiria vifuatavyo kumi na moja: Kuanzishwa na muundo wa Bodi ya Zabuni (74%); Uanzishaji na muundo wa PMU (58%); Utendaji kazi wa Maafisa Masuuli, Bodi za Zabuni na Vitengo vya Manunuzi (64%); Utayarishwaji Mpango wa Mwaka wa Manunuzi (56%); kutekeleza idhinisho za lazima (61%); Matangazo ya kushindanisha wakandarasi/watoa huduma (89%); Muda wa maandalizi ya zabuni (72%); matumizi ya njia sahihi ya manunuzi (83%); Kuzingatia matumizi ya nyaraka mahsusi za zabuni kama ilivyoainishwa katika kanuni (79%); Kuweka kumbukumbu (56%) na usimamizi wa mikataba wa (66%). Katika eneo hili, Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa ilifikia kiwango cha juu cha utekelezaji wa 90% wakati Baraza la Michezo la Taifa lilifikia kiwango cha chini cha utekelezaji cha 8%.

(a) Taasisi za Manunuzi kutoa taarifa kwa Wakaguzi

Pamekuwepo ongezeko kubwa katika kutoa taarifa kuhusu tuzo za mikataba kutoka asilimia 65 mwaka jana hadi asilimia 81 katika mwaka 2010/11. Mwenendo wa utoaji taarifa kwa miaka mitatu iliyopita ilikuwa kama ifuatavyo:

2008/2009	2009/2010	2010/2011
59%	65%	81%

www.JamiiForums.com

(b) Asilimia ya manunuzi ikilinganishwa na jumla ya matumizi ya serikali

Kuna kupungua kidogo kwa manunuzi kama asilimia ya matumizi yote ya serikali. Kwa mfano, manunuzi ya mwaka wa fedha 2010/11 yalikuwa karibu 41% ya matumizi yote ya Serikali ikilinganishwa na 52% ya mwaka uliopita. Mwelekeo kwa miaka mitatu iliyopita ni kama ifuatavyo:

2008/2009	2009/2010	2010/2011
70%	52%	41%

(c) Utoaji vibali baada kutenda

Waombaji watatu (3) waliotaka vibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) baada ya kutenda walishindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa kuhusu maombi yao. Maombi hayo matatu ni kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu zabuni ya ununuzi wa pikipiki zenye thamani ya sh. milioni 125; Bohari Kuu ya Madawa kuhusu zabuni ya ununuzi wa madawa ya ARV yenye thamani ya Shilingi 1,675,780,000 na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya ununuzi wa magari 85 aina ya Land Rover yenye thamani ya Paundi za Kiingereza (GBP) 2,191,014.55 na sh. 183,600,000 kama gharama za hapa nchini

Mwelekeo unaonyesha kuwa idadi sawa ya maombi kwa ajili ya utoaji vibali baada kutenda ilipokelewa kama ilivyokuwa katika marekebisho yaliyofanyika wakati wa kufanya mapitio ya mwisho. Mapitio ya maombi hayo yalibaini udhaifu kama ifuatavyo:

i) Mipango mibovu na ya dharura ya manunuzi ya vifaa

ii) Kutokuwepo kwa sababu za msingi zilizosababisha manunuzi ya dharura kufanywa;

www.JamiiForums.com

iii) Kukosekana kwa sababu za msingi katika kutumia njia moja kama chanzo cha manunuzi;
iv) Vibali kwa ajili ya mchakato wa ununuzi kutopatikana;
v) Uongozi mbaya wa shughuli za manunuzi; na
vi) Malipo kwa wazabuni na watoa huduma kutofanyika kwa wakati.

(d) Kuundwa kwa Vitengo vya Manunuzi na kuvipa watumishi

Kuundwa kwa Vitengo vya manunuzi na kuvipa watumishi wenye sifa stahiki ni tatizo linalozikabili Taasisi za Manunuzi. Kaguzi zilizofanywa na PPRA zilibaini kuwa wastani wa kiwango cha uzingativu katika kuunda Vitengo vya manunuzi na kuvipa watumishi wenye sifa stahiki kilikuwa 56% kwa Wizara, Idara na Wakala.

(e) Mpango wa mwaka wa manunuzi

Mpango wa manunuzi ni jambo muhimu kwa vile unaisaidia Taasisi ya Manunuzi:
Kuepuka dharura zisizo za lazima; kujumuisha manunuzi pale inapowezekana ili kupata thamani ya fedha na kupunguza gharama za manunuzi; pale inapowezekana, kuingia mikataba endelevu kwa manunuzi yanayohitajika mara kwa mara; kuepuka manunuzi yasiyo jumuifu na kufuata utaratibu wa manunuzi unaofaa; na kupanga vyema vikao vya bodi za zabuni ili kupunguza gharama za uendeshaji. Mapitio ya utayarishaji wa mipango ya manunuzi ya mwaka unaonyesha kwa wastani uzingativu wa asilimia 46%, kwa Wizara, Idara na Wakala.

www.JamiiForums.com

(f) Usimamizi wa Mikataba

Katika kuchunguza utoshelevu wa usimamizi wa mikataba, timu za mapitio zilichambua masuala yafuatayo: Kama nyaraka za mikataba zilikuwa na taarifa zote muhimu, kama mikataba ilikuwa imesainiwa vizuri; uzingatiwaji muda; usimamizi wa mawanda ya mikataba; usimamizi wa ubora; usimamizi wa masuala ya mawasiliano; na usimamizi wa masuala ya gharama za mikataba. Ukaguzi umeonyesha kiwango cha uzingativu cha asilimia 64 na 41 katika usimamizi wa mikataba na udhibiti wa ubora wa mikataba kwa pamoja kwa Wizara, Idara, Wakala

Katika ujumla wake, tathimini ya usimamizi wa mikataba, ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Baadhi ya mikataba haikuwa imesainiwa
- Baadhi ya mikataba ilikosa nyaraka muhimu kama vile masharti ya mkataba, michoro, maelezo ya kina ya jinsi ya kutekeleza mkataba; mikataba mingine ilikuwa na nyaraka zisizohusiana ma mkataba kama vile tangazo la zabuni/dodoso la bei na maelezo kwa waomba zabuni
- Kutotumia kifungu cha fidia kwa kuchelewa kutekeleza mikataba
- Kutokuwa na vikao katika eneo la mradi kutathmini uekelezaji wa miradi.
- Kutokuwepo mipango ya kudhibiti na kutoa hakikisho la ubora katika utekelezaji wa mikataba; kazi zilizokamilika hazikufanyiwa tathmini kuona kama zimekidhi matakwa ya utekelezaji aliyopewa mkandarasi katika mkataba
- Taarifa za utekelezaji hazikuandaliwa
- Taarifa za wasimamizi wa mikataba hazikutayarishwa
- Muda wa utekelezaji mikataba kuongezwa bila kufuata taratibu
- Malipo kufanywa kwa kazi ambayo haijafanyika kwa kuzidisha kiwango cha kazi iliyokamilika

www.JamiiForums.com

- Kutokuteuliwa kwa Kamati za mapokezi na ukaguzi wa mali zilizonunuliwa kuthibitisha usahihi, ubora na idadi.
- Kutokuwepo kwa udhibiti wa ubora na usimamizi mbaya wa mikataba kilikosababishwa na ufinyu wa rasilmali (watu, fedha, magari, zana za kudhibiti ubora n.k.)
- Kukosekana miongozo katika uendeshaji wa miradi ya kijamii

(g) Utunzaji wa kumbukumbu

Tathmini iliyofanywa ilibaini kuwepo mapungufu makubwa kwenye orodha ya wazabuni, dodoso za bei, mikataba, nyaraka za manunuzi kutowekwa sehemu moja, upungufu katika usimamizi wa nyaraka na mikataba, upungufu wa sehemu za kutunzia nyaraka pamoja na ukosefu wa taratibu za kutunza mafaili. Matatizo haya yalisabisha wakaguzi kutopata uhakika kamili kuhusu zabuni zilizotangazwa na muda mwingi ulitumika kwa vile nyaraka hazikutunzwa sehemu moja. Athari za uwekaji mbaya wa kumbukumbu ni pamoja na usimamizi mbaya wa manunuzi; ufisadi, wizi na upotevu wa mali

5.14 Taarifa ya Idara ya Usimamizi mali za Serikali kuhusu usimamizi wa vifaa na mali

Sehemu ya XV ya kanuni za Fedha za Umma inashughulika na matakwa ya kuwepo uhakikimali huru wa vifaa vya Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa. Kwa hali hiyo, nimepokea taarifa ya uhakiki mali kwa mujibu wa Kanuni ya 245 (3) ya Kanuni ya Fedha zaUmma ya mwaka 2001 (ilivyorekebishwa 2004). Kutokana na Kanuni hiyo, Mhakiki Mali wa Serikali anatakiwa kubaki na nakala moja ya taarifa niyo kwa ajili ya kumbukumbu zake na kupeleka nakala moja kwa Afisa Masuuli mhusika, Katibu Mkuu Hazina, Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi wa

www.JamiiForums.com

Hesabu za Serikali.Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni iliyotajwa hapo juu, kitengo cha Uhakiki Mali chini ya Wizara ya Fedha, kilifanya uhakikimali wa kina katika wizara/Idara na Wakala 20 na Sekretariati za Mikoa 13 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2011.Nimeridhika na kazi iliyofanywa na kitengo hiki na nimeona kuwa taarifa walizotoa ni za manufaa na zenye mambo muhimu ya kuingiza katika taarifa yangu. Katika mwaka husika, pamekuwepo na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa vifaa kama ilivyoelezwa katika **Kiambatanisho IV.**

www.JamiiForums.com

www.JamiiForums.com

SURA YA 6

UCHAMBUZI WA HESABU JUMUIFU ZA TAIFA

Utangulizi

- Taarifa ya Mapato na Malipo
- Taarifa ya ulinganisho wa makisio na kiasi halisi kilicholipwa
- Taarifa ya Mtiririko wa fedha
- Taarifa ya malipo kwa aina ya kazi
- Vielekezi katika taarifa ya fedha

Hesabu Jumuifu za Taifa pamoja na viambatanisho huwezesha wasomaji kufanya uchambuzi na kutathmini utendaji wa Serikali wa mwaka na msimamo wa Serikali katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi unaohusika.

6.1 Masuala yaliyojitokeza mwaka huu na mapendekezo

6.1.1 Tathimini ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka

a) Matumizi ya kawaida (matokeo ya hesabu)
Katika mwaka huu wa fedha utendaji na uchangiaji unaolenga kuonesha uwazi na uwajibikaji katika Serikali kuu kwa Matumizi ya Kawaida ni kama ifuatavyo:

A	B	A-B
Makisio yaliyo idhinishwa (Sh)	Fedha iliyopelekwa (Sh)	Pungufu ya fedha iliyopelekwa (Sh)
7,858,873,015,000	7,587,424,923,903	271,448,091,097

A	B	A-B
Fedha iliyopelekwa (Sh)	Matumizi yaliyofanyika (Sh)	Bakaa ya fedha ambayo haikutumika (Sh)
7,587,424,923,903	7,581,154,383,395	6,270,540,508

Hesabu jumuifu kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka huu wa fedha katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa yalikuwa ni Sh. 7,581,154,383,395 ikilinganishwa na makisio yaliyo idhinishwa ya kiasi cha Sh.7,858,873,015,000.

www.JamiiForums.com

Taarifa za fedha jumuifu zinaonesha kwamba, jumla ya fedha zilizotolewa na hazina ni Sh. 7,587,424,923,903 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na matumizi halisi ya Sh.7,581,154,383,395 hii ikiwa na maana kwamba kiasi cha Sh.271,448,091,097 hakikupelekwa kulingana na makisio yaliyoidhinishwa. Kiasi cha Sh.6,270,540,508 kilibaki na kurudishwa katika akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali iliyopo Benki Kuu.

(ii) Matumizi ya Maendeleo (matokeo ya hesabu)

Katika mwaka huu wa fedha wa ukaguzi, matokeo ya heasbu kwa Matumizi ya maendeleo ilikuwa kama ifuatavyo:

A	B	A-B
Makisio yaliyo idhinishwa (Sh)	Fedha iliyopelekwa (Sh)	Pungufu ya fedha iliyotumwa (Sh)
3,750,684,569,000	2,223,684,150,465	1,527,000,418,535

A	B	A-B
Fedha iliyopelekwa (Sh)	Matumizi yaliyofanyika (Sh)	Bakaa ya fedha ambayo haikutumika (Sh)
2,223,684,150,465	2,218,032,826,357	5,651,324,108

Taarifa za fedha jumuifu zinaonesha kwamba, jumla ya fedha zilizotumika kwa shughuli za maendeleo ni Sh. 2,218,032,826,357 ikilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa ya Sh.3,750,684,569,000.

Jumla ya fedha iliyotolewa na hazina ilikuwa Sh.2,223,684,150,465 ikilinganishwa na kiasi cha Sh.

www.JamiiForums.com

2,218,032,826,357 ambazo ni fedha zilizotolewa na kutumika ambapo kiasi cha Sh.1,527,000,418,535 hakikutolewa kama ilivyoidhinishwa , halikadharika fedha ambayo haikutumika ilikuwa Sh.5,651,324,108 fedha ambazo zilirudishwa katika akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali iliyopo Benki Kuu.

(ii) Jumla ya matumizi ya Serikali Sh.9,799,187,209,752

Jedwali hapa chini linaonesha matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa kwa miaka 2009/10 na 2009/11.

Matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka Sh.6,237,494,869,945 mwaka fedha wa 2009/2010 hadi kufikia Sh.7,581,154,383,39 mwaka 2010/2011 sawa na asilimia 18, wakati matumizi ya maendeleo yamepungua kutoka Sh.2,284,901,099,246 mwaka wa fedha wa 2009/2010 hadi kufikia Sh.2,218,032,826,357 kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ikiwa ni sawa na asilimia 3.

Akaunti ya matumizi	2009/10 (Sh)	2010/11 (Sh)	%
Kawaida	6,237,494,869,945	7,581,154,383,395	18
Maendeleo	2,284,901,099,246	2,218,032,826,357	3
Jumla	**8,522,395,969,191**	**9,799,187,209,752**	**15**

(iii) Makusanyo ya maduhuli

Taarifa Jumuifu ya mapato iliyoishia tarehe 30 Juni, 2011 inaonesha makusanyo halisi ya Sh.11,425,587,436,564 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.11,823,445,375,763 hivyo kuleta upungufu wa makusanyo ya Sh.397,857,939,199 sawa na asilimia 3 ya makisio ya bajeti yaliyoidhinishwa.

www.JamiiForums.com

Mtiririko wa makusanyo ya maduhuli kwa muda wa miaka mitatu ya nyuma ni kama inavyoonekana hapa chini:

Mwaka	2008/2009 (Sh)	2009/2010 (Sh)	2010/2011 (Sh)
Makisio	7,704,909,780,498	10,063,686,670,897	11,823,445,375,763
Makusanyo halisi	6,427,630,892,809	7,928,122,248,611	11,425,587,436,564
Upungufu	1,277,278,887,689	2,135,564,422,286	397,857,939,199

Makusanyo katika akaunti ya kawaida yanatokana na kodi mbalimabali, makusanyo yasiyo ya kodi na makusanyo kutokana na raslimali za serikali ambapo makusanyo katika akaunti ya maduhuli ya maendeleo yanayotokana na misaada ya wafadhili, mikopo ya nje na ndani ya nchi.

6.2 Madeni ya Mikopo yanayodaiwa na Serikali Sh.480,229,660,682

Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2011, Serikali ilikuwa inadai kiasi cha Sh.480,229,660,682 kutoka katika taasisi zake mbalimbali pamoja na makampuni binafsi ikiwa ni mikopo iliyo tolewa kwa taasisi na kampuni hizo ukilinganisha na Sh.459,443,095,386 zilizotolewa taarifa kwa kipindi cha mwaka uliopita kama inavyoonesha kwenye jedwali hapa chini. Hili ni ongezeko la asilimia tano (5%). Deni hili halijaonesha mchanganuo wa umri wake na kuonesha ulipaji wake.(**Kiambatanisho V)**

6.3 Taarifa ya Madeni yasiyolipwa Sh.577,537,084,848

Tathimini ya hesabu jumuifu za serikali imebaini kuwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30.06.2011 zilikuwa zimelimbikiza madeni ya Sh. 577,537,084,848 hii ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 259.3 ukilinganisha na

www.JamiForums.com

deni lililotolewa taarifa mwaka jana la Sh.160,756,067,190.
Utaratibu huu wa kulimbikiza madeni ni kinyume kabisa na utaratibu wa makisio ya fedha taslimu ambao ndiyo mfumo wa bajeti ya Serikali kuu.Serikali haijaweka mfumo wowote kwa ajili ya kuikabili hali hiyo.

6.4 Taarifa ya deni la Taifa Sh.14,441,617,939,770.20

Taarifa ya hesabu jumuifu inaonyesha kwamba deni la taifa limeongezeka kwa 38% kutoka Sh.10,503,806,011,884.90 mwaka 2009/10 hadi Sh.14,441,617,939,770.20 mwaka 2010/11, mapendekezo yangu kwa serikali kupunguza mikopo ya fedha ya bajeti kwa kuimarisha ukusanyaji wa kodi na kupanua wigo wa kodi katika maeneo kama vile sekta ya madini hayajatekelezwa.

Aina ya deni	2007/2008	2008/2009	2009/2010	2010/2011
Deni la nje	4,601,657,485,229	5,386,646,362,543	7,747,903,803,161	10,734,316,352,447
Deni la ndani	1,875,794,357,188	2,234,640,367,491	2,755,902,208,703	3,707,301,587,322
Jumla ya deni	6,477,451,842,417	7,621,286,730,034	10,503,806,011,885	14,441,617,939,770
Kuongezeka kwa deni	1,002,439,757,563	1,143,834,887,617	2,882,519,281,851	3,937,811,927,885
% Deni la nje	26%	17%	44%	38.5%
% Deni la ndani	2%	19%	23%	34.5%
% Jumla ya deni	18.31%	17.66%	39.27%	38%
Pato la Taifa (GDP)	7.3%	7.1%	6.0%	6.5%

6.5 Taarifa ya malimbikizo ya Maduhuli

Taarifa inaonyesha kuwa, malimbikizo ya maduhuli ylipungua kutoka Sh.116, 320,437,345 katika mwaka 2009/10 hadi Sh. 26697463538 mwaka 2010/11, sawa na 77%. udhibiti uliowekwa na Serikali bado hadi sasa haujaboreshwakwa nia ya kuinua ukusanyaji wa mapato.

www.JamiiForums.com

6.6 Taarifa ya mali na vifaa vingine Sh.38,292,059,659

Taarifa jumuifu ya mali na vifaa vingine ilionyesha kuwa tarehe 30 Juni 2011 Serikali ilikuwa na jumla ya Sh.38 292,059,659.00. Hii ni ongezeko la% 128 kutoka ile ya mwaka uliopita ya Sh.16, 806,978,964. Ilionekana kuwa mali na vifaa vingine mara nyingi vinavyotumika (consumables) vilinunuliwa mwisho wa mwaka bila udhibiti ili kuhakikisha kwamba fedha zilizopangwa katika bajeti ya mwaka husika zinatumika

6.7 Taarifa ya upotevu Sh.11,152,048,065

Taarifa ya hesabu jumuifu ilionyesha kwamba jumla ya hasara iliyoingiwa na Serikali katika maeneo ya fedha za umma, mali na madai ya yaliyotelekezwa, ilipungua kutoka Sh.11,152,048,065 katika mwaka 2009/2010 hadi Sh.7,998,801,086 mwaka 2010/2011, huu ukiwa ni upungufu wa Sh.3,153,246,979 sawa na 28%. Serikali haijachukua ama juhudi madhubuti ili kupunguza matukio ya hasara au wakati kuanzisha mchakato kwa ajili ya Bunge kufuta hasara hizi. Azimio la mwisho la kufuta hasara ni na. 10/2009 lililotolewa tarehe 31 Julai, 2009.

6.8 Madeni ya Serikali ambayo hayakuonyeshwa katika hesabu

Taarifa ya hesabu Benki Kuu ya Tanzania zilizochapishwa kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2011 zilijumuisha madeni mbalimbali ambayo Serikali inadaiwa na Benki Kuu. Hata hivyo, madeni hayo hayakuonyeshwa katika taarifa ya hesabu jumuifu kama kiasi ambacho kinatakiwa kulipwa na Selikali kwa Benki Kuu kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

(i) Nakisi ya Serikali Benki Kuu Sh.548.332 bilioni

Hesabu zilionyesha kuwaSerikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) mnamo tarehe 30 Juni 2011 ilikuwa na nakisi ya Sh. 548,332,614,000 (2010:

www.JamiiForums.com

Sh. 429,466,112,000) katika akaunti yake iliyoko benki. Kuu.

ii) Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi Sh.15.461 bilioni jumla ya Sh.15.461 bilioni zilionyeshwa kama deni kutoka kwa Serikali kuhusiana na fedha ambazo Benki Kuu ya Tanzania iliikopesha Selikali ili kuwezesha utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji wa kiuchumi.

(iii) Gharama za kupunguza mzunguko wa fedha katika uchumi: Sh.22.195 bilioni

Kiasi cha Sh.22.195 bilioni (2010: Sh.26.851.5 bilioni) kilionyeshwa na Benki Kuu mnamo tarehe 30 Juni 2011 kama deni ambalo Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilikuwa inadaiwa na Benki Kuu kuhusiana na gharama za kupunguza mzunguko wa fedha katika uchumi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki Kuu ya Tanzania hugawana gharama za usimamizi wa ukwasi kwa msingi utaratibu uliokubaliwa katika Mkataba wa Makubaliano

(iv) Riba kutokana na nakisi ya Benki Kuu Sh.17.530 bilioni

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2011 Serikali ilikuwa na deni la riba ya Sh.17.530 bilioni (2010: Sh.3.456.6 bilioni) kutokana na nakisi ambayo selikali ilikuwa nayo katika kipindi cha mwaka 2010/2011. Kulingana na sehemu ya 34 ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, Serikali inatakiwa kulipia riba kutokana na nakisi hiyo.

6.9 Amana za Serikali ambazo hazikuonyeshwa katika katika taarifa za fedha

Taarifa za hesabu za Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2011 zilionyesha kuwa Serikali ilikuwa na amana mbalimbali katika akaunti za. Hata hivyo, amana hizo hazikuonyeshwa katika taarifa jumuifu ya hasabu za kama ifuatavyo:

www.JamiiForums.com

(i) Fedha zilizowekwa BoT na Selikali kulipia Madeni ya nje: Sh. 25.059 bilioni

Kiasi cha Sh. 25.059 billion kilipokelewa na Benki Kuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kulipia madeni ya Selikali yaliopo katika fedha za kigeni. Kiasi hiki hakijachukuliwa na Selikali kwa muda mrefu.

(ii) Fedha za kulipia madeni ya Serikali Sh.25.562 bilioni

Kiasi hiki kinahusiana na fedha zilizowekwa na Serikali kulipia madeni ya Serikali baada ya kuanzisha mfumo wa malipo wa elektroniki.

(iii) Dhamana ya Mfuko wa miradi ya Maendeleo wa Sh.11.166 bilioni

(iv) Mfuko huu ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuendeleza miradi ya mikopo ya maendeleo kwa ajili ya kutengeneza na kuuza bidhaa nje ya nchi.Mnanao tarehe 30 Juni 2011, Serikali ilikuwa na mtaji uliotolewa mwaka 2003/04 na 2005/06 katika Mfuko huu ulofikia Sh.56.500 bilioni. Kiasi cha Sh.15.771.9 milioni kilipatikana kama riba kutokana na mikopo iliyotolewa, wakati jumla ya Sh.2,448.54 milioni ilipatikana kutokana na riba ya kuwekeza katika amana za Serikali. jumla ya Sh.61, 668.2 milioni hadi sasa zimetolewa kama mikopo kwa makampuni ya maua na mboga. Mnamo tarehe 30 Juni 2011 Mfuko ulikuwa na urari wa Sh.11,166.7 milioni

(Vi) Mfuko wakudhamini wauzaji bidhaa nje ya nchi: Sh.41.841 bilioni

Mfuko huu ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2001 chini ya

www.JamiiForums.com

Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya kuuza bidhaa nje ya nchi. Mfuko hutoa dhamana ya benki za biashara kukinga hatari ya wafanyabiashara hawa kushindwa kulipa mikopo yao. Katika kipindi cha mwaka 2010/11, Serikali iliongeza mtaji wa Sh.4, 309.5 milioni. Mnamo tarehe 30Juni, 2011 Mfuko ulikuwa na urari wa Sh.46,904.3 milioni(2010: Sh.31, 783,500,000)

(V) Mfuko wa kuuza Madeni: Sh.2.098 bilioni

Kiasi hiki ni bakaa ya fedha zilizowekwa na Serikali kwa ajili ya kubaadili na kuuza madeni zilizozuiliwa katika akaunti zikiwa zinasubiri taarifa za maendeleo ya kazi kutoka kwa walengwa ili benki kuu iweze kufanya malipo hao.

(Vi) Fedha zilizotokana na kusamehewa madeni na IMF Sh.10.560 bilioni

Kiasi hiki kinahusiana na fedha ambazo awali zilitolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali kwa ajili ya kusaidia kuboresha mizania ya malipo malipo na mauzo ya vifaa na huduma nje ya nchi. Baadaye Serikali kupitia ilipewa fedha hiyo kupitia Mpango wa kusamehe madeni. Wakati wa mwisho wa 2009/2010 akaunti hiyo ilikuwa na bakaa ya Sh.85, 716,634

(Vii) Benki ya Maendeleo Kilimo Tanzania ya sh. 30.0 bilioni

Kiasi cha shilingi 30,000 milioni kinahusiana na fedha zilizotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuchangia kutoka bajeti ya 2009/10 kuwezesha kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Bakaa ambayo ilikuwepo katika akaunti Benki Kuu mwisho wa mwaka wa fedha 2009/2010 ilikuwa Sh.50,000 milioni

www.JamiiForums.com

6.10 Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa na Serikali Sh.514,959,828,292

Jedwali la 38 lililokuwa likionyesha taarifa ya fedha ya dhamana za Serikali, hata hivyo lilijumuisha mikopo ambayo Serikali iliyapatia makampuni sita (6) ya maua na moja (1) la mifugo. Hata hivyo, kiasi hicho kilionyeshwa kama mikopo ambapo ilijumuishwa pamoja na mikopo ya kibiashara ya Sh.514,959,828,292 ambayo walengwa waliipata kutoka taasisi mbalimbali za fedha. Mikopo hii kwa makampuni haya ni mali ya Serikali na si madeni.

www.JamiiForums.com

SURA YA 7

7.O UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI

7.1. Utangulizi

Sura hii, inachambua misingi ambayo imepelekea utoaji wa aina fulani ya maoni ya ukaguzi. Uchambuzi huu una

lengo la kufafanua vigezo na msingi iliyotumika katika kutoa maoni ya ukaguzi kama ilivyojadiliwa katika sura iliyotangulia.

Hati ya ukaguzi ni maoni rasmi au kukataa kutoa maoni kunakotolewa na mkaguzi huru kutokana na ukaguzi au tathmini iliyofanywa kwa Taasisi au Idara yake (mkaguliwa). Hati hii hutolewa ili kumwezesha mtumiaji wa taarifa za fedha kama hakikisho ili aweze kufikia maamuzi kutokana na matokeo ya ukaguzi uliofanywa.

Hati ya ukaguzi huchukuliwa kama nyenzo muhimu wakati wa kutoa taarifa za fedha kwa watumiaji. Inakusudia kulishauri Bunge na watumiaji wengine wa taarifa za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango kubalifu vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) ikiwemo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kuzingatia Sheria na Kanuni nyingine zilizowekwa.

Kwa lugha ya kawaida, hati ya ukaguzi ni hakikisho kwamba taarifa ya fedha iliyowasilishwa na mkaguliwa kwa kiwango kikubwa ni sahihi na ya kuaminika kwa ajili ya kufanya maamuzi ya Serikali kama vile Serikali kutathmini kama fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa zimetumika kwa manufaa ya Umma. Ni muhimu kutambua kwamba hati ya ukaguzi inayotolewa kwa taarifa za fedha siyo hakikisho la moja kwa moja kwamba hali ya kifedha ya Taasisi ni nzuri na sahihi kabisa kuweza kutegemewa katika kufanyia maamuzi. Hati ya ukaguzi ni maoni tu kwamba taarifa iliyowasilishwa ni sahihi na haina makosa makubwa

www.JamiiForums.com

ambapo maamuzi mengine huachiwa mtumiaji wa taarifa kuamua.

7.2 Aina ya hati za ukaguzi

Kuna aina tano (5) za hati za ukaguzi, kila moja ikieleza mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Hati hizo ni kama ifuatavyo:

- **Hati inayoridhisha**
  Wakati mwingine hati hii huchukuliwa na wengi kama "hati safi". Aina hii ya hati hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ikihusisha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni.

- **Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo**
  Katika mazingira fulani, hati ya ukaguzi inayoridhisha huweza kurekebishwa kwa kuongeza aya yenye masuala ya msisitizo yanayodokeza masuala muhimu ambayo yasiporekebishwa na mkaguliwa yanaweza kusababisha kutolewa kwa hati yenye shaka katika ukaguzi unaofuata. Kuongezwa kwa aya ya masuala ya msisitizo hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa.

Madhumuni ya masuala ya msisitizo ni kutoa uelewa zaidi kwa hali iliyotokea wakati wa ukaguzi licha ya kutolewa kwa hati ya ukaguzi inayoridhisha.

- **Hati yenye shaka**

  Hali na mazingira inayosababisha kutolewa kwa hati hii, huwa katika kundi moja au mawili ambayo ni:

www.JamiiForums.com

- Kunapokuwa na mashaka ambayo husababisha mkaguzi ashindwe kutoa hati ya ukaguzi.
  Mambo yanayoweza kusababisha kutolewa kwa hati hii ni haya yafuatayo:
- Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo
- Bidhaa na huduma zimenunuliwa bila kuwa na hati za kupokelea hivyo kukosekana uhakikisho kama zimepokelewa na kuingizwa katika vitabu
- Malipo mbalimbali kukosa viambatanisho
- Stakabadhi za maduhuli kutowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi
- Mali zinazomilikiwa au kununuliwa kukosa majedwali. Hii inasababisha mashaka ya kuwepo kwa mali hizo
- Kutopatikana kwa ushahidi wa mapokezi ya fedha zilizolipwa. Kutokuwepo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji unaweza kusababisha upotevu wa fedha. Katika hali hii kunakuwa na ufinyu wa mawanda ya ukaguzi.

Pale ambapo mkaguzi anapotoa maoni yanayotofautiana na hali halisi ya taarifa ya fedha zilizotolewa (kutokubaliana na taratibu kubalifu za utunzaji na uzingatiaji wa sheria na kanuni).

Kutokubaliana na uongozi katika njia iliyo bora ya utunzaji wa kumbukumbu na uzingatiaji wa sheria hutokea katika mazingira yafuatayo:

- Mali zinazomilikiwa na Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kutoingizwa katika rejista.
- Mali zilizonunuliwa kutoingizwa vitabuni na hivyo kutolewa na matumizi yake kutoweza kuthibitishwa.
- Kutobainishwa salio la benki katika vitabu vya fedha
- Wakati kumbukumbu za hesabu zinapokosekana, kutokamilika au kutokuwa sahihi.

www.JamiiForums.com

- Kutobainishwa kikamilifu kwa sera ya uhasibu iliyotumika
- Pale ambapo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zinapotumia njia isiyo sahihi kama vile viwango vya uchakavu visivyo sahihi

Kwa hali hiyo, hati yenye shaka inaonyesha kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa ni sahihi isipokuwa kwa madhara yatokanayo na masuala halisi ya kiukaguzi yaliyogunduliwa.

(iii) Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha hutolewa inapogundulika kuwa taarifa za fedha za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa kiasi kikubwa si sahihi zinapoangaliwa katika ujumla wake, hazikuandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inayoelezea kuwa taarifa zilizopo siyo sahihi na haziaminiki katika kupima matokeo ya uendeshaji katika Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa.

Maelezo ya hati isiyoridhisha huwa wazi ambapo ninaeleza kwamba taarifa za fedha hazikuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka2001 (ilyorekebishwa 2004).

(iv) Hati mbaya

Hati mbaya ambayo hujulikana kama kukataa kutoa hati, hutolewa wakati ninaposhindwa na hivyo kukataa kutoa hati kwa taarifa za fedha. Aina hii ya hati hutolewa ninapojaribu kufanya ukaguzi kwa Taasisi na kushindwa kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kusababisha kutotoa hati ya ukaguzi. Hali

www.JamiiForums.com

inayosababisha kutolewa kwa hati mbaya inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uhuru au ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ama kwa makusudi au la, mkaguliwa kukataa kutoa ushahidi na taarifa kwangu katika maeneo muhimu kwenye taarifa za fedha na panapokuwa na mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa.

Jedwali: Misingi ya kutoa hati ya ukaguzi

Hali na sababu zinazosababisha kutolewa kwa hati ya ukaguzi	**Masuala yenye athari lakini si mazito**	**Masuala yenye athari na mazito**
Taarifa za fedha ni za kupotosha	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha
Kushindwa kupata ushahidi wa kutosha na sahihi		Hati mbaya

Jedwali hilo hapo juu hutoa mwongozo wa namna hati za ukaguzi zinavyotolewa, tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

Pale ninapogundua masuala yanayosababisha kutokubaliana na masuala hayo ni yenye athari lakini si mazito, ninatoa hati yenye shaka (isipokuwa pale ambapo masuala yana athari na ni mazito hati isiyoridhisha hutolewa)

(b) Pale ambapo matokeo ya ukaguzi yanasababisha kuwepo mashaka na:

(i) Mashaka hayo ni makubwa yana athari lakini si mazito, hati yenye shaka hutolewa

(ii) Mashaka yana athari na ni mazito, hati mbaya hutolewa

www.JamiiForums.com

Madhumuni ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kutoa ripoti ya ukaguzi ambayo inaonyesha uwiano ulio wazi, kuweka msisitizo kwa mambo muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na uongozi wa wakaguliwa na kubainishwa fursa za kuboresha utendaji.

Jumla ya Wizara 60 na Sekretarieti za Mikoa 21 zilikaguliwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

7.3 Hati inayoridhisha isiyokuwa na masuala ya msisitizo

Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 11 (13%) kati ya 81 zilizokaguliwa mwaka huu zilipewa hati inayoridhisha isiyo na masuala ya msisitizo kama inavyoonekana katika Kiambatisho VII

7.4 Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

Matokeo ya ukaguzi ya mwaka huu yalionyesha kuwa kati ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 81 zilikaguliwa, 58 au asilimia 72% zilipewa hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo.

7.5 Hati yenye shaka

Kati ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 81 zilizokaguliwa 12 au asilimia 15 zilipewa hati zenye shaka.

7.6 Hati isiyoridhisha

Hapakuwa na fungu lolote katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 81 zilizokaguliwa katika mwaka 2010/2011 lililopewa hati isiyoridhisha ikilinganishwa na mwaka 2009/2010 ambapo Mafungu mawili (2) au asilimia 2 yalifanya vibaya na hivyo kupewa ya aina

www.JamiiForums.com

hiyo.

7.7 Hati mbaya

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2010/2011 hapakuwa na hali iliyosababisha ufinyu wa wigo wa ukaguzi kiasi cha kulazimika kutoa hati mbaya ikilinganishwa na hati moja iliyotolewa mwaka 2009/2010 Sekretariati ya Mkoa wa Dodoma

Jedwali lifuatalo vinaonyesha aina ya hati zilizotolewa kwa Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa katika taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011.

Maelezo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Jumla
Wizara/Idara	11	39	10	0	0	60
Sekretarieti za Mikoa	0	19	2	0	0	21
Jumla	11	58	12	0	0	81

7.8 Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

Ufuatao ni mchanganuo wa sababu za kutoa hati inayoridhisha yenye mambo ya msisitizo kwa kila fungu:

1.	**Fungu 16: Mwanasheria Mkuu wa Serikali**
	• Hapakuwa na kumbukumbu nzuri za utunzaji wa vifaa kutokana na udogo wa chumba cha stoo. Mpangilio wa mali ulikuwa sio wa kuridhisha pia usio salama. Mali yenye thamani ya Sh. 472,417,987.87 inayomilikiwa na Fungu 16 na 35 ilikuwa imehifadhiwa pamoja katika chumba

www.JamiiForums.com

	hicho cha stoo. • Mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 41,777,458 zilizonunuliwa katika mwaka unaotolewa taarifa hazikuwekwa alama za utambulisho (codification) na hazikuingizwa katika daftari la mali.
2.	**Fungu 22: Deni la Taifa na Huduma za Ujumla**
	• **Mapokezi ya Sh. bilioni 1.2 kutoka NMB kwa ajili ya wastaafu hewa** Kiasi cha Sh. Bilioni1.2 kilirejeshwa Hazina na NMB baada kukaa kwa muda mrefu bila wadai halali kwenda kudai fedha hizo. Hii inaonyesha Hazina kutokuwa na udhibiti makini katika kulipa mafao ya pensheni kwa wastaafu, jambo linaloweza kusababishwa kulipwa kwa wastaafu hewa. • **Malipo ya pensheni kwa wastaafu hewa Sh.71,422,610** Ukaguzi wa majaribio wa malipo ya pensheni umebaini kuwa kiasi cha Sh. 71,422,610 kililipwa kwa wastaafu waliofariki. Hapakuwa na utaratibu wowote wa kuhakiki uwepo wa wastaafu hao. Udhaifu huu katika udhibiti umesababisha fedha za umma kutumika pasipo manufaa yoyote kupatikana. • **Udhaifu katika kusimamia dhamana za Serikali** Wizara ya Fedha haijaweka viwango vya dhamana kinyume na Kifungu cha 13 cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Ruzuku ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2003). Aidha, dhamana za jumla ya Sh. 204,270,357,672 zikijumuisha msaada wa ugharamiaji wa Sh. 64,321,859,470 na dhamana kwa kuuza bidhaa nje Sh. 197,838,168,202 zilitolewa kwa makampuni binafsi kinyume na Sheria ambayo inataka dhamana hizo zitolewe kwa makampuni ya umma pekee.

www.JamiiForums.com

	• **Kukosekana kwa Waraka wa Makubaliano kati ya Serikali na Benki Kuu ya Tanzania** Imeonekana wakati wa ukaguzi kwamba, mara kadhaa Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikijihusisha na masuala mbalimbali ya usimamizi ikiwepo urejeshwaji wa mikopo na soko la fedha la ndani kama vile minada ya dhamana za Hazina pasipo kuingiwa mikataba rasmi na wahusika jambo lanalofanya uwajibikaji kisheria wa pande husika kuwa mgumu.
3.	**Fungu 26: Ofisi ya Makamu wa Rais**
	• Taarifa za fedha za Ofisi ya Makamu wa Rais zimeonyesha kuwepo kwa kiasi cha Sh. 291,298,811.46 ikiwa ni mihadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hii ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu.
4.	**Fungu 27: Msajili wa Vyama vya Siasa**
	• Masurufu ya jumla ya Shs. 38,437,000 hayakurejeshwa hadi wakati wa ukaguzi kinyume na matakwa ya kifungu cha 103 (1) cha Kanuni za Fedha ya Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) zinazotaka masurufu kurejeshwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kazi husika kukamilika. • Malipo ya jumla ya Sh.23,965,716.14 hayakufanyiwa ukaguzi wa awali kabla ya kulipwa • Malipo ya jumla ya Sh.134,356,708 yalilipwa kutoka vifungu visivyohusika na hivyo kufanya bajeti kutoonekana kama chombo cha udhibiti wa matumizi.
5.	**Fungu 28: Idara ya Jeshi la Polisi**
	• **Uhamishwaji fedha wenye shaka kwenda katika akaunti ya Amana Sh. 924,488,391** Maelezo ya ufafanuzi katika taarifa za fedha yanaonyesha kuwa Akaunti ya Amana ilikuwa na kiasi cha Sh. 1,595,412,430 kinachojumuisha Sh. 924,488,391

www.JamiiForums.com

	zilizohamishiwa katika akaunti hiyo mwishoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011. Mchanganuo wa fedha katika akaunti hiyo unaonyesha kuwa kulikuwa na bakaa ya Sh. 670,924,039 kutoka mwaka 2009/2010 ikimaanisha kuwa fedha zilizohamishiwa katika akaunti hii hazikuwa na mihadi yoyote kwani zilikuwa zimekaa bila kutumika kwa zaidi ya miezi sita (6) • **Masuala yasiyoshughulikiwa katika taarifa za benki** Uongozi wa Jeshi la Polisi haujashughulikia masuala yahusuyo hundi zenye thamani ya Sh.2,291,077,374.80 zilizolipwa ambazo wahusika hawajaziwasilisha benki kwa muda mrefu ili zilipwe. **Masuala mengineyo** Uongozi wa Jeshi la Polisi haujatayarisha na kuwasilisha Hazina kwa ajili ya kuidhinishwa, taarifa ya potevu ya kiasi cha Sh. 56,701,500 pamoja na hukumu ya mahakama • **Madeni na Mihadi Sh. 34,231,485,055** Jeshi la Polisi limelimbikiza madeni ya kiasi cha Sh. 34,231,485,055 yahusuyo mali na huduma hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hii ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu.
6.	**Fungu 29: Idara ya Magereza**
	• Malipo ya jumla ya Sh. 57,147,108 yalilipwa kutoka vifungu visivyohusika na hivyo kufanya bajeti kutoonekana kama chombo cha udhibiti wa matumizi. • Idara iliingia katika mkataba na M/S Hughes Motors (T) Ltd wa kununua magari matano (5) aina ya 4WD pick up single cabin. Hata hivyo, Idara haikuitoza Kampuni ya magari adhabu ya kiasi cha Sh. 24,737,175 kwa kuchelewa kuwasilisha magari hayo kwa mujibu wa mkataba. • Malipo ya kiasi cha Sh. 8,887,000 yalifanywa kwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa hati ya malipo Na. 29 VC 10000810 ya tarehe 29 Septemba, 2010 bila kuauniwa na

www.JamiiForums.com

	nyaraka kinyume na Kanuni ya 86 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004).
7.	**Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais**
	Mali za kudumu zisizoandikwa katika daftari la mali Sh.13,661,411 Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 ukaguzi wa mali za kudumu ulibaini dosari zifuatazo: • Mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 13,661,411 zilizonunuliwa katika mwaka wa fedha husika hazikuandikwa katika daftari la mali. • Jenereta ya kuzalisha umeme aina ya Caterpillar 500 USA SR- 700G03580 yenye uwezo wa kuzalisha 500KV haikuandikwa katika daftari la mali. • **Madeni na Mihadi Sh. 283,807,788.36** Taarifa za fedha za Ofisi ya Makamu wa Rais zimeonyesha kuwepo kwa kiasi cha Sh. 283,807,788 36ikiwa ni mihadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hii ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu.
8.	**Fungu 33: Sekretarieti ya Maadili**
	• Kulikuwa na masuala ya miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa yenye thamani ya Sh. 11,870,000 • Sekretarieti ya Maadilli haina Sera ya jinsi ya kutambua na kushughulikia viashiria vya hatari mbalimbali
9.	**Fungu 34: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**
	• **Gharama za nauli ya ndege kulipwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 26,120,025** Kiasi cha Sh. 105,777,331 kilipwa kwa ajili ya huduma ya tiketi za ndege kwa Wizara. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa kiasi kilichoonyeshwa katika Ankara ya madai iliyoambatanishwa na tiketi kilikuwa Sh.

www.JamiiForums.com

	79,657,306 na hivyo kusababisha kuwepo kwa malipo zaidi ya Sh. Shs.26,120,025. • **Kukosekana kwa stakabadhi za kukiri mapokezi ya Sh. 105,919,530** Katika mwaka wa fedha unaotolewa taarifa, Wizara ililipa kiasi cha Sh. 238,291,770 kwa M/s Antelope Tours & Safari Ltd. Kati ya fedha zilizolipwa, kiasi cha Sh. 105,919,530 hakikuwa na stakabadhi za kukiri mapokezi. Hii ni kinyume na Kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). • **Madeni yasiyolipwa Sh. 8,268,990,786.82** Wizara ilikuwa na madeni ya jumla ya Sh. 8,268,990,786.82 ambayo kati yake, kiasi cha Sh. 3,932,190,284.94 ni madeni ya Makao Makuu na Sh.4,336,800,581.88 yanahusu Balozi za Tanzania nchi za nje. Kuwepo kwa madeni haya ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu. • **Mikataba ya kukusanya maduhuli ya visa isiyokuwa na kipengele cha malipo kwa wakala** Wizara iliingia katika mikataba na Balozi Ndogo 16 ya kukusanya maduhuli yatokanayo na mauzo ya visa. Hata hivyo, mikataba iliyosainiwa haikuwa na kipengele kinachoonyesha kiasi ambacho balozi hizo ndogo zinatakiwa kubakiza kama malipo ya uwakala. Hali hii imesababisha kila ubalozi mdogo kutumia viwango tofauti vya kubakiza mapato kutegemeana na maduhuli yaliyokusanywa. • **Udhaifu katika kudhibiti malipo ya masurufu** Watumishi wane wa Wizara walilipwa masurufu mapya ya safari kabla ya kufanya marejesho ya masurufu mengine waliyopewa hapo awali ya jumla ya Sh. 31,580,318.14
10.	**Fungu 37: Ofisi ya Waziri Mkuu**
	• **Madeni yasiyolipwa na Mihadi Sh. 1,569,149,421** Kulikuwa na madeni na mihadi ya jumla ya Sh.

www.JamiiForums.com

	1,569,149,421 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011. Kuwepo kwa madeni haya ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu na yanaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 kwani sehemu yake inaweza kutumika kulipia madeni ya nyuma. • **Kutotayarishwa heabu za Mfuko wa Taifa wa Maafa** Katika mwaka wa fedha unaotolewa taarifa, Mfuko wa kusaidia Maafa ulipokea kiasi cha Sh. 8,599,141,144 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali unaosimamia dharura za kitaifa. Hata hivyo, imebainika kuwa Hesabu za Mfuko wa kusaidia athari za maafa hazikutayarishwa. Kwa hali hiyo, haikuwezekana kukagua na kutoa maoni kuhusu usahihi wa fedha zilizolipwa kwa wahanga wa majanga. • **Kutobainisha wanaodaiwa fedha katika Mfuko wa Kusaidia athari za majanga Sh. 3,019,349,946** Kulikuwa na wadaiwa wa kiasi cha Sh. 3,019,349,946 zinazotokana na mauzo ya chakula cha msaada kwa wilaya mbalimbali. Wadaiwa hawa hawakuonyeshwa katika taarifa za fedha za fungu hili. • **Chakula cha msaada tani 3,759.89 kilichopelekwa katika Halmashauri lakini hakikupokelewa** Ukaguzi umebaini kuwa Tume ya Taifa inayoshughulika na misaada kwa maafa iliidhinisha jumla ya tani 8,262.90 kama chakula cha maafa. Hata hivyo, imebainika kuwa chakula kilichopelekwa katika Halmashauri ni tani 7,013.20 tu na hivyo kuacha tofauti ya tani 1249.7 bila maelezo • **Fedha zilizotolewa kusaidia ujenzi kwa waliokumbwa na maafa kutotumika Sh. 539,379,189** Fedha kiasi cha Sh. 539,379,189 zilizotolewa kwa waathirika wa njaa na mafuriko ili kusaidia chakula

www.JamiiForums.com

	na ujenzi wa nyumba zilizobomoka zilikuwa katika akaunti hadi mwisho wa mwaka wa fedha unaotolewa taarifa. Kwa mantiki hii, ni wazi kuwa lengo la misaada hiyo kutolewa mapema ili waathirika waondokane na njaa na adha ya makazi halijafikiwa. • **Malipo yenye shaka Sh. 1,326,002,959** Taarifa za fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh. 1,326,002,959 kililipwa kwa Taasisi isiyo ya Kiserikali iitwayo "Financial Deepening Services Trust (FDST)" kwa ajili ya utekelezaji wa mradi chini ya Ofisi hiyo uitwao "Private Sector Competitiveness Project (PSCP)". Hata hivyo, ukaguzi wa hesabu za FDST umebaini kuwa hakuna fedha zilizopokelewa FDST kutoka PSCP katika mwaka wa fedha husika. Aidha, ukaguzi umebaini kuwa kiasi hicho cha fedha kilipelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa PSCP. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali – Zanzibar atajulishwa kuhusu fedha hizo.
11.	**Fungu 38: Jeshi la Wananchi wa Tanzania (Ngome)**
	• **Gharama za matibabu nje ya nchi kuonyeshwa kama ruzuku Sh. 467,480,778** Fungu hili lilifanya malipo ya Sh. 467,480,778 kama gharama za matibabu nje ya nchi chini ya kifungu Na. 280201. Kiasi hiki cha fedha kimeonyeshwa katika taarifa za fedha kama ruzuku. Gharama za matibabu zilizoelezwa hapo juu zimetumika ndani ya Jeshi lenyewe na sio ruzuku. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha unaotolewa taarifa, hapakuwa na ruzuku yoyote iliyotolewa na Jeshi kwenda katika taasisi nyingine. Kwa mazingira hayo, haikuwa sahihi kuonyesha matumizi hayo katika taarifa za fedha kama ruzuku. • **Mali za kudumu ambazo hazijahakikiwa Sh.**

www.JamiiForums.com

	2,266,596,621 Kati ya mali za kudumu zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha kama majengo, magari na kompyuta, mali zenye thamani ya Sh. 2,266,596,621 hazikukutwa zinakotakiwa kuwa wakati wa uhakiki. • **Makato ya mishahara kuwekwa katika akaunti ya Amana Sh. 734,092,928** Kias cha Sh. 734,092,928 kikiwa ni makato ya mishahara ya wanajeshi kutoka kwenye vifungu No. 210102 na 210101 vya matumizi ya kawaida ziliwekwa katika akaunti ya Amana ya Mkuu wa Majeshi. Hata hivyo, hapakuwa na nyaraka zozote kuhusiana na makato haya. • **Malipo zaidi kutoka katika Amana Sh. 465,655,201** Malipo zaidi ya mishahara ya Sh. 465,655,201 yaliwekwa katika Akaunti ya Amana ya Mkuu wa Majeshi. Hata hivyo, hakuna uthibitisho wowote unaoonyesha kuwa kiasi hicho cha fedha kililipwa Hazina kama inavyoagizwa na Waraka wa Hazina kupitia barua yenye Kumb. Na. EB/AG/5/03/01/Vol.VI/136 ya tarehe 31 Augosti, 2007 na barua Kumb. Na. CA: 307/334/01 ya tarehe 1 Januari, 2010. • **Makosa katika kutumia Takwimu za Kifedha za Serikali (GFS Codes)** Malipo ya kiasi cha Sh. 152,267,812 yalilipwa kutoka vifungu visivyohusika kinyume na Kanuni ya 87(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) na hivyo kufanya bajeti kutoonekana kama chombo cha kudhibiti wa matumizi.
12.	**Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa**
	• **Malipo zaidi ya posho ya chakula kwa mzabuni Sh. 85,075,000** • Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011, Jeshi la Kujenga Taifa lilifanya malipo ya Sh. 193,475,000 kwa

www.JamiiForums.com

	ajili ya posho ya chakula. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa Sh. 85,075,000 zililipwa zaidi kwa mzabuni kutokana na makosa katika ukokotoaji wa kiasi kilicholipwa kama Sh. 193,475,000 badala ya kiasi halisi kilichotakiwa kulipwa na Mkuu wa Kambi cha Sh.108,400,000 • Kulikuwa na madeni ya jumla ya Sh. 1,770,734,739.62 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011. Kuwepo kwa madeni haya ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu na yanaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 kwani sehemu yake inaweza kutumika kulipia madeni ya nyuma. • Mali za Kudumu zenye thamani ya Sh. 5,518,115,791 hazikuandikwa katika daftari la Mali za Kudumu
13.	**Fungu 41: Wizara ya Katiba na Masuala ya Sheria**
	Taarifa ya Mali, Mitambo na Vifaa imeonyesha kuwa katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2011, kulikuwa na manunuzi ya mali za kudumu yenye thamani ya Sh. 31,937,324.60 ambayo haikuweza kuhakikiwa katika daftari la mali kutokana na sababu zifuatazo: • Mali zilizonunuliwa zenye thamani ya Sh. 31,937,324.60 hazikuandikwa katika daftari la mali • Gharama za manunuzi, tarehe ya kununua na jina la mzabuni havikuonyeshwa katika daftari la mali la tarehe 28 Februari, 2011 • Jalada Kuu la Kumbukumbu za Mali (master inventory file) linalopaswa kuwepo kwa mujibu wa Kanuni ya 266 - 270 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) halikuwasilishwa ukaguzi lilipohitajika
14.	**Fungu 42: Ofisi ya Bunge**
	• Kiasi cha Sh 6,960,000 kama Posho ya kujikimu kwa Wabunge wakati wa vikao vya Bunge lakini hawakuwepo Dodoma na kiasi cha Sh 20,915,126 kililipwa kwa maafisa wa Bunge kinyume na kanuni za kudumu na miongozo ya utumiShi. • Masurufu ya Sh 65,803,144 yalikuwa hayajarejeShwa hadi mwisho wa mwaka kinyume na kanuni Na. 103 (1) na (7)

www.JamiiForums.com

	inayowataka watumishi kurejesha masurufu ya nyuma kabla ya kupewa mengine. Pia kanuni inataka masurufu kurejeshwa ndani ya siku 14 baada ya kurudi safarini au baada ya kukamilisha kazi iliyokusudiwa. • Malipo ya Sh.163, 195,130.34 hayakuwa na nyaraka muhimu kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebiShwa 2004). • Malipo ya Sh 94,000,000 yalilipwa kwa watumishi mbalimbali wa ofisi ya Bunge kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2011 kwa ajili ya kazi za ziada na poSho nyingine. Hata hivyo kiasi hiki kilionyeshwa kwenye hesabu za Bunge kama mali zisizogusika. Uainishaji huu sio sahihi na unaweza kupotosha watumiaji wa hesabu za Bunge. • Ukaguzi ulibaini jumla ya matumizi ya Sh.170, 858,030 ambayo hayakuwa na hati za malipo kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebiShwa 2004). • Menejimenti ilinunua mashine ya uchapiShaji kwa gharama ya Sh.370, 019,894 ambayo haifanyi kazi, na matokeo yake ofisi iliamua kukodi maShine nyingine kwa gharama ya Sh.190,480,496 kwa mwaka. • Kinyume na Kanuni Na. 265 (1)) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) menejimenti haiweki kumbukumbu sahihi kama vile rejista ya rasilimali za kudumu na hivyo kusababiSha matatizo yafuatayo: a) magari mawili yenye namba za usajili STK 8590 Toyota Land Cruiser hardtop na STK 3039 Toyota Land Cruiser hayakuingizwa kwenye rejista ya mali zakudumu, na hivyo kupunguza thamani ya mali za kudumu ilivyoripotiwa katika taarifa za fedha. b) Aidha, rejesta iliyopo haonyeshi taarifa/maelezo muhimu za mali kama vile namba zinazoonyeSha idadi ya mali, mwaka wa kutengenezwa, namba ya

www.jamiiforums.com

	chassier nk, na hivyo kuweka mipaka ya ukaguzi wetu wa mali za ofisi ya Bunge.
15	**Fungu 43: Wizara ya Kilimo na Chakula**
	• **Madeni na Mihadi yenye thamani ya Sh.5,528,060,215 ambazo hazijalipwa.** Taarifa ya fedha ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imeripoti Sh.5, 528,060,215 kama jumla ya madeni na mihadi ambayo yalikuwa hayajalipwa hadi tarehe 30 Juni, 2011. Hii ni kinyume na misingi fedha taslimu ya viwango vya kimataifa vya uhasibu wa sekta ya umma. Kiasi cha madeni na mihadi ambacho hakijalipwa kitaathiri bajeti na utendaji wa Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2011/2012. • **Kukosekana mchanganuo wa fedha za amana** Wizara inatunza amana za aina nne, yaani Amana Mkuu, Global Sasakawa, mishahara isiyodaiwa na mihadi (commitments). Kila amana inaonyeSha jumla ya fedha zilizopo mwiSho wa mwaka bila kuonyeSha orodha ya wenye amana hizo. Aidha, Wizara ina akaunti mbili za kukusanyia maduhuli, moja kwenye benki ya NMB tawi la Bank House na nyingine ipo Benki Kuu. Hata hivyo, Wizara inatunza kitabu kimoja tu cha fedha ambacho kinachanganya mapato yote yanayopokelewa na kupelekwa NMB au Benki Kuu. Kwa utaratibu huu, imekuwa vigumu kujua kiasi kamili cha salio la mwiSho lililotumika kutayarisha suluhiSho za benki. • **Kutoandaa Daftari la Mali za Kudumu** Taarifa za fedha za Wizara kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2011 zilionyeSha mali za kudumu zenye thamani ya Sh 26,474,547,881 ambapo mali za Sh 5,832,419,214 zilinunuliwa kipindi cha mwaka husika. Hata hvyo Wizara haikutengeneza rejista ya mali zakudumu na hakuna uhakiki wa mara kwa mara unaofanywa kutathmini mali zilizopo.

www.JamiiForums.com

	• **Kukosekana kwa uShahidi wa Upokeaji wa Mauzo ya Mbolea ya Minjingu Sh 4,050,079,400** Jumla ya Shs.4, 050,079,400 zililipwa kwa ''M / S Minjingu Mines Ltd and Fertilizer Ltd'' kama dhamana ya Serikali kwa ajili ya usambazaji wa mbolea ya Minjingu kwa wakulima wa Tanzania Bara wakati wa msimu wa kilimo wa 2009/2010. Hata hivyo hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa kiasi hicho cha fedha kimekusanywa toka kwa wahusika. • **Vocha za Ruzuku ya Pembejeo za Sh.4, 162,107,950 ZisizothibitiShwa.** Katika kipindi cha mwaka 2010/11, Wizara ilisambaza jumla vocha 3,063,653 za ruzuku ya pembejeo kwa ajili ya wakulima wa pamba yenye thamani ya Sh 8,473,514,000 kwa mikoa mbalimbali. Uchunguzi wa hati za malipo ulibaini kuwa, Wizara ilitoa jumla ya Shs.4,162,107,950 kwa Benki ya NMB kwa ajili ya ununuzi wa vocha hizo toka kwa wafanya biaShara. Hata hivyo, ukaguzi wa mfumo wa udhibiti wa ndani unaosimamia mchakato wa vocha za ruzuku ulibaini kuwa, Wizara haikuwa na ufahamu wa thamani ya vocha zilizoidhinishwa na kupitishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kwa ajili ya kununuliwa na Benki ya NMB. Kwa kuzingatia ukweli huu, ukaguzi haukuweza kubainisha mara moja kama kiasi cha Sh.4, 162,107,950 kiilitumika kwa ajili ya kunulia vocha halali za wakulima.
16	**Fungu 44: Wizara ya Viwanda na BiaShara**
	Matumizi Yasiyo na Manufaa Sh 10,881,863 Wizara kulilipa jumla ya Sh. 10,881,863 kwa M / s Toyota Tanzania kwa ajili ya matengenezo ya gari ya ofisi. Ushauri juu ya matengenezo ya gari ulitolewa na Kitengo cha Ukaguzi wa kiufundi kilichoko Hazina badala ya TEMESA kinyume na kanuni Na. 59 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma. Aidha, Wizara aliondoa gari hilo kutoka M / s Toyota Tanzania kabla ya matengenezoi kukamilika na kufanya malipo ya Sh

www.JamiiForums.com

	10, 881,863 kuonekana batili.
17	**Fungu 48: Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi**
	• Taarifa ya fedha kwa mwaka ulioishia tarehe Juni 30, 2011 inaonyeSha malimbikizo ya maduhuli ya Shs.275, 822,935. Hata hivyo, ukaguzi wa mchanganuo wa hesabu na kumbukumbu nyingine umebaini kuwa malimbikizo ya maduhulu ya kodi za ardhi toka vituo vya mikoani haikujumuishwa kwenye mchanganuo. Mchanganuo uliowasilishwa unaonyeSha wadaiwa wa Dar es salaam pekee. Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilihamisha kiasi cha ya Shs.42, 392,650 kutoka Mfuko wa amana(retention scheme) A/C kwenda akaunti ya Maendeleo Na 3111200003 kwa ajili mwenge wa uhuru na ununuzi wa matairi. Hata hivyo, fedha hizi hazikutengwa kwa ajili ya shughuli hizo na hivyo kufanya matumizi hayo kuwa batili.
18	**Fungu 49: Wizara ya Maji**
	• Kiasi cha Sh 374, 242,863 sawa na asilimia 18% kilitozwa kama kodi ya ongezeko la thamani kwa malipo ya jumla ya Sh 2,064,943,337 yaliyofanywa na Wizara kupitia fedha za wafadhili kinyume na mwongozo wa Benki ya Dunia wa Mei, 2006. • Wizara ilishindwa kudai fidia ya dola za kimarekani 368,707.11 sawa na Sh 588,456,548 kutoka kwa wazabuni walioShindwa kutimiza majukumu yao kulingana na mikataba.
19	**Fungu 51: Wizara ya Mambo ya Ndani**
	• Maeneo ya mapato na manunuzi ya hayakushughulikiwa na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika mwaka wa fedha unaoShia tarehe 30 Juni 2011i. Hii inafanya wigo wa kazi za kitengo kuwa mdogo. • Malimbikizo ya maduhuli ya jumla ya Sh 122,715,961.45 yalikuwa hayajakusanywa mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2011

www.JamiiForums.com

	• Hakukuwa na maelezo juu ya tofauti kati ya bajeti na kiasi halisi cha Mapato yasiyo ya Kodi, mishahara , manunuzi ya mali zisizogusika (Intangible assets) na manunuzi ya mali za muda mfupi. • Hakukuwa na maelezo ya tofauti kati ya bajeti ya awali na bajeti ya mwiSho kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi, vifaa ofisi, ruzuku, na ununuzi wa mali za kudumu. Hata hivyo bakaa hizo haikuonyeShwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vya uhasibu wa sekta ya umma kwa fedha taslimu ambavyo vinataka bakaa zenye masharti kutolewa maelezo. Menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Ndani haina sera za usalama wa mifumo yake ya teknolojia
20	**Fungu 52: Wizara ya Afya na Ustawi wajamii**
	• Taarifa ya mtiririko wa fedha ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2011 ilionyeSha bakaa yafedha ya Sh 733,658,627 kwa ajili ya kurudishwa hazina na Sh 4,009,381 kwa ajili ya akaunti maalum (Holding account). Hata hivyo bakaa hizo hazikuonyeshwa kwenye vitabu kulingana na viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekata ya umma vinavyotaka bakaa zenye maSharti kuonyeShwa kama maelezo kwenye taarifa za hesabu. • Kiasi cha Sh 3,240,076,891 kilihamishwa kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya amana kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Hata hivyo hakuna kabili kilichoombwa kutoka hazina kwa ajili ya kuhamiSha fedha hizo. • Jumla ya Sh 55,308,775 zimekaa kwenye akaunti ya amana tangu mwaka wafedha 2007/2008 hadi 2010/2011 chini ya idara ya ustawi wajamii bila kutumika na hakuna maelezo yanayoonyeSha kuwa hizo ni kwa ajili ya kazi zipi. • Taarifa ya upotevu wa fedha fedha, vifaa na madai yaliyotelekezwa ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2011 ilionyeSha matumizi ya Sh 31,900,906 ambayo

www.JamiiForums.com

	yalilipwa bila kuwa na manufaa kwa serikali. • Kwa kipindi kinachoiShia tarehe 30 Juni 2011 Wizara ilikuwa na deni la Sh 1,342,000,000 ambalo halijathibitiShwa kutokana na kesi mbalimbali. Hata hivyo ukaguzi zaidi uligundua kuwa deni hilo linatokana na wafanyakazi walioaShiShwa kazi kinyume na sheria na uzembe wa kimatibabu. • Wizara ilitumia kiasi cha Sh 73,956,552 kutoka kwenye vifungu visivyohusika na kuaShiria mapungufu ya udhibiti wa bajeti • Hati za malipo za Sh 77,332,806 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kinyume na kanuni Na 86 ya kanuni za fedha za umma za mwaka 2011 • Ukaguzi wa mishahara kwa mwezi wa Juni 2011 ulibaini kuwa Wizara ililipa kiasi cha Sh 49,501,628 zililipwa kwa afisa mbalimbali ambao wameShapitiSha umri wa kustaafu kinyume na kanuni za kudumu. • Taarifa za fedha kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2011 zilionyesha madeni ambayo hayajalipwa ya Sh 44,016,818,552 kinyume na maagizo ya Serikali yaliyotolewa na Mlipaji Mkuu kupitia barua yenye Kum Na C/BA.54/534/01/02 ya tarehe 02/12/2008 ambayo iliagiza taasisi za serikali kuepuka madeni kwa kufanya matumizi kulingana na fedha zilizopo.
21	**Fungu 53: Wazara ya Maedeleo ya Jamii Jinsia na Watoto**
	• **Madeni yasiyolipwa** Wizara imeripoti madeni ya Sh 2,034,032,772. Kwa kuwa serikali inatumia mfumo wa bajeti ya fedha taslimu, kuwa na madeni mwisho wa mwaka kunasababisha mzigogo kwa serikali kulipa madeni haya ambayo ambayo ni wazi kuwa yataathiri bajeti ya mwaka unaofuata. Hii pia ni ushahidi kuwa mfumo funganifu wa fedha imeShindwa kuzuia madeni haya

www.JamiiForums.com

	yasitokee. • **Shughuli zilizofadhiliwa na mfuko wa umaja wa mataifa wa kuhudumia watoto (UNICEF) ambazo hazikufanyika Sh 14,175,000** Wizara imeshindwa kutekeleza shughuli kulingana na sera za mfuko wa umoja wa mataifa wa kuhudumia watoto . kulingana na sera hizo, shughuli zilizopangwa zisipotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu, fedha zilizotengwa inapaswa zirudiShwe .
22	**Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**
	• **Madeni na mihadi isiyolipwa Sh 157,822,999** Taarifa za fedha za tume ya haki za binadamu na utawala bora kwa mwaka unaoiShia tarehe 30 juni 2011 zilionyeSha madeni na mihadi ya Sh 157,822,999 ambayo yalikuwa hayajalipwa. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao kwa sehemu ya bajeti itatumika kulipa madeni hayo. • **Utengenezaji wa magari kwenye gereji binafsi Sh 16,110,643** Kiasi cha Sh 16,110,643 kilitumika kutengeneza magari kwenye gereji za watu binafsi lakini hakuna ushahidi unaoonyeSha kuwa magari hayo yalikaguliwa na Wakala wa Umeme na Mitambo (TEMESA) kabla na baada ya matengenezo
23	**Fungu 56: Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.**
	• **Madeni yasiyolipwa Sh 147,821,065** Wizara ilikuwa na madeni ya Sh 147,821,065 wakati wa kufunga mwaka wa fedha. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shuguli zilizopangwa kwa kuwa sehemu ya bajeti itatumika kulipia madeni. • **Kiasi kilichokopwa toka akaunti ya amana ambacho**

www.JamiiForums.com

	hakijarudiShwa Sh 47,779,380 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMESA) ililipa kiasi cha Sh 47,779,380 kama mkopo kutoka akaunti ya amana kwa ajili ya kugharimia shughuli za idara mbalimbali. Hata hivyo mpaka tunaandika ripoti hii, kiasi hicho bado kilikuwa hakijarudiShwa
24	**Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**
	• Ukaguzi haukuweza kuhakiki mali za kudumu zenye thamani ya Sh 53,063,606,780. kutokana na kukosekana kwa rejista yenye kumbu kumbu sahihi. • Wizara ilikuwa na mihadi ya Sh 641,414,979,664 wakati wa kufunga mwaka wa fedha. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kuwa bajeti iliyopo itatumika kulipia madeni
25	**Fungu 58: Wizara ya Nishati na Madini**
	• **Maduhuli yaliyokusanywa na kubakizwa na Shirika la maendeleo ya petroli (TPDC) Sh 9,733,796,202** Uhakiki uliofanywa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2011 ulibaini kuwa maduhuli ya Sh 9,733,796,202 yalibakizwa na Shirika la maendeleo ya petroli bila kibali. • **Matumizi yasiyoingizwa kwenye vitabu vya wizara Sh 88,000,000** Katibu mkuu kupitia barua yeke yenye kumbukumbu Na. CAB.56/88/01 ya tarehe 23Juni, 2011 aliziandikia taasisi nne zilizoko chini ya wizara kuwataka watendaji wakuu wa taasisi hizo kuchangia gharama za kuendeSha semina ya wabunge iliyokuwa ifanike mjini Dodoma mwezi Juni 2011. hata hivyo niligundua kuwa kiasi hicho cha Sh 88 milioni hakikujumuiShwa kwenye matumizi ya wizara na hakuna maelezo yaliyotolewa kwenye taarifa za fedha. • **UhamiSho wa Sh 171,542,000 kwenda GST kwa ajili ya**

www.JamiiForums.com

	mchakato wa bajeti Kiasi cha Sh 171,542,000 zilihamishwa kwenda benki ya NMB kupitia akaunti Na 5051000068 inayomilikiwa na Taasisi ya utafiti wa madini (GST) Dodoma kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa robo ya nne ya mwaka 2010/2011. hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa fedha hizo zilitumika kenye maandalizi ya hotuba ya bajeti ya Wizara tofauti na maelezo yaliyopo kwenye hati za malipo. • **Malipo bahili toka kwenye akaunti ya maendeleo Sh 43,602,941** Ukaguzi wa hati za malipo ulibaini kiasi cha Sh 43,602,941 zilizolipwa toka akaunti ya maendeleo kulipia matumizi ya kawaida. Hii ina maana kuwa miradi ya maendeleo iliyopangwa kufanyika kwa kutumia kiasi hicho cha fedha iliahirishwa. • **Utendaji wa Wizara chini ya Malengo** Uhakiki wa utekelezaji wa shughuli za kawaida za Wizara uligundua kuwa baadhi ya Shughuli zilifanyika chini ya malengo kati ya asilimia 0 na 47. hata hivyo hakuna sababu za kuridhiSha zilizotolewa kuhusiana na utendaji huo wa chini. Hii inaashiria kwamba baadhi ya Shughuli zilizopangwa kufanyika kwa kipindi hicho hazikutekelezwa ipasavyo na zinaweza kuathiri bajeti ya mwaka ujao kutokana na kupanda kwa gharama. • **UhamiSho wa fedha usioidhinishwa Sh 162,000,000** Katika mwaka huu wa fedha, kiasi cha Sh 162,000,000 kilihamishwa toka akaunti Na. 505100068 inayoendeshwa na taasisi ya kutafiti madini (GST) Dodoma. Fedha hizi zilikusudiwa kulipia shughuli za maendeleo lakini zilitumika kugharimia shughuli za kawaida bila idhini yoyote. • **Malimbikizo ya maduhuli ambayo hayakuonyeshwa Sh 503,412,421.40**

www.JamiiForums.com

	Ukaguzi wa taarifa za fedha na michanganuo yake umebaini kuwa malimbikizo ya Sh 503,412,421 toka mwaka yatokanayo na mirahaba hayakuonyeshwa kwenye vitabu vya wizara kwa mwaka huu wa fedha kinyume na sehemu X ya kanuni za fedha za umma za mwaka 2004 Tozo za kiSheria z akesi zilizotolewa hukumu na mahakama hazikuonyeshwa kwenye taarifa za hesabu Sh 215,552,764 Wizara ilipewa hati ya madai ya Sh.2115,552,764 kama tozo la kisheria kutokana na maamuzi ya mahaka kwenye kesi dhidi ya IPTL. Kutokana na maamuzi haya ya mahakama wazara ililipa Sh 1,900,000,000 kama sehemu ya madai hayo kupitia akaunti ya maendeleo lakini suala hili lilipelekwa kwenye Baraza. Hata hivyo ilibainika kuwa kiasi kilichobaki cha Sh 215,552,764 hakikuonyeshwa kwenye taarifa ze fedha kama deni linalosubiri hukumu ya baraza ambayo ilipangwa kutajwa mwezi April 2011. mpaka tunaandaa taarifa hii mwezi Desemba 2011 hukumu ya Baraza bado ilikuwa haijajulikana.
26	**Fungu 59: Tume ya kurekebisha Sheria**
	Matumizi ya fedha za mradi wa BEST kwa shughuli amabazo hazikuwa kwenye mipango Sh.10,898,400 • Fedha za Maendeleo za Mradi wa BEST zilitumika kulipia posho za vikao kwa washiriki wa warsha ya uandishi wa taarifa ya mwaka pamoja na mipango kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2011 kama sehemu ya matumizi ya kawaida. Uongozi wa Tume uliahidi kuzirudisha fedha hizo kwenye akaunti ya maendeleo, lakini mpaka kufikia tarehe 14 Disemba fedha hizo hazikuwa zimerejeshwa kwenye akaunti husika. • Matumizi ya Sh.101,516,410 yalilipwa kutoka kwenye vifungu visivyohusika.

www.JamiiForums.com

27	**Fungu 60: Mahakama ya Kazi**
	Malipo yasiyo na nyaraka kamili kiasi cha Sh.44,019,728 • Malipo ya kiasi cha Sh.44,019,728 yalifanyika bila ya kuwa na nyaraka kamili, hivyo hatukuweza kujiridhisha kama yalikuwa ni malipo halali. **Madeni mwishoni mwa mwaka kiasi cha Sh.142,464,390** • Mahakama ya Kazi ilikuwa na madeni ya kiasi cha Sh. 142,464,390. Madeni haya yanaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti na shughuli za mwaka ujao, ikiwa fedha za mwaka huo zitatumika kuyalipa.
28	**Fungu 61: Tume ya Taifa ya Uchaguzi**
	• **Madeni yasiyolipwa Sh. 2,485,155,129** Tume ilikuwa na madeni ya Sh. 2,905,761,848 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011, ambapo malipo ya mikataba yalikuwa ni Sh. 2,485,155,129 sawa na 85.5%. Hata hivyo kiasi kilicholipwa na kilichobakia havikuwekwa bayana. • **Matumizi yasiyo na nyaraka kamili Sh. 427,906,854** Malipo ya Sh. 427,906,854 yalifanyika yakiwa na nyaraka pungufu hivyo kukiuka kanuni za 86(1) na 95(4) za Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001(zilizorekebishwa 2004) Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Tume iliingia mikataba na wazabuni yenye thamani ya Sh. 787,271,963 kwa ajili ya kupatiwa huduma na bidhaa mbalimbali. Hata hivyo mikataba husika haikutolewa ili ikaguliwe. • **Mali za Kudumu zisizo na Mchanganuo**

www.JamiiForums.com

	Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Tume ilionesha katika vitabu vyake vya hesabu mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 787,271,963 zikiwemo zilizonunuliwa mwaka huo zenye thamani ya Sh. 705,007,254. Hata hivyo, jedwali la mali za kudumu zilizonunuliwa halikutolewa. Vilevile daftari la mali za kudumu la Tume halioneshi mali zote za kudumu zinazomilikiwa na Tume. **Vithibisho vya kupokelewa fedha na michanganuo ya matumizi yake havikutolewa Sh. 35,642,419,966** Tume iliwapatia Wakurugenzi wa Maendeleo wa Halmashauri za Wilaya mbalimbali jumla ya Sh. 35,642,419,966 kupitia benki ya NMB, kwa ajili ya uchaguzi mkuu. Lakini vithibitisho vya kupokelewa fedha na michanganuo ya matumizi yake havikutolewa ili vihakikiwe, hivyo kukiukwa kanuni za 86 (1), 87 na 95(4) za Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (kama zilivyorekebishwa 2004).
29	**Fungu 64: Mahakama ya Biashara**
	Mahakama ya Biashara ilitoza kwa upungufu wa Sh. 1,393,036 ada ya mahakama hivyo kukiuka Sura ya 358 ya Sheria ya Mahakama ya Biashara (Ada) (marekebisho) kanuni, 2005 kifungu cha 2(a) na (b). Ikiwa hali ipo hivi, hili linaweza kuwa na athari kubwa kwa mapato ya Serikali kwa ujumla wake. **Madeni na Mihadi** Mahakama ya Biashara ilikuwa na madeni ya Sh. 11,592,346 na mihadi ya Sh. 427,405,790 na jumla ya hayo yote ni Sh. 438,998,136 mnamo tarehe 30 Juni 2011. Madai haya yanaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti na shughuli za mwaka ujao, ikiwa fedha za mwaka huo zitatumika kuyalipa.
30	**Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira**

www.JamiiForums.com

	Kwa mwaka tulioukagua, jumla ya Sh.6 15,775,222.65 ziliripotiwa kama madeni yasiyolipwa ya muda kati ya siku 30 na zaidi ya miezi 6. Kiasi hiki ni asilimia 7% ya cha mwaka uliopita. Hii inaweza kuathiri shughuli zilizopangwa kama bajeti kwa kiasi inaweza kutumika kwa ajili ya kulipa madeni hayo. Ukaguzi wa uendeshaji wa Mfuko wa Mikopo ya Maendeleo ya Vijana chini ya Wizara ulibaini madeni ya muda mrefu kati ya siku 30 hadi miaka 5 kwa kipindi kilichoishia Juni 30, 2011. • Madeni yanayodaiwa ya thamani ya Sh. 1,683,906,606.91 ikiwa ni kiasi kilichotolewa na riba yake. Fedha hizi zilitolewa kwa halmashauri mbalimbali za wilaya na SACCOS kote nchini kama mfuko wa mikopo inayozunguka. Ucheleweshaji wa marejesho ya mikopo hii inazuia utoaji wa mikopo zaidi kwa makundi mengine ya vijana na SACCOS. Wakati wa Ukaguzi, ilibainika kuwa Wizara haikuwa na daftari la kuorodhesha mali za kudumu. Kutokana na kukosekana kwa daftari la mali, ni vigumu kufuatilia utumiaji na mizunguko ya mali hizo kama ununuzi, ugawaji, uuzaji kuachana na mali husika n.k, na hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya mali bila utawala kujua.
31	**Vote 66: Ofisi ya Rais Tume ya Mipango**
	Tume ilikuwa na fedha ambazo hazikudaiwa jumla ya Sh.140,235,227 ambazo ziliwekwa kwenye Akaunti ya Amana toka mwaka wa fedha 2006/2007 bila ya kuhamishiwa Mfuko Mkuu wa Serikali, kama inavyotakiwa na Kanuni ya 133 ya Kanuni za Fedha za Serikali za 2001 (marekebisho 2004).
32	**Fungu 67: Sekretariati ya Ajira**

www.JamiiForums.com

	Kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2011 Ofisi ya Raisi Sekretariati ya Ajira ilikuwa na mihadi isiyolipwa ya kiasi cha Sh. 253,058,267. Fedha hizi zilihamishiwa kwenye akaunti ya amana ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, maelezo ya ankara au bili zilizosababisha fedha hizo zitengwe hazikuwasilishwa ukaguzi. . Sekretarieti iliwalipa maofisa wake kiasi cha Sh. 7,509,600 kama posho ya kujikimu kwa siku 13 waliposafiri kwenda Israeli katika ziara ya mafunzo. Matumizi haya hayakuzingatia kuwa washiriki wote walikuwa wamelipiwa kila kitu ikiwemo malazi, hivyo kuyafanya kuwa malipo mara mbili. **Matumizi yalilipiwa chini ya vifungu visivyohusika Sh. 7,486,000** Matumizi ya vifaa na bidhaa jumla ya Sh. 7,486,000 yalilipiwa chini ya vifungu visivyohusika. Hii ina maana kuwa kuna udhaifu katika udhibiti wa bajeti.
33	**Fungu 69: Wizara ya Maliasili na Utalii**
	• Waongozaji na mawakala wa utalii hawakuwa wamelipa ada wala kusajiliwa, na hivyo kukiuka kanuni ya 6 ya shughuli za utalii (ada na tozo). Kutokana na hayo, mapato ya jumla ya Dola za Kimarekani 147,300 sawa na Sh. 249,673,500 kushindwa kukusanywa wakati wa mwaka husika. • Watu ambao ajira zao zimekoma kwa sababu mbalimbali kama kuacha kazi, kifo au au kutoroka walilipwa jumla ya Sh.18,911,031 kama mishahara hii ikiashiria kuwepo kwa udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani juu ya mishahara. • Wizara ilikuwa imelipa zaidi kiasi cha Sh.

www.JamiiForums.com

	18,442,393.66 kutoka akaunti yake ya LMDA-inayohusu Misitu ya Uoto ya Buhindi. Hata hivyo, akaunti hii haikufanyiwa usuluhishi na daftari linalotunza kumbumkumbu za kasma husika lililokuwa na bakaa ya Sh. 21,776,180.34 hivyo kuleta tofauti ya Sh. 3,333,786.68 isiyo na maelezo. • Wizara ililipa kiasi cha Sh. 10,928,351.88 kwa ajili ya huduma za mtandao kwa ajili ya mfanyakazi wake bila ya kibali kutoka kwa mamlaka husika. • Tulibaini kuwa kiasi cha Sh. 11,000,000 kililipwa kutoka Chuo cha Wanyapori cha Pasiansi kwenda katika ofisi ya kanda ya kuzuia ujangiri bila ya kibali cha Afisa Masuuli. • Kiasi cha Sh. 12,000,000 kilichotolewa kwenda Chuo cha Wanyapori cha Pasiansi hakikuwa kimekifikia chuo hicho hadi wakati tunamaliza ukaguzi. • Wakati wa ukaguzi tulibaini kuwa, matumizi ya fedha kwa ajili ya mafuta yenye thamani ya Sh. 37,124,900 yalilipwa chini ya kifungu cha 410408 (generator) badala ya kifungu 220302 (dizeli). Kwa maana hiyo thamani ya mali halisi za wizara imezidishwa kimakosa. • Kitengo cha Uangalizi wa Misitu Kanda ya Ziwa (Mwanza) kilikusanya Sh. 44,308,060 kama mapato ya mauzo ya bidhaa za misitu zilizokamatwa katika Kituo cha Kaniha. Hata hivyo makusanyo yote yaliwekwa katika akaunti ya wizara Na. 2061100044 badala ya Akaunti ya Taifa ya Misitu. Si marejesho ya fedha husika wala maelezo vilivyotolewa na uongozi kwa suala hili.
34	**Fungu 90: Mahakama ya Ardhi**
	Madeni yasiyolipwa Sh. 24,790,590 Taarifa za Mahakama ya Ardhi zilionesha jumla ya Sh.

www.JamiiForums.com

	24,790,590 kama madeni yasiyolipwa. Katika hali hii, kuna uwezekano fedha za 2011/2012 zikatumika kulipia madeni ya mwaka 2010/2011 hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka husika. **Malipo yenye nyaraka pungufu** Matumizi ya thamani ya Sh. 11,401,856 yalifanyika bila ya nyaraka kamili kinyume na Kanuni Na. 86 (1) na 95 (4) za Kanuni za Fedha za Umma. Hali hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma, na inaashiria kuwa malipo hayachunguzwi vya kutosha kabla ya kuidhinishwa.
35	**Fungu 91: Tume ya Udhibiti wa Madawa**
	• **Kiasi kilichotolewa zaidi ya kilichoidhinishwa Sh. 11,777,090** Kamishna wa Bajeti aliipatia Tume fedha zaidi ya zile zilizoidhinishwa na bunge, bila maelezo yoyote kuhalalisha jambo hilo. • **Ukaguzi wa miradi iliyo chini ya Tume ya Udhibiti wa Madawa** ➢ **Mali za kudumu zisizokuwemo daftarini zenye thamani ya Dola za Kimarekani 72,324.86** Mali zenye thamani ya Dola za kimarekani 72,324.86 hazikuingizwa kwenye daftari la mali za kudumu. Mali hizi zinaweza kutumika isivyo halali au kupotea bila taarifa. ➢ **Mali isiyo idhinishwa yenye thamani ya Dola za Kimarekani 138,835** Upitiaji wa taarifa ya utendaji ulibaini kuwa kiasi cha Dola za Kimarekani 138,835 kilitumika bila ya kuwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa.
36	**Fungu 93: Idara ya Uhamiaji**

www.JamiiForums.com

- Masuala ya miaka iliopita yaliyohusiana na tuhuma za wizi wa mapato jumla ya Sh. 83,344,000 na Dola za Kimarekani 75,580 ambayo yanasubiri hukumu ya mahakama hayajapatiwa ufumbuzi.

Madeni

- Taarifa za kifedha zilizowasilishwa kwa ukaguzi kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2011 ilionesha kuwa, Idara ya Uhamiaji ilikuwa na madeni ya kiasi cha Sh. 154,712,448.70. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao uliopangwa kama bajeti yake inaweza kutumika kwa ajili ya kulipa madeni hayo.

- Uongozi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa ya Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro haukuwasilisha nyaraka mbalimbali kama hati za malipo, stakabadhi za mapato, na ERVs zilizotumika kukusanya mapato kutokana na ada ya pasipoti, vibali vya makazi, CTA na ETD kama muhtasari hapa chini unavyoonesha:

Namba	Kutoka	Mpaka
1.	33320601	33320800
2.	36538801	36539000
3.	36558201	36558400
4.	41528001	41528200
5.	41528201	41528400
6.	41528401	41528600
7.	41552401	41552600
8.	42638001	42638200

- Kiasi cha Sh. 2,527,647,932.95 kiliingizwa vitabuni kwa ajili ya kazi za ujenzi zilizokuwa zinaedelea katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ujenzi wa makao Makuu ya Uhamiaji na ukarabati wa ofisi za mikoa ya Rukwa na Mbeya. Kiasi hicho cha mwaka

www.jamiiforums.com

	uliopita kilitarajiwa kuja kulipwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 hivyo kilipaswa kuoneshwa vitabuni kama mihadi lakini hakikuoneshwa hivyo. Aidha, uthibitisho wa kukamilika miradi hii mitatu haukutolewa na uongozi. • Uongozi haukuwasilisha nyaraka za Sh. 64,360,099 zilizokosekana kwenye hifadhi za hati za malipo.
37	**Fungu 96: Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo**
	• Wizara ilikuwa inadaiwa Sh. 3,615,777,165 na wazabuni mbalimbali, wauzaji wa bidhaa, watoa huduma na madai ya wafanyakazi. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao kama bajeti kwa kiasi hicho inaweza kutumika kulipia madeni haya. • **Mapato yatokanayo na mashine ya kutengenezea filamu hayakuainishwa ipasavyo Sh.129,028,644.88** Mfumo wa kihasibu na udhibiti wa mapato yatokanayo na mitambo ya filamu ni dhaifu. Kwani kwa mwaka tulioukagua Sh. 129,028,644.88 zilizopatikana hazikuchambuliwa na kuainishwa ipasavyo, kwa maana ya maombi na vibali vilivyotolewa havikuwianishwa kwa ajili ya uthibitisho na udhibiti. • Malipo yalifanyika yalikuwa na nyaraka pungufu kwa kiasi cha Sh. 28,442,500 kinyume na kanuni ya 95(4) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (marekebisho 2004). Usahihi wa malipo hayo kama matumizi halali ya Serikali haukupatikana. • Kutokana na ufinyu wa bajeti ujenzi wa nyumba ya utamaduni haukukamilika. Ujenzi huu unasuasua kwa takribani mwaka wa nne sasa. Wizara iwasiliane na Hazina na kutafuta wafadhili ili kukamilisha ujenzi huu.

www.JamiiForums.com

38	Fungu 98: Wizara ya Ujenzi
	• **Vifaa vya bohari visivyo na uthibitisho wa kuhesabiwa Sh. 129,613,885** Vifaa vya bohari vyenye thamani ya Sh. 129,613,885 havikuwa na uthibitisho kuwa vilihesabiwa kama Kanuni Na. 237(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (marekebisho ya 2004) zinavyotaka. • **Malipo nje ya kasma yalioneshwa kwenye taarifa ya upokeaji na ulipaji wa fedha taslimu kama mali zisizo za kudumu Sh. 283,882,893,368** Malipo nje ya kasma Sh. 283,882,893,368 yaliingizwa kwenye taarifa ya upokeaji na ulipaji wa fedha taslimu chini ya akaunti ya maendeleo isivyo sahihi kama ununuzi wa mali zisizo za kudumu. • **Madeni yasiyolipwa Sh.422,299,119,935** Taarifa ya kifedha ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 ilionesha madeni ya Sh. 422,299,119,935. Ilikuja kubainika kuwa mwezi Aprili, 2011 Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ililipa Sh. 23,986,126,405 moja kwa moja kwenye akaunti ya makandarasi kwa kutoa fedha kutoka akaunti ya Madeni ya Miundombinu Na.9924193421. Hata hivyo, Uongozi wa TANROADS badala ya kukipunguza kiasi hiki kutoka kwenye madeni yake ukakiacha hivyo kusabisha madeni kuzidishwa isivyo sahihi kwa Sh. 23,986,126,405. • **Kukosekana mkataba uliosainiwa kati ya wizara na wakala za Serikali zilizo chini yake kwa mwaka 2010/2011** Kwa majibu Kifungu cha 3 (2) (a) (d) cha Sheria ya Wakala wa Serikali ya Mwaka 1997, wizara inapaswa kusaini makubaliano ya utendaji na wakala husika kila tarehe 1 Julai. Hata hivyo wizara haikusaini

www.JamiiForums.com

	makubaliano ya utendaji na wakala wake ambao ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Wakala wa Ufundi, Umeme na Mitambo Tanzania (TEMESA), wakati makubaliano na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) yalisainiwa tarehe 26 Septemba 2011. kwa muktandha huo hatukuweza kujiridhisha uhalali wa taarifa za utendaji na matumizi ya wakala hao kama yalivyooneshwa vitabuni yakiwa na jumla ya Sh. 480,240,556,608.
39	**Fungu 90:Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi**
	• **Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani hayakudaiwa kutoka TRA** Kiasi cha Sh. 34,372,479 kililipwa kimakosa TRA ili kutolea mizigo ya mradi wa OFCF kutoka Japani ambayo ina msamaha wa kodi. • **Fedha zilizotangulizwa Hazina dogo sisizo na uhalalisho wa matumizi** Jumla ya Sh. 962,458,209 zilitangulizwa hazina ndogo kwa manunuzi ya mali za kudumu mikoani. Michanganuo na vielelezo vya matumizi havikutolewa kuhalalisha matumizi hayo. • **Mali za kudumu zenye thamani ya Sh.1,851,679,002 hazikuwa na chapa ya utambulisho** Mali za kudumu zenye thamani ya Sh.1,851,679,002 zilizonunuliwa mwaka husika hazikupigwa chapa ya utambulisho.
40	**Fungu 70: Sekretariati ya Mkoa wa Arusha**
	• Kamati ya Ukarabati wa Hospitali ya Mount Meru iliingia mkataba na kampuni ya Mazishi ya Arusha ili kukusanya ada ya chumba cha kuhifadhia maiti, tangu tarehe 31 Septemba 2011. Kuanzia kipindi hicho hadi tarehe 30 Juni 2011 hukuna fedha zozote zilizopokelewa kutoka kwa wakala huyo ambazo

www.JamiiForums.com

	zilipaswa kuwa Sh. 118,800,000. Aidha, taarifa za fedha hazikuonesha fedha hizo kama madeni. Hazina ilitoa jumla ya Sh. 675,516,000 kwa kupitia Sekeretariati ya Mkoa kwa ajili ya halmashauri za wilaya sita (6) na Manispaa moja (1). Lakini vithibitisho kuwa fedha hizo zilizifikia halmashauri husika havikutolewa mpaka tunamaliza ukaguzi (Disemba 2011). Sekretariati ilikuwa na madeni ya Sh. 356,211,696.41 mwishoni mwa mwaka. Madeni haya yanaweza kuathiri bajeti ya mwakani ikiwa fedha zake zitatumika kuyalipa.
41	**Fungu 71: Sekretariati ya Mkoa wa Pwani**
	Uongozi wa Sekretariati ya Mkoa wa Pwani hauna daftari la orodha ya mali za kudumu kinyume na Kanuni ya 264(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka, 2001 (zilizorekebishwa 2004).
42	**Fungu 72: Sekretariati ya Mkoa wa Dodoma**
	• Sekretariati ya Mkoa wa Dodoma iliungua moto Agosti 29, 2010 ambapo nyaraka na mali nyingine eneo A la Jengo la Mkoa ziliharibiwa. Juhudi zilifanywa kupata nyaraka kutoka kwenye mfumo wa IFMS na Hazina. Hata hivyo, hati za malipo za Sh. 104,711,330 hazikupatikana na kutolewa kwa ajili ya uhakiki. • Wakati wa mwaka tunaoukagua Sekretarieti ilipanga kutekeleza miradi mbalimbali. Hata hivyo, uhakiki wa mapitio ya utendaji wa kila mwaka wa kazi halisi na taarifa za fedha za miradi ulibainisha kuwa baadhi ya shughuli chini ya miradi hiyo hazikutekelezwa kutokana na kutotolewa fedha.

www.JamiiForums.com

	• Hasara iliyoelezwa kuwa imetokana na moto kiasi cha Sh. 5,030,455,379 haikuwa na mchanganuo.
43	**Fungu 73: Sekretariati ya Mkoa wa Iringa**
	• Fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) zilizotengwa kwa ajili ya RAS Iringa na Halmashauri kiasi cha Sh. 182,830,000 na Sh. 961,785,000 sawia kwa ajili ya mwezi Agosti 2010 hazikutolewa ufafanuzi wa matumizi yake na kuoneshwa vitabuni kama ilivyoagizwa na Hazina. • Taarifa ya fedha zilionesha madeni yasiyolipwa ya Sh. 246,032,885.72. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao na mipango yake ikiwa bajeti kwa kiasi inaweza kutumika kwa ajili ya kulipa madeni hayo. • Sekretarieti iliingia mikataba na M / S Pacha Kampuni ya Ujenzi ya Morogoro, na M / S Sepro Limited ya Dar es Salaam kwa ajili ya awamu ya III ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Iringa kwa mkataba wa Sh. 380,282,502 na Ukumbi wa Mikutano wa Mkuu wa Mkoa Iringa awamu ya I kwa mkataba wa Sh. 348,166,605.06. Miradi yote ilikuwa inatarajiwa kukamilika tarehe 30/6/2011, hata hivyo hadi wakati wa ukaguzi miradi hii haikuwa imekamilika.
44	**Fungu 75: Sekretariati ya Mkoa wa Kilimanjaro**
	• **Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari Sh. 3,069,200** Ukaguzi wa vifaa vya ghalani umebaini kuwa vifaa vyenye thamani ya Sh.3, 069,200 vilivyoagizwa na kulipiwa kwa mwaka uliomalizika havikuingizwa kwenye daftari la vifaa vya ghalani na mchaganuo wa matumizi yake haukuweza kupatikana. Hii ni

www.JamiiForums.com

	kinyume na Kanuni za 191 na 192 za Kanuni za Fedha za Umma, 2001. • **Makato yanayozidi kikomo Sh. 2,503,033.85** Ukaguzi wa baadhi tu ya taarifa za mishahara kwa mwezi Juni, 2011 umebaini kuwa makato kutoka kwenye mishahara yanazidi kikomo cha theluthi (1/3) ya mshahara kilichowekwa na PO-PSM kwa barua yenye kumb. Na. C/CE.45/271/01/1/87 ya 19/3/2009 na Sheria ya Mikopo Namba 7 ya mwaka 1970.
45	**Fungu 76: Sekretariati ya Mkoa wa Lindi**
	• Sekretariati ya Mkoa wa Lindi ilikuwa na miradi ya Sh. 720,505,798 ambayo haijakamilika hadi wakati wa ukaguzi, yaani Disemba, 2011. Kipindi cha mikataba kwa miradi yote 15 kilikuwa kimekwisha. • Sekretarieti ya Mkoa inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi na maarifa kwa ajili ya kuendesha mfumo wa Epicor. • Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kina mkaguzi mmoja tu (1) badala ya watatu kwa mujibu wa ikama.
46	**Fungu 77: Sekretariati ya Mkoa wa Mara**
	• Ukaguzi wa kumbukumbu za taarifa za wafanyakazi na taarifa kuu ya mishahara kutoka hazina kwa kipindi kilichoishia 30/6/2011 ulibaini kuwa tarehe za kuzaliwa kwa wafanyakazi 85 zilikosewa. Hali hii ina maana kuwa tarehe ya kustaafu kwa wafanyakazi hawa haiwezi kufuatiliwa kwa urahisi. Sekretarieti inapaswa kushirikiana na Hazina ili kuondoa tatizo hilo. • Jumla ya Sh. 1,400,379,000 zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Sekretarieti hazikutolewa na Hazina. Kukosekana kwa fedha hizo kuliifanya Sekretarieti kushindwa kutekeleza shughuli zilizokusudiwa.

www.JamiiForums.com

47	**Fungu 78: Sekretariati ya Mkoa wa Mbeya**
	• Sekretariati ya Mkoa wa Mbeya ihakikishe kuwa fedha zinaombwa kwa kiwango kinachotakiwa na itoe taarifa za maendeleo ya utekelezaji ili kuhalalisha Matumizi ya Maendeleo. • Katika mwaka tulioukagua, Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya haikupata fedha zilizoidhinishwa kiasi cha Sh. 28,008,474,533, na kwa maana hiyo shughuli zilizotengewa fedha hizo hazikutekelezwa. • Miradi ya maendeleo chini ya Sekretariati yenye thamani ya Sh. 59,000,0000 haikuwa imetekelezwa kama ilivyopangwa. • Tulipotembelea miradi mwezi Disemba 2011 tulibaini kuwa ofisi ya Katibu Tarafa ya Ilolo iliyopo wilayani Mbozi ilijengwa na kukamilika kwa thamani ya Sh. 29,000,000 lakini Sekretariati ya Mkoa haikuweza kupata Hati ya Kumiliki kiwanja ilipo ofisi hiyo.
48	**Fungu 79: Sekretariati ya Mkoa wa Morogoro**
	Uhalali wa gharama za usimamizi wa miradi haukupatikana Sh. 335,527,974 Sekretariati ilipokea kiasi cha Sh. 335,527,974 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu, merekebisho ya sekta ya umma, maendeleo ya kilimo, maji na usafi vijijini unaofanywa na

www.JamiiForums.com

	halmashauri mbalimbali katika mkoa. Upitiaji wa taarifa za usimamizi na ufuatiliaji ulibaini kuwa taarifa hizo hazikubainisha sababu za kushindwa kufanikiwa kwa halmashauri kwenye mipango/miradi tajwa, kwani miradi mingi imebainika kutekelezwa kwa kiwango cha chini wakati mingine haikukamilika kabisa. Kwa maana hiyo usamimizi na ufuatiliaji haukuleta tija iliyotarajiwa. • **Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 40,879,650** Hati za malipo ya Sh. 40,879,650 zililipwa zikiwa na nyaraka pungufu kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). • **Mishahara iliyolipwa kwa watumishi wasiokuwepo Sh.10,333,600.40** Jumla ya Sh.10,333,600.40 zililipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufukuzwa, kuacha kazi au akauti za watumishi waliokufa. • **Daftari lisilo na usahihi wa kumbukumbu za taarifa za mishahara ya watumishi wasiokuwepo** Katika mwaka tulioukagua, Sekretarieti haikuwa na daftari sahihi la mishahara ya watumishi wasiokuwepo kwani baadhi ya majina ya watumishi wasiokuwepo hayakuingizwa kwenye daftari. Hii ni kinyume na Kanuni ya 110 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (zilizorekebishwa 2004). Hii ina maana kwamba mishahara inaweza kulipwa kwa watumishi wasiokuwepo hivyo kuleta hasara.
49	**Fungu 80: Sekretariati ya Mkoa wa Mtwara**
	• Taarifa ya matumizi kiasi cha Sh. 276,446,222 kilichohamishwa kama mihadi iliyoahirishwa kulipwa

www.JamiiForums.com

	kutoka akauti ya maendeleo kwenda akaunti ya amana, haikutolewa na Sekretariati ya mkoa kwa ukaguzi • Taarifa ya Sekretariati ya Mkoa ilionesha kulikuwa na mali zisizoshikika za kiasi cha Sh. 146,428,000. Hata hivyo posho na matumizi mengineyo kiasi cha Sh. 88,215,850 zilijumuishwa pamoja na kiasi hicho cha mali zisizoshikika wakati sio sehemu ya mali hizo.
50	**Fungu 81: Sekretariati ya Mkoa wa Mwanza**
	• Ukaguzi wa baadhi ya taarifa za mishahara kutoka kwenye kompyuta, kumbukumbu za mishahara, pamoja na mafaili binafsi ya watumishi ulibaini kuwa kiasi cha Sh. 20,782,368 kililipwa kwa watu ambao hawakuwa watumishi tena lakini walibaki kwenye orodha ya kulipia mishahara badala ya kufutwa. Katika kiasi hicho Sh. 17,929,508.34 ilikuwa ni makato ya lazima yaliyolipwa kwa taasisi mbalimbali na Sh. 1,972,151 ni mishahara baada ya makato iliyolipwa kwa watu hao. • Ukaguzi ulibaini kuwa Sekretariati ililipa kiasi cha Sh. 10,085,000 kama honoraria na ununuzi wa samani nje ya bajeti. • Ukaguzi wa vitabu ulibaini kuwa Sekretariati ilinunua vitu vya kudumu vya thamani ya Sh. 46,083,400 lakini haikutumia vifungu vya vitu vya kudumu kulipia manunuzi hayo. • Sekretarieti ya Mkoa iliingia mkataba Na. RAS/009/2010/2011/W/02 wa tarehe 29 Juni , 2010 na M/s CF Builders Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Chumba cha Wagonjwa Mahututi, Jiko na ukarabati wa Chumba cha Upasuaji katika Hosptali ya Sékou

www.JamiiForums.com

	Toure kwa jumla ya Sh. 283,167,526.40. Tarehe ya kuanza kazi ilikuwa 13/07/2010 na ilitarajiwa kukamilika 30/11/2011. Hata hivyo, ziara yetu ya kutembelea miradi hiyo iliyofanyika mwezi Januari, 2012 ilibaini kwamba kazi zenye thamani ya Sh. 140,868,860 sawa na 49.70% zilikuwa bado hazijakamilika pamoja na kuwa muda wa mkataba ulikuwa umekwisha. • Sekretarieti ya Mkoa iliingia mkataba Na. RAS/09/2010/2011/W/04 tarehe 2 Septemba, 2011 na M/s Jeshi la Ujenzi wa Taifa (Suma JKT) kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana - Awamu ya III-Mwanza kwa mkataba wa Sh. 191,835,501. Tarehe ya kuanza kazi ilikuwa Septemba 9, 2011 na ilitarajiwa kukamilika tarehe 31 Disemba, 2011. Hata hivyo, ziara yetu ya kutembelea mradi huo iliyofanyika tarehe 8 Disemba, 2011 ilibaini kwamba kazi zenye thamani ya Sh. 79,600,000 zilikuwa bado hazijakamilika pamoja na kuwa muda wa mkataba ulikuwa umekwisha. • Katibu Tawala wa Mkoa aliingia mkataba Na. RAS/009/2010/2011/W/05 tarehe 2 Septemba, 2011 na M/s CF Builder Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Awamu III kwa mkataba wa Sh. 361,096,815. Tarehe ya kuanza kazi ilikuwa 9 Septemba, 2011 na ilitarajiwa kukamilika tarehe 19 Disemba, 2011. Hata hivyo, ziara yetu ya kutembelea jengo hilo tarehe 19 Disemba, 2011 ilibaini kwamba kazi hiyo ilikuwa haijaanza.
51	**Fungu 82: Sekretariati ya Mkoa wa Ruvuma**
	Mambo Mengineyo Jumla ya Sh. 12,087,500 zililipwa kwa watu mbalimbali kama masurufu kwa ajili ya ununuzi wa

www.JamiiForums.com

	vitu mbalimbali. Kuna uwezekano kwamba bei za marejesho zilikua zaidi ya bei halisi, hivyo haikuthibitika kuwa matumizi hayo yaliinufaisha Sekretariati. Matumizi ya jumla ya Sh. 38,655,268 yalilipwa chini ya vifungu (GFS) visivyostahili kinyume na Kanuni ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (zilizorekebishwa 2004), hivyo ikiashiria ukosefu wa udhibiti wa bajeti. Malipo ya jumla ya Sh. 5,600,000 hayakuwa na vithibitisho vya madai kama vile ankara, uthibitisho wa kuleta bidhaa, stakabadhi, karatasi za kulipia na daftari la mahudhurio. Hii ina maana kwamba sehemu ya ukaguzi wa awali ni dhaifu. Katika mwaka unaokaguliwa, mafuta yenye thamani ya Sh. 2,267,000 yaliyonunuliwa hayakuthibitika kuwa yalipokelewa na kuingizwa vitabuni. Hivyo uingizwaji vitabuni na matumizi yake havikuweza kuhakikiwa. • Madai ya Sh. 23,896,583.24 yalijumuishwa kwenye madeni bila kuwa na vithibithso vya deni kama Ankara au mikataba. • Kazi za ziada kwenye mkataba zenye thamani ya Sh. 20,664,320 hazikuidhinishwa ipasavyo. Kazi za ziada zinaweza kuongeza gharama za mkataba nje ya makisio kama zisiposimamiwa ipasavyo. • Sekretarieti ililipa jumla ya Sh. 15,092,800 kwa shughuli mbalimbali lakini uhalali wa malipo hayo haukuthibitika kwa sababu zifuatazo: – ➢ Malipo ya posho ya kujikimu kwa waajiriwa wapya yalijumuisha wategemezi wasiostahili posho hizo. ➢ Baadhi ya watumishi walilipwa posho za kujikimu

www.JamiiForums.com

	wakiwa safarini bila kusafiri kama ilivyothibitishwa na saini zao kwenye karatasi za mahudhurio siku ambazo walitakiwa kuwa safarini. ➢ Malipo ya malazi yalibainika kufanywa kwa hoteli ambayo haina uwezo wa kuweka idadi ya wageni iliyotajwa. ➢ Baadhi ya Manunuzi hayakufuata taratibu za kawaida za manunuzi.
52	**Fungu 83: Sekretariati ya Mkoa wa Shinyanga**
	Matengenezo ya magari yalifanywa bila ya kupitishwa kwanza kwa Wakala wa Mitambo na Umeme (TEMESA) Sh. 6,569,797 Ilionekana kwamba malipo ya Sh. 6,569,797 yalilipwa kwa gereji binafsi kwa ajili ya matengenezo ya magari ambayo hayakuwa yamepitishwa kwanza kwa Wakala wa Serikali wa Umeme na Mitambo (TEMESA) kinyume na Kifungu 59 (1) na (2) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005 (GN.97). • **Makato kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi ya kila mwezi yaliyozidi kiwango kinachokubalika** Ukaguzi wa baadhi ya kumbukumbu za mishahara umebaini kuwa makato kutoka kwenye mishahara yalizidi kikomo cha theluhi (1/3) kilichowekwa na Utumishi (PO-PSM) kwa barua Kumb. Na. C/CE.45/271/01/1/87 ya 19/3/2009 na Sheria ya Mikopo Namba 7 ya mwaka 1970.
53	**Fungu 84: Sekretariati ya Mkoa wa Singida**
	Kiasi cha Sh.19,000,000 kililipwa kwa M/S Garage Action Auto wa S.L.P 2645 Dodoma kama malipo kwa ajili ya matengenezo ya gari lenye usajili Na. STK

www.JamiiForums.com

	5331. Hata hivyo, gari hilo halikuwa limetoka gareji hadi tunaandika taarifa hii. Sekretarieti ya Mkoa wa Singida ilifanya malipo ya Sh. 29,120,000 kwa Afisa Usalama - Singida kwa shughuli za Mitihani ya Taifa ya kidato cha nne iliyofanyika Oktoba 2010. Hata hivyo viambatisho vya malipo hayo havikutolewa kwa ajili ya uhakiki.
54	**Fungu 85: Sekretariati ya Mkoa wa Tabora**
	Ukiukaji wa kanuni na taratibu • **Matumizi yaliyofanywa chini ya vifungu visivyo husika Sh. 26,151,386** Kiasi cha Sh. 26,151,386 kililipiwa chini ya vifungu visivyo stahili wakati matumizi hayo hayakuwa yametengewa fedha kwenye bajeti. Sekretariati ilikarabati nyumba anayokaa Mkuu wa Mkoa wakati hakukuwa na bajeti ya kazi hiyo. • **Matengenezo ya gari lenye usajili Na. STK 4888 kiasi cha Sh. 40,643,265 yenye mashaka** Gharama za matengenezo ya gari lenye usajili Na. STK 4888 zilibainika kuwa kasoro zifuatazo: • Hati ya kuthibitisha kukamilisha kazi haikutolewa kwa ukaguzi, injini mpya iliyoelezwa kuwa ilifungwa haikuoneshwa kweye kadi ya kazi na hapakuwa na risiti kukiri kupokea Sh. 40,643,265 za malipo. **Masuala Mengineyo** Madeni yasiyolipwa ya Sh. 851,096,823.18 yalikuwa vitabuni tarehe 30 Juni, 2011. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao zilizopangwa kwa kutumia bajeti ya mwaka kulipia madeni ya nyuma.

www.JamiiForums.com

55	**Fungu 86: Sekretariati ya Mkoa wa Tanga**
	• Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga iliingia mkataba na Mkandarasi M/s Chite Trader Contractor kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa nje kwenye makazi ya Mkuu wa Wilaya. Mkataba ulikuwa ni wa wiki 12 hadi Septemba 4, 2011. Hata hivyo, pamoja na ujenzi kutokamilika mpaka tarehe ya ukaguzi (Novemba, 2011), hakuna makato yoyote ya adhabu ya ucheleweshaji kazi yaliyokatwa kwenye malipo yanayofanywa kwa mkandarasi. • Madeni yasiyolipwa ya Sh. 596,703,205.50 yalikuwa vitabuni tarehe 30 Juni, 2011. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao zilizopangwa kwa kutumia bajeti ya mwaka kulipia madeni ya nyuma.
56	**Fungu 88: Sekretariati ya Mkoa wa Dar Es Salaam**
	• Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam alimlipa Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala kwa Hati ya Malipo Na. 3463/6 H/Na. 997647 ya 28/6/11 kwa ajili ya kupata viwanja 71 eneo la kinyerezi kwa ajili ya kuwapatia waathirika wa mabomu yaliyotokea Gongo la Mboto Dar es Salaam. Viwanja vya Kinyerezi viliwekewa pingamizi mahakamani na hivyo RAS DSM akaamua kutafuta viwanja vingine eneo la Msongola. Hata hivyo hatukuweza kupata uthibitisho kama viwanja hivyo vilipatikana Msongola na maendeleo ya mpango wa viwanja hivyo. • Bakaa ya Akaunti ya Amana ya Juni 30, 2011 ilijumuisha Sh. 437,849,688 zilizo hamishiwa kutoka Akaunti ya Maendeleo kama mihadi. Hata hivyo, mihadi hiyo haikuoneshwa kwenye taarifa ya mihadi ya Akaunti ya Maendeleo ya tarehe 30

www.JamiiForums.com

	Juni 2011 kinyume na Kifungu Na. 25 (2) (b) cha Sheria ya Fedha ta Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). • **Mchanganuo wa wawekaji kwenye akaunti ya Amana hakutolewa Sh. 601,955,154** Mchanganuo wa wawekaji katika akaunti ya Amana haukuwasilishwa pamoja na taarifa za fedha. Kutokana na hali hiyo hatukuweza kuhakiki usahihi wa bakaa za wawekaji zenye jumla ya Sh. 601,955,154 katika akaunti hii ya amana kwa kipindi kilichoishia 30 Juni 2011. Hundi ya kiasi cha Sh. 13,935,000 iliyolipwa na IPP Ltd kwa ajili ya waathirika wa mabomu ya Gongo la Mboto ilirejeshwa kutokana na kuzidi kiwango kinachoruhusiwa kulipia hundi cha Sh. 10,000,000, hivyo mlipaji kutakiwa kuwasilisha fedha hizo kwa TISS. Hata hivyo fedha hizo hazikuthibitika kulipwa tena.
57	**Fungu 89: Sekretariati ya Mkoa wa Rukwa**
	• Sekretariati ya Mkoa wa Rukwa inapaswa kuhakikisha kuwa ukarabati wa hospitali ambao umeshagharimu Sh. 142,273,907 kati ya Sh. 200,000,000 zilizopangwa unakamilika na hivyo huduma ya hospitali kuwa bora zaidi • Sekretariati ya Mkoa wa Rukwa inapaswa kuharakisha ujenzi wa nyumba za watumishi ambazo zimeshagharimu Sh. 100,000,000 kati ya Sh. 420,000,000 zilizopangwa unakamilika na hivyo kupunguza watumishi kuondoka mkoani. • Serikali kwa kupitia Sekretariati ya Mkoa wa Rukwa ilipeleka jumla ya Sh. 17,433,136,301 kwa Manispaa na Halmashauri za Wilaya. Sekretariati ioanishe

www.JamiiForums.com

	mifumo ya udhibiti katika halmashuri inazozisimamia ili kuongeza ufanisi na tija na kuongeza manufaa ya fedha zinazotolewa. **Masuala Mengineyo** Kuna mapendekezo ya ukaguzi uliopita yanayohusisha jumla ya Sh.43,484,890.93 ambayo hayajatekelezwa ipasavyo. Hii inaviza juhudi za kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa fedha katika Sekretarieti ya Mkoa.
58	**Fungu 95: Sekretariati ya Mkoa wa Manyara**
	Malipo ya kiasi cha Sh. 84,073,500 kililipwa kwa watumishi mbalimbali na taasisi zingine bila ya kuwa na viambatisho kama stakabadhi, fomu za maombi, orodha za walipwaji, orodha za mahudhurio n.k. kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (zilizorekebishwa 2004). Hesabu za mwaka zimeonesha kuwa kuna madeni ya jumla ya Sh. 51,850,980 yanahusisha Katibu Tawala wa Wilaya ya Kiteto (Sh. 32,251,695) na Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati (Sh.19,599,285) ambayo hayakuwa kwenye daftari la wadeni, kwa maana hiyo tumeshindwa kujua kama madeni haya ni halali.

7.9 Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa zilizopata hati zenye shaka

Zifuatazo ni Wizara na Idara za Serikali zilizopata hati zenye shaka pamoja na sababu zake.

1.	**Fungu 14: Idara ya Zima Moto na Uokozi**
	• Idara haina michanganuo ya kina kwa ajili ya mapato na malipo mengineyo ya kiasi cha Sh.

www.JamiiForums.com

	1,804,733,968.66 na Sh. 1,550,247,999 sawia kama yanavyoonekana kwenye ukurasa wa 18 wa taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia 30th Juni, 2011. Kutokana na kukosekana uwazi wa kutosha, usahihi wa mapato na malipo haukuweza kuthibitishwa. • Kiasi cha Sh.182,048,226 kwa ajili ya mafao ya watumishi kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha hakikuwa na michanganuo ya kiasi hicho. • Kiasi cha Sh.184,282,950 kwa ajili ya vifaa kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha hakikuwa na michanganuo ya kiasi hicho. • Kiasi cha Sh. 559,510,005.64 kwa ajili ya manunuzi na vifaa vya ofisini kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha kwa kipindi kilichoishia 30 Juni 2011 hakikuwa na michanganuo ya kiasi hicho. • Jumla ya Sh. 17,829,800 zililipwa kwa M/S Kim Builders and General Traders kwa hati ya malipo Na. 0602 hundi Na. 055312, ankara Na. 0065 na hati ya kuthibitisha vifaa kuletwa Na. 0013 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi vya Idara. Hata hivyo, vifaa hivyo havikuingizwa vitabuni wakati wa kupokewa wala wakati wa utoaji wa vifaa kwa watumiaji. • Idara haikuweka bayana jinsi itakavyolipa madeni ya Sh. 557,680,368.09 yaliyobaki vitabuni mwishoni mwa mwaka. **Masuala Mengineyo** • Uongozi wa Idara ya Zimamoto na Uokozi uliwalipa wakandarasi mbalimbali jumla ya kiasi cha Sh. 318,000,000 kwa kazi ambazo hazikuwa zimethibitishwa na washauri na wasimamizi wa

www.JamiiForums.com

	miradi husika. • Uongozi wa Idara ya Zimamoto na Uokozi haujatekeleza na wala hauna Sera ya Mawasiliano na Technolojia. • Uongozi wa Idara ya Zimamoto na Uokozi hauna sera ya kusimamia viashiria vya hatari ambayo ingebainisha jinsi ya kushughulikia viashiria hivyo vya hatari.
2.	**Fungu 18 : Mahakama Kuu**
	• Gharama ndogo ndogo za ujenzi kiasi cha Sh. 109,900,000 zilijumuishwa kwenye gharama za jengo na ardhi wakati kiasili gharama hizo si za vitu vya kudumu. Kosa hilo la kihasibu bado halijarekebishwa vitabuni. • Mahakama Kuu ililipa Sh. 23,700,000 badala ya Sh. 8,400,000 kama kodi ya mwaka kwa kipindi cha kuanzia Januari 2010 hadi Disemba 2010 kwa ajili ya nyumba ya makazi iliyopo kiwanja Na. 658 Mbezi, Dar es Salaam. Malipo haya yalifanyika baada ya kubadili masharti ya mkataba wa upangaji bila kufuata taratibu hivyo kusababisha malipo ya zaidi ya Sh. 15,300,000 (Sh. 23,700,000 – Sh. 8,400,000). • Malipo ya Sh. 27,359,720 yalifanywa bila ya kuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). Kutokana na hali hiyo tumeshindwa kuthibitisha kama malipo husika yalikuwa halali. • Mahakama Kuu ililipa Sh. 18,018,540 kwa wafanyakazi ambao ajira zao zilikuwa zimekoma kwa kustaafu au kifo lakini bado walikuwa hawajafutwa kwenye orodha ya kulipia mishahara.

www.JamiiForums.com

	• Masurufu yasiyorejeshwa ya kiasi cha Sh. 97,469,800 hayakuingizwa katika taarifa za fedha, hivyo kufanya taarifa hizo kuwa na makosa. • Mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 2,071,624,728 ziliingizwa kwenye taarifa za fedha bila ya kuwa kwenye orodha ya mali za kudumu.
3.	**Fungu 19: Mahakama za Mwanzo na za Wilaya**
	• Gharama za matengenezo madogo ya kiasi cha Sh. 79,841,000 zilijumuishwa kwenye gharama za jengo na ardhi wakati kiasili gharama hizo si za vitu vya kudumu. Kosa hilo la kihasibu bado halijarekebishwa vitabuni. • **Makusanyo yasiyopelekwa benki Sh. 48,106,602.74** Kiasi cha Sh. 48,106,602.74 kilichokusanywa katika mwaka wa fedha 2010/2011 kutoka vituo mbalimbali vya ukusanyaji mapato hakikupelekwa benki kinyume na Kanuni ya 60 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (zilizorekebishwa 2004). Aidha, jumla ya kiasi cha Sh. 1,076,950 kilikuwa ni pungufu kwenye kiasi kilichopelekwa benki. • Mahakama za Mwanzo na za Wilaya zililipa Sh. 148,544,460 kwa wafanyakazi ambao ajira zao zilikuwa zimekoma kwa kustaafu au kifo lakini bado walikuwa hawajafutwa kwenye orodha ya kulipia mishahara. • Tulibaini kuwa mapokezi katika kitabu cha kupokelea kiasi cha Sh. 159,314,3246.72 na kiasi kilichothibitishwa kupokelewa kwa mujibu wa taarifa za benki Sh. 607,299,059.96 ambavyo havikuwa na uhusiano kwa upande mmoja na

www.JamiiForums.com

	mwingine kama ilivyopaswa kuwa. Usuluhishi haukuwa umefanyika kubaini na kurekebisha kasoro hii. • Mahakama za Mwanzo na za Wilaya zilikuwa na madeni ya Sh. 2,072,904,877.84 na mihadi ya kiasi cha Sh. 259,314,508.93 kutokana na manunuzi ya bidhaa na huduma na vilevile madai ya watumishi. Madeni haya yanaweza kuathiri shughuli za mwaka ujao ikiwa fedha za mwaka huo zitalipia madeni haya. • Mali za kudumu za kiasi cha Sh. 1,985,972,390 zinazomilikiwa na Wizara ya Sheria na Katiba chini ya Mahakama za Mwanzo na za Wilaya hazikuorodheshwa kwenye daftari la mali za kudumu.
4.	**Fungu 24: Tume ya Maendeleo ya Ushirika**
	Tume ililipa kiasi cha Sh. 2,606,150 kwa wauzaji wa bidhaa na huduma pamoja na wafanyakazi wa Tume kwa shughuli mbalimbali. Hata hivyo, hati za malipo na nyaraka zilizoambatishwa na malipo hayo hazikutolewa kwa ajili ya ukaguzi. **Matumizi yasiyokubalika Sh. 43,035,000** Jumla ya Sh.43,035,000 zilizolipwa kwa mwaka uliomalizika hazikuwa na nyaraka za kutosha kwa ajili ya uhakiki. **Malipo yaliyoahirishwa Sh. 34,953,650** Matumizi ya Sh.34,953,650, ya mwaka 2009/2010 yaliahirishwa na kuja kulipwa mwaka 2010/2011 kinyume na Kanuni ya 85 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (zilizorekebishwa 2004). **Malipo zaidi ya madeni yaliyohakikiwa Sh. 1,145,671,870** Madeni ya kiasi cha Sh. 629,522,680 ya Chama Cha

www.JamiiForums.com

	Ushirika - Nyanza yalihakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kulipwa mwezi Oktoba 2009 na Machi, 2010. Hata hivyo Nyanza ilikuja kulipa madeni mengine ya Sh. 1,145,671,870 ya 2010/2011 ambayo hayakuwa kwenye yale yaliyohakikiwa. **Masuala Mengineyo** **Vifaa na nyaraka vilivyolipiwa bila ya kuletwa Sh.36,118,000** Nyaraka zilizochapishwa za kiasi cha Sh. 23,513,000 kutoka Mpiga Chapa wa Serikali na vifaa vya ofisi vya Sh. 12,605,000 kutoka kwa wazabuni mbalimbali vilivyoagizwa na kulipiwa havikuwa vimefika mpaka wakati wa ukaguzi (Oktoba, 2011).
5.	**Fungu 32: Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi Wa Umma**
	• Kutokana na utunzaji wa kumbukumbu usiofaa Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilikuwa na matumizi ya Sh. 2,681,019,858 yaliyofanywa kwa kutumia hati za malipo zisizokuwa na nyaraka za kutosha. Kiasi hiki kiliingizwa vitabuni, lakini uhalali wake haukuweza kuthibitika. • Tulibaini tofauti kubwa ya Sh. 1,769,926,271 kati ya kiasi cha Sh. 581,600,000 kilichooneshwa kwenye kifafanuzi Na. 19 cha taarifa ya mwaka kinachohusu ujenzi na ununuzi wa mali za kudumu na kiasi cha Sh. 2,351,526,271 kilichomo kwenye orodha ya mali za kudumu. Hivyo hatukuweza kujiridhisha kuwa bakaa ya mali za kudumu iliyomo kwenye mizani ni sahihi na yakuaminika. Ofisi ya Raisi - Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanapaswa kusuluhisha na kusahihisha tofauti iliyoonekana ili vitabu na taarifa vitoe taswira sahihi.

www.JamiiForums.com

6.	**Fungu 40: Mahakama ya Rufani**
	• Ununuzi wa Mali, Mitambo, na Vifaa vya Sh. 41,422,152,408 havikuwa vimeingizwa kwenye daftari la orodha ya mali za kudumu, hivyo hatukuweza kujiridhisha juu ya matumizi yaliyofanywa ili kupata vitu hivyo. • Stakabadhi za kukusanyia mapato za kiasi cha Sh. 17,044,773 ambazo ziliorodheshwa kwenye Kitabu cha Mkusanya Mapato (RCCB) hazikutolewa ili kuthibitisha kiasi kilichokusanywa na kupelekwa benki kinyume na Kanuni ya 65 (1) na (3) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (zilizorekebishwa 2004). • Kanuni ya 78 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (zilizorekebishwa 2004) inataka, mapato yanayokusanywa kuwasilishwa benki kila siku kama yalivyo. Kinyume chake, mapato ya kiasi cha Sh. 11,417,071 yalikusanywa kutoka vituo mbalimbali bila ya vithibitisho kuwa yalipelekwa benki.
7.	**Fungu 46: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi**
	Wizara ilionesha kuwa na bakaa ya fedha taslimu Sh. 3,543,412,937 katika taarifa za fedha. Lakini nyaraka zilizopatikana kutoka Ofisi Kuu ya Malipo (CPO) zilionesha bakaa tofauti ya Sh.14,931,082,406. Kwa hiyo, bakaa ya fedha taslim iliyomo kwenye taarifa ya fedha haikuweza kuthibitika kuwa ni ya kuaminika. Machanganuo ni kama ufuatao:

Akaunti	**Bakaa Jumuifu ya taslimu kutoka taarifa ya ofisi kuu ya malipo (Sh.)**
Akaunti Ya Amana	14,253,691,194
Akaunti Ya Maendeleo	332,934,251
CPS Amana maalum A/C	28,686,931

www.JamiiForums.com

(16.141)	
CPS Mat. Kawaida A/C (18.330)	315,770,030
Jumla	**14,931,082,406**

• Fedha zilizopelekwa kwenye taasisi lakini hazikuthibitika kupokelewa au zilipokelewa zaidi ya kiasi zilichotolewa

Wizara ilitoa jumla ya Sh. 445,058,164,147 sawa na 75.5% ya kiasi kilichopokelewa katika mwaka kwa taasisi ishirini na tisa (29) zilizo chini ya Wizara. Uthibitisho wa kupokea fedha kutoka kwa taasisi hizo kwa miaka 2009/2010 na 2010/2011 uligundua kwamba taasisi tatu (3) hazikupokea jumla ya Sh. 1,486,134,045 wakati taasisi saba (7) zilipokea Sh. 14,470,198,562 zaidi ya kiasi kilichotolewa. Aidha, taasisi kumi na tisa (19) hazikuweza kututhibitishia kama zilipokea Sh. 637,269,015,239 zilizodaiwa kutolewa.

Bakaa ya Mali za kudumu isiyo ya kweli Sh. 34,684,834,642

Wizara ilionesha vitabuni ongezeko la mali za kudumu kwa kiasi cha Sh. 34,684,834,642 ambazo hazikuwa na majedwali ya mchanganuo wake.

Uhamisho wa Sh. 21,870,959,025 kwenda vyuo na vyuo vikuu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo vilioneshwa kama ongezeka la mali kwenye taarifa za fedha za wizara.

Uongozi hakuwasilisha ukaguzi nyaraka za mali za kudumu za Sh. 33,468,773,693 zilizojumuishwa kwenye bakaa ya Sh. 34,684,834,641 iliyopo katika taarifa za fedha.

Bakaa ya vifaa isiyo sahihi kwa Sh. 1,089,130,222

www.JamiForums.com

	Bakaa ya vifaa na mali nyingine ya Sh. 1,089,130,222 ilijumuishwa kwenye bakaa ya taarifa za kifedha ya Sh. 2,814,588,173 ikiwa haina nyaraka zinazoweza kuhakikiwa. **Madeni hayakuingizwa kwenye taarifa za fedha Sh. 5,063,267,729** Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ilikuwa na madeni yanayohusu Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki na Mradi wa Vitabu Mzumbe ya jumla ya Sh. 5,063,267,729, lakini hayakuingizwa kwenye taarifa za fedha. **Malipo yasiyo na viambatisho** Hati za malipo ya Sh. 1,368,769,051 hazikuweza kupatikana wakati malipo ya Sh. 3,885,667,644 yalikuwa na nyaraka pungufu, kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (zilizorekebishwa 2004).
8.	**Fungu 92: Tume ya Kudhibiti Ukimwi**
	Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) ina akaunti NMB inayojulikana kama Akaunti ya Malipo Mbalimbali ya TACAIDS Na. 2011100141 ambayo uongozi unaitumia kwa shughuli zingine zilizo nje ya mfumo wa Mfuko Mkuu wa Serikali. Taratibu za uendeshaji wa Akaunti hii hazikuwekwa bayana kwani si taarifa ya benki wala usuluhishi wake vilivyotolewa kwa wakaguzi. Tulipotaka kupata uthibitisho NMB Oktoba 2010 hatupata majibu mpaka wakati tunaandaa taarifa hii Februari 2011. Kwa maana hiyo hatukuweza kukagua bakaa wala kujua mwenendo wa Akaunti hiyo kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2011. **Masuala Mengineyo**

www.JamiiForums.com

	• **Kodi ya Mshahara (PAYE) iliyolipwa pungufu Sh. 79,128,598** Ukokotozi wa kodi ya mishahara (PAYE) kwa wafanyakazi 186 haukuhusisha posho, na hivyo kusababisha kodi iliyolipwa TRA kuwa pungufu kwa Sh. 79,128,598 kwa kipindi cha Julai, 2010 hadi Juni, 2011.
9.	**Fungu 94: Ofisi ya Raisi Tume ya Ajira Serikalini**
	Kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi Fedha zilizohamishwa Sh. 575,202,800 hazikuwa na stakabadhi za kuthibitisha kupokelewa na wapokeaji, na michanganuo ya matumizi yake. Hivyo basi, uhalali wa matumizi na makusudio yake hayakujulikana. Tume ililipa Sh. 10,513,000 kama posho ya kujikimu kwa siku kumi na tatu (13) kwa maofisa ambao walisafiri nje ya nchi katika ziara ya kikazi. Ulipaji huu wa posho hakuzingatia kuwa wahusika walishalipiwa kila kitu yakiwemo malazi hivyo kufanya malipo kuwa mara mbili. Ukaguzi wa hati za malipo za matumizi ya kawaida ulibaini kuwa malipo ya jumla ya Sh. 5,940,000 yalifanywa bila nyaraka husika kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (zilizorekebishwa 2004). Tume iliwapa ada ya jumla ya Sh. 15,710,000 wafanyakazi wake waliokuwa masomoni badala ya kulipa moja kwa moja vyuoni. Stakabadhi za vyuo husika kukiri kupokea malipo hayo hazikupatikana ili zihakikiwe.
10.	**Fungu 74: Sekretariati ya Mkoa wa Kigoma**
	• Bakaa ya fedha taslimu Sh. 106,101,486 ya 30 Juni 2009 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha haikuingizwa kama bakaa ya kuanzia kwa mwaka uliofuatia kwa kipindi kilichoishia 30 Juni 2010. Athari ya kosa hilo imekuwa ni kuandikwa kwa bakaa

www.JamiiForums.com

	ya fedha taslimu kimakosa kwa vipindi vilivyofuata vya 30 Juni 2010 na 30 Juni 2011 kwa kiasi hicho. • Sekretariati haikuadaa na kuwasilisha taarifa ya usuluhishi ya benki kwa akaunti za matumizi ya kawaida, amana, na maduhuli kwa mwaka 2010/2011, kutokana na hilo, usahihi wa bakaa ya fedha iliyooneshwa kwenye vitabu vya fedha haukuthibitika. **Bakaa ya vifaa Sh. 82,994,991** Bakaa ya vifaa ya Sh. 82,994,991 iliyomo kwenye taarifa za fedha haikuambatishwa na hati ya kuthibisha kuhesabiwa vifaa hivyo mwishoni mwa mwaka. • Matumizi ya mafuta ya Sh. 132,535,232 kwenye magari hayakuthibitika uhalali wake kwa kuwa hakukuwa na kumbukumbu zozote za matumizi ya magari kwenye daftari la mwenendo wa magari. • Malipo ya Sh. 191,271,601.62 hayakuwa na nyaraka za kutosha kutokana na udhibiti dhaifu wa utunzaji wa kumbukumbu. • Sekretariati ililipa Sh. 57,614,067.75 kwa gereji binafsi mbalimbali ikiwa ni gharama za matengenezo ya magari za miaka ya nyuma. Hata hivyo, madeni hayo hayakuwa kwenye kumbukumbu zozote kuonesha kuwa yalikuwepo. • Sekretariati ilifanya matengenezo ya magari ya Sh. 47,567,906 bila ya kuyapitishwa kwanza kwenye gereji ya Serikali. • Ukaguzi wa hati za malipo na daftari la orodha ya masurufu ulibaini kuwa masurufu ya kiasi cha Sh. 67,287,700 hayakuwa yamerejeshwa mpaka wakati wa ukaguzi.

www.JamiiForums.com

	• Mishahara isiyolipwa kiasi cha Sh. 22,091,007.46 iliyopokelewa kutoka halmashauri na Sekretariati yenyewe haikurejeshwa Hazina kinyume na Waraka wa Serikali Na. EB/AG/5/03/01 Vol. VI/36 wa 31 Agosti, 2007.
11.	**Fungu 85: Sekretariati ya Mkoa wa Kagera**
	• **Kuchepushwa fedha za maendeleo Sh. 481,017,718** Fedha za maendeleo kiasi cha Sh. 481,017,718 zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Kabango na ujenzi wa jengo jipya la ofisi ya Mkoa wa Kagera zilichepushwa nakutumika kwa shughuli nyingine. • **Malipo yalifanywa kutoka akaunti ya amana bila ya kunukuu stakabadhi ya kupokelea fedha kwenye akaunti hiyo Sh. 572,402,630** Jumla ya Sh. 572,402,630 zililipwa kutoka Akaunti ya Amana bila ya kunukuu stakabadhi iliyopokelea fedha hizo kwenye akaunti hiyo. Kukosekana stakabadhi ya kupokelewa fedha hizo kunaashiria kuwa fedha za wawekaji wengine zinaweza kutumika isivyokusudiwa. • **Matumizi yasiyoidhinishwa kutoka kwenye fedha za maendeleo Sh. 200,221,879** Katika mwaka husika, fedha za mradi jumla ya Sh. 200,221,879 zililipwa kwa ajili ya shughuli nyingine. **Masuala Mengineyo** • **Ujenzi wa nyumba ya kuishi Katibu Tawala katika Wilaya ya Missenyi Awamu ya I Usioendelea Sh. 40,630,759** Awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba ya kuishi Katibu Tawala wa Wilaya ya Missenyi kwa mkataba ambao ulipangwa kukamilika tarehe 2 Oktoba 2010, ilionekana kusimama katika hatua ya ukuta kama tulivyobaini wakati wa ziara ya eneo hilo

www.JamiiForums.com

	tarehe 27 Disemba 2011. Wakati huo kiasi cha Sh. 40,630,759 kilikuwa tayari kimeshalipwa kwa mkandarasi. • **Ujenzi wa Wodi Daraja A katika Hospitali ya Mkoa wa Kagera awamu ya pili, ujenzi umekamilika lakini haitumiki** Tarehe 25 Mei, 2010 Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera ilisaini mkataba kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa wodi daraja A katika Hospitali ya Mkoa wa Kagera kwa Sh. 210,991,080 ikijumuisha VAT, kwa kipindi cha Juni 2, 2010 hadi Oktoba 27, 2010. Hata hivyo, ziara tulioifanya Disemba 28, 2011 ilibainisha kuwa, wodi ilikuwa imekamilika lakini haitumiki. • **Ujenzi wa Ofisi Mpya ya Mkoa wa Kagera Kwa Sh. 537,784,004 uliosimama** Malipo ya kiasi cha Sh. 537,784,004 yalifanywa kutoka Akaunti za Maendeleo, Amana, na Akaunti ya Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mkoa wa Kagera. Wakati wa ziara tulioifanya Disemba 28, 2011 tulibaini kuwa, hakuna kazi ya ujenzi iliyokuwa ikiendelea na mkandarasi hakuwa katika eneo la kazi, ingawa baadhi ya vifaa vya ujenzi na Lori moja vilikuwepo. • **Madeni Sh. 892,603,137** Taarifa ya fedha ya Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera ilionesha madeni ya kiasi Sh. 892,603,137 yasiyolipwa yaliyotokana na kazi za mikataba. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka ujao ikiwa kiasi kutoka kwenye bajeti kitatumika kwa ajili ya kulipa madeni hayo.
12.	**Taarifa za Hesabu Jumuifu za Taifa**

www.JamiiForums.com

1. Mapitio ya taarifa za kifedha za Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 zilionesha kiasi ambacho Benki Kuu inaidai Serikali na kile ambacho Serikali inaidai Benki Kuu. Hata hivyo kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye Taarifa za Hesabu Jumuifu kama madeni au madai ya Serikali kwa Benki hiyo.

   Kutotoa taarifa sahihi za madeni, mali na uwekezaji wa Serikali katika taasisi zake inafanya taarifa za fedha isiwe na picha halisi ya kifedha mwishoni mwa mwaka. Madeni na madai haya ni pamoja na:

   a) **Kiasi kinachodaiwa na Benki Kuu**

      (i) Madeni Kwenye Akaunti za Serikali Sh. 548,333 milioni

      Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na deni la Sh. 548,333 milioni mpaka tarehe 30 Juni, 2011 (2010: Sh. 429,466 milioni) ikiwa ni fedha zilizochukuliwa kwenye akaunti za Serikali.

      (ii) Mfuko wa Uwezeshaji Sh. 15,461,000,000

      Kiasi cha Sh. 15,461,000,000 kilioneshwa kama madai kutoka Serikalini kuhusiana na fedha zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kuwezesha utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji wa kiuchumi kwa niaba ya Serikali.

      (iii) Gharama za Kupunguza Ujazo wa Fedha Katika Mzunguko Sh. 22,195 milioni

      Kiasi cha Sh. 22,195.3 kilijumuishwa kwenye madai ya Benki Kuu ya tarehe 30 Juni, 2011 (2010: Sh. 26,851.5) ikiwa ni mgao wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa gharama za kupunguza ujazo wa fedha katika mzunguko kwa mwaka 2010/2011. Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki Kuu ya Tanzania zimekubaliana kuchangia

www.JamiiForums.com

gharama hizo kwa kanuni zilizowekwa katika Mkataba wa Makubaliano.

(iv) Riba inayodaiwa na Benki Kuu kutokana na Serikali kuchukua fedha zaidi kwenye akaunti Sh. 17,530.4 milioni

Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2011 Serikali ilichukua kiasi cha Sh. 17,530.4 milioni zaidi ya fedha zilizokuwepo kwenye akaunti zake (2010: Sh. 3,456.6 milioni). Kulingana na kifungu cha 34 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, Serikali inadaiwa kiasi cha Sh. 17,530.4 milioni.

(b) Kiasi kinachodaiwa na Serikali Sh. 25.059 bilioni

(i) Gharama za kuhudumia Madeni Sh. 25.059 bilioni

Kiasi hicho kinahusisha kiasi kilichopokelewa na Benki kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kulipa madeni ya nje na huduma nyingine kwa fedha za kigeni kwa niaba ya Serikali.

(ii) Ulipaji wa Madeni ya Serikali Sh. 25.562 bilioni

Kiasi hiki kinahusu fedha zinazosuburi kulipwa nje ya nchi kupitia Benki Kuu kwa niaba ya Serikali mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2011 kufuatia kuanzishwa kwa malipo kwa njia ya mtandao katika kipindi cha mwaka huo wa fedha.

(iii) Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Dhamana Sh. 11.166 bilioni

Kwa mujibu wa Benki Kuu, Mfuko wa Maendeleo wa Dhamana ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusaidia miradi ya maendeleo inayojishughulisha na utengenezaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje.

www.JamiiForums.com

		Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2011, mchango wa Serikali kwenye mfuko huo kwa mwaka 2003/2004 na 2005/2006 ni Sh. 56,500.0 milioni. Riba iliyopokelewa na inayodaiwa na Serikali kutokana na mikopo ni Sh. 15,771.9 milioni wakati jumla ya Sh. 2,448.54 milioni zilipatikana kutokana na riba kutoka fedha zilizowekezwa kwenye Dhamana za Hazina (Treasury Bills). Jumla ya Sh. 61,668.2 milioni hadi sasa zimetolewa kama mikopo kwa ajili ya kuyawezesha makampuni yanayouza maua na mboga nje ya nchi. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2011 Mfuko ulikuwa na bakaa ya Sh. 11,166.7 milioni (2010: Sh. 7,881.2 milioni). **(iv) Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa usafirishaji nje ya nchi Sh. 41.841 bilioni** Mfuko ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2001 chini ya mfumo wa dhamana ya mikopo kwa wanaouza nje ya nchi, katika jitihada za kukuza mauzo ya nje. Mfuko hutoa dhamana kwa benki za biashara kufidia uwezekano wa baadhi ya wakopaji kutolipa mikopo yao. Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali iliongeza mtaji wa Sh. 4,309.5 milioni kwenye mfuko. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2011 Mfuko alikuwa na bakaa ya Sh. 46,904.3 milioni (2010: Sh. 31,783.5 milioni) inayojumuisha michango ya Serikali na Benki Kuu na mapato yatokanayo na uwekezaji katika Dhamana za Hazina na ada ya mikopo. **(v) Mfumo wa kubadilisha madeni Sh. 2.098 milioni** Hii ni bakaa ya katika mfuko wa kubadilishia madeni ambayo imezuiliwa ikisubiria taarifa za utekelezaji kutoka kwa waliokopeshwa jinsi

www.jamii-forums.com

	walivyotumia fedha walizopata, ili kuhalalisha utoaji zaidi. Bakaa haijabadilika kwa kuwa hakuna waombaji zaidi waliojitokeza. **(vi) Mfuko wa Kuleta Unafuu wa Madeni ya Mashirika ya Kimataifa Sh. 10.560 bilioni** Hizi ni fedha ambazo awali zilitolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ili kusaidia kuleta uwiano wa kuuza na kununua nje ya nchi na baadaye zilipewa Serikali kupitia mpango wa unafuu wa madeni ya mashirika ya kimataifa. Mpaka kufikia mwisho wa mwaka 2009/2010 akaunti hiyo ilikuwa na bakaa ya Sh. 85,716,634. **(vii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania Sh. 50 bilioni** Benki Kuu iliripoti kiasi cha Sh. 30 bilioni ikiwa ni bakaa ya fedha za mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutoka kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010 kati ya Sh. 50 bilioni zilizotengwa kwa ajili ya kufanikisha uanzishwaji wa benki ya maendeleo ya kilimo Tanzania. **2. Makosa katika kuripoti mikopo iliyotolewa na Serikali kama dhamana Sh.64,321,859,471** Ufafanuzi Na. 38 wa taarifa za fedha unaonesha mikopo ya moja kwa moja iliyotolewa na Serikali kwa Makampuni ya Maua. Hata hivyo, kiasi kilichooneshwa kilitambuliwa kama mikopo na kujumuishwa pamoja na mikopo ya kibiashara ya Sh. 514,958,828,292 iliyochukuliwa na walengwa kutoka taasisi mbalimbali. Mikopo hii ya moja kwa moja ni mali ya Serikali na sio dhamana ya madeni kwa Serikali. Hivyo basi, taarifa ya mikopo ya moja kwa moja iliripoti pungufu ya Sh. 64,321,859,471 wakati taarifa ya dhamana iliripoti zaidi kwa kiasi hicho hicho.

www.JamiiForums.com

3. Taarifa za Hesabu Jumuifu hazikutayarishwa kulingana na mahitaji ya Kifungu cha 25 (a) na (b) cha Sheria ya Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) kutokana na kushindwa kuandaa mizania inayoonesha rasilimali na madeni ya Mfuko Mkuu na taarifa ya vyanzo na matumizi ya fedha kwa ajili ya Mfuko Mkuu inayoonesha mapato na matumizi ya Mfuko kwa mwaka.

Masuala ya Msisitizo

- **Madeni yasiyolipwa Sh. 577,537,084,848**
  Taarifa za hesabu jumuifu zilionesha madeni ya Sh. 577,537,084,848 ambayo yalikuwa hayajalipwa hadi tarehe 30 Juni 2011. Hii ni kinyume na viwango vya kimataifa vya uhasibu wa sekta ya umma vya fedha taslimu na kanuni Na. 53 (1), (3) - (5) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (zilizorekebishwa 2004) ambayo inataka akaunti za Serikali kutunzwa kwa misingi ya fedha taslimu na kwamba hakuna Afisa Masuuli atakayefanya malipo katika akaunti ya Serikali ambayo haina fedha.

  Kanuni inakataza kuacha madeni yatokee bila ya kuwa na fedha, na kuwa hiyo ni kukiuka dhana ya Bunge kuidhinisha fedha kabla kutumiwa. Aidha, Kanuni Na. 54 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 inakataza Maafisa Masuuli kuhamisha matumizi ya mwaka mmoja kwenda mwaka mwingine. Uhamisho wa aina hiyo unachukuliwa kama matumizi yasiyoidhinishwa.

- **Mihadi isiyolipwa Sh. 79,113,403,430**
  Ukaguzi umebaini kuwa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali zilikuwa na mihadi ya jumla ya Sh. 79,113,403,430 ambayo ilikuwa haijalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011. Kuna uwezekano kuwa Maafisa Masuuli waliingia mihadi hii mwishoni mwa mwaka ili kuepuka kurudisha kwa Mlipaji Mkuu wa

www.JamiiForums.com

	Serikali kiasi cha fedha zilizobakia kwenye akaunti zao. • **Madeni yaliyotolewa na Serikali ambayo hayajalipwa Sh. 480,229,660,682** Serikali ilikuwa na mikopo ya jumla ya Sh. 480,229,660,682 iliyotolewa kwa taasisi mbalimbali binafsi na za umma ambayo ilikuwa haijarudishwa hadi kufikia tarehe 30 Juni,2011. Jitihada za kukusanya mikopo hii haziridhishi na baadhi ya mikopo haijarudishwa zaidi miaka kumi (10) sasa. • **Deni la Taifa ambalo halijalipwa Sh. 14,441,617,939,770** Taarifa ya hesabu jumuifu ziliripoti madeni ya taifa ya Sh. 14,441,617,939,770 ambayo yalikuwa hayajalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 38 ikilinganishwa na Sh. 10,503,806,011,885 yaliyoripotiwa kwa kipindi cha mwaka jana. Ongezeko hili ni kubwa sana kiasi kwamba limeongeza jumla ya deni kwa asilimia 125 ya bajeti ya Serikali (matumizi ya kawaida na fedha za wahisani) ya Sh. 11,609,557,584,000. Hali hii kama haijadhibitiwa itasababisha uchumi wa nchi kuyumba na kuingia kwenye mgogoro wa kifedha kwa kuwa kama ilivyoelezwa kwenye kipengere Na. 1 kwenye mambo yenye msisitizo, baadhi ya madeni hayakujumuishwa kwenye taarifa za hesabu jumuifu.

www.JamiiForums.com

SURA YA 8

MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO

8.1 Majumuisho

Matokeo ya ukaguzi katika taarifa hii yaliwasilishwa kwa Maafisa Masuuli wote kwa ajili ya utekelezaji. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali-Wizara ya Fedha.

Katika taarifa hii nimebainisha dosari na mapungufu mengi katika mifumo ya udhibiti wa ndani yaliyosababisha na kuwepo mianya na usimamizi dhaifu wa fedha. Masuala haya yanatakiwa kushughulikiwa na Maafisa Masuuli kwa kuweka mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani na itakayolenga kuzuia kabisa kutokea tena kwa mapungufu haya.

Ili kueleza kikamilifu mapungufu niliyoyataja katika taarifa hii, nimewajibika kutoa tena mapendekezo yangu kuhusu dosari nilizobaini katika ukaguzi, ambayo kama yatatekelezwa, yataweka usimamizi bora wa masuala ya fedha ndani ya Serikali.

8.2 Mapendekezo

8.2.1 Kutotekeleza mapendekezo ya miaka ya nyuma

Mapendekezo yangu kwa kaguzi za miaka ya nyuma yameonekana kutotekelezwa na baadhi ya maafisa Masuuli, hii inaashiria kuwa Serikali haitilii maanani mapendekezo yangu. Katika hili, masuala yaleyale yamekuwa yakijirudia kila mwaka.

Serikali iongeze jitihada na kuhakikisha kuwa mapendekezo ninayotoa yanatekelezwa kwa wakati ili kuzuia kutokea tena mapungufu au dosari za aina hii.

www.JamiiForums.com

Hazina inatakiwa kutoa maelekezo/mwongozo kwa Maafisa Masuuli wote wachukue hatua muafaka katika kuboresha mifumo ya kutunza kumbukumbu na nyaraka, suala ambalo ndio chanzo cha hoja za ukaguzi. Ukosefu wa viambatanisho husababisha kushindwa kutekeleza mapendekezo yangu.

8.2.2 Matokeo ya ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu

- Maafisa Masuuli kabla ya kuwasilisha katika ofisi yangu nyaraka za malipo ya kustaafu kwa ajili ya ukaguzi, wanapaswa kuhakikisha ukamilifu na usahihi wa nyaraka hizo kulingana na sheria na taratibu za ajira pamoja na sheria na kanuni za kulipa mafao ya kustaafu.
- Serikali ihakikishe kwamba watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na maafisa wa kijeshi wanapoteuliwa kushika nyadhifa za kisiasa kwanza walipwe mafao yao katika utumishi wa awali kwa kipindi walichotumikia umma katika masharti ya utumishi huo. Hii itasaidia kulipwa mapema mafao ya uzeeni na pia kuepuka kulipa mafao mara mbili. Vyeo vya kisiasa vinakuwa na masharti ya mkataba na hustahili mafao ya kijinua mgongo

Kwa ujumla matatizo haya yamesababishwa na maafisa wanaohusika na kuandaa mafao ya wastaafu kutokufuata sheria zinazosimamia stahili na ulipaji wa mafao ya wastaafu na utumiaji wa taarifa za wastaafu ambazo sio sahihi katika kutafuta stahili zao.

Pamoja na kwamba mapungufu haya niliyaeleza katika taarifa yangu iliyopita, lakini mapungufu haya yamejitokeza tena katika ukaguzi wangu wa mwaka 2010/11.

Ili kuondoa mapungufu haya, napendekeza kuzingatia mambo yafuatayo:

www.JamiiForums.com

a) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ihakikishe masharti ya ajira yanaeleza ni kwa kiasi gani yataendana na malipo ya kustaafu kutokana na sheria iliyopo ya malipo ya kustaafu. Mfano wa watumishi wa aina hii ni kama ifuatavyo:

(i) Watumishi wanaoajiriwa ambao walikuwa nje ya utumishi wa umma kama wale wanaotoka katika mashirika ya kimataifa ambao wanakuja na mishahara yao
(ii) Maafisa waliopita katika ajira zaidi ya moja
(iii) Maafisa wanaoteuliwa katika nafasi za kisiasa
(iv) Maafisa wa kijeshi wanaopewa kazi nyingine
(v) Maafisa wanaofanya kazi kwa kuazimwa

b) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe mwongozo kwa mamlaka za ajira kuhusiana na malipo ya kustaafu kwa watumishi wanaolipwa mishahara nje ya viwango vya serikali.

c) Hazina na wadau wengine wa malipo ya kustaafu waimarishe mifumo ya kupitia na kuhakiki nyaraka za malipo ya kustaafu kabla ya kuziwasilisha katika ofisi yangu kwa uhakiki. Vigezo kama idadi ya majalada yaliyoletwa katika ofisi yangu kuhakikiwa na kukutwa hayana hoja vitumike katika kupima ufanisi na kupunguza au kuondoa usumbufu kwa wastaafu.

d) PSPF isihusike tulipa mafao ya kustaafu kwa watumishi walio katika ajira za mikataba na watumishi wasiostahili.

8.2.3 Matengenezo ya magari ambayo hayakupitia TEMESA Sh.77,318,833

Ninashauri taasisi za Serikali kuzingatia kanuni namba 59(1) na (2) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 kwa kuhakikisha kuwa matengenezo ya magari

www.jamiiforums.com

lazima yaidhinishwe na Wakala wa Ufundi, Umeme na Mitambo (TEMESA) kabla na baada ya matengenezo

8.2.4 Malipo ya mishahara yaliyofanywa kwa watumishi wastaafu, walioacha kazi na wasiostahili

Ili kuzuia malipo ya aina hii kwa siku zijazo, Afisa Masuuli wa mafungu yote wanapaswa kuangalia na kupitia mara kwa mara kumbukumbu za watumishi walio bado kwenye ajira ili kuthibitisha uhakika wa uwepo wao katika ajira. Mawasiliano pia yanatakiwa kuboreshwa ili kuhakikisha kuwa majina ya wastaafu na walioacha kazi yanaondolewa pindi utumishi unapokoma.

8.2.5 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.8,076,574,791

Ninashauri kwamba afisa masuuli wa wizara na idara za serikali kuhakikisha kwamba hati za malipo yanayofanywa kwenye Wizara/Idara zao yawe yameambatanishwa na nyaraka sahihi kulingana na Kanuni 95(4) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004)

8.2.6 Vifaa vilivyolipiwa bado havijapokelewa Sh 31,027,797,820

Ninawashauri Maafisa Masuuli wanaohusika kufuatilia kwa karibu vifaa hivyo na kuhakikisha kwamba vinapokelewa na kuandikwa kwenye vitabu vya ghalani.

8.2.7 Malipo yaliyofanyika katika kasma isiyosahihi Sh.340,756,700

Ninawashauri Maafisa Masuuli kutumia fedha za umma kama ilivyoainishwa kwenye kasma na inapotokea kwamba kasma imekwisha utaratibu wa kuhamisha fedha ufuatwe kwa kuomba kibali toka Wizara ya Fedha kama ilivyo elekezwa kwenye kanuni 51(1-8) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004)

www.JamiiForums.com

8 .2.8 Malipo yenye shaka Sh.1,471,933,333

Afisa masuuli wanapashwa kutekeleza wajibu wao wa kuhakikisha nidhamu katika matumizi na usimamizi wa rasilimali za umma zilio chini ya mamlaka zao. Hatua sahihi inabidi kuchukuliwa ili kuangalia uhalali wa malipo haya.

8.2.8 Kuongezeka kwa malipo ya posho

Serikali inapaswa kuanzisha udhibiti wa posho ili kuhakikisha kuwa posho zilizoidhinishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya utumishi wa Umma ndizo tu zinazolipwa. Vile vile serikali iangalie uwezekanao wa kuongeza mishahara badala ya posho ili watumishi wote waweze kunufaika.

8.2.10 Usimamizi wa manunuzi ya umma

Asilimia 41 ya fedha za umma zinatumika katika manunuzi ya huduma na mali. Pamoja na kwamba matumizi yamepungua kutoka asilimia 51 iliyotumika mwaka jana, bado nashauri Wizara na Taasisi za serkali kuongeza udhibiti katika manunuzi ikizingatiwa kwamba Wizara na Idara za seikali bado kuzingatia kikamilifu matakwa ya sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004. Udhibiti unaotakiwa ni pamoja na wizara/idara za serikali kuwa na watumishi wenye taaluma ya ununuzi, kuimarisha vitengo vya ununuzi, kuimarisha taasisi zinazoendesha mafuzo ya/na kujenga uwezo katika fani ya ununuzi kwenye seriali kuu na serikali za mitaa, kuimarisha bodi za zabuni, na kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani.

8.2.11 Misamaha ya kodi

Serikali inashauriwa kupitia upya sera yake ya misamaha ya kodi kwa lengo la kupunguza misamaha hiyo kuwa ya kiwango cha chini kadri itakavyowezekana. Katika mwaka huu wa fedha, misamaha ya kodi iliongezeka kutoka Sh.680,667,900,000 katika mwaka 2009/10 hadi

www.JamiiForums.com

Sh.1,016,320,300,000 katika mwaka 2010/2011. Kuna haja ya kuangalia misamaha hii ili iweze kupungua jinsi inavyowezekana kwa manufaa ya umma. Vile vile, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wafanye mapitio yenye umakini katika bajeti zake za makusanyo ya mapato kwa lengo la kuzifanya ziwe na uhalisia zaidi.

- Mamlaka ya mapato Tanzania iangalie uwezekano wa kuongeza wigo wa kodi kwa kuhusisha sekta isiyo rasmi
- Serkali ifanye utafiti wa kina ili kuanisha sababu za kushindwa kufikia malengo ya ukasanyaji wa kodi. Baadaye kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania iangalie namna ya kuondoa matatizo hayo ili kuongeza ukusanyaji kodi.

8.2.12 Misaada kutoka nje ya nchi Sh.2,322,857,234,115

Kutokana na maoni yangu ya miaka ya nyuma, hii inaonyesha kuwa misaada ya kutoka nje haina uhakika hivyo si ya kutegemea moja kwa moja. Kuna haja ya serikali kuangalia uwezekano wa kuondokana na utegemezi kwa kuweka mikakati ya kuongeza uwezo wa kukusanya kodi na pia kuwa na udhibiti na matumizi ili kuondokana na matumizi yasiyo na faida.

8 .2.13 Maduhuli yasiyokusanywa kwa wakati

Hesabu Jumuifu za Taifa zimeonyesha maduhuli yasiyokusanywa yamepungua kutoka Sh.116,320,437,345 kwa mwaka 2009/2010 hadi kufikia Sh. 26,697,463,538 kwa mwaka 2010/11 sawa na asilimia 77. Hii inaonyesha kuwa kuna juhudi katika kukusanya mapato ya serkali. Naishauri serikali kuwa endelevu katika kukusanya maduhuli haya.

8.2.14 Taarifa ya madeni ya taifa Sh.14,441,617,939,770

Taarifa Jumuifu ya Fedha za Taifa zinaonyesha kwamba deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 37 kutoka Sh

www.JamiiForums.com

10,503,806,011,884 mwaka 2009/2010 hadi kufikia Sh. 14,441,617,939,770 mwaka 2010/2011.

Kulingana na taarifa za fedha, deni la ndani limeongezeka kutoka Sh.141,395,130,054 na Sh.521,261,841,212 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19% na 23% kwa mwaka 2008/2009 na 2009/2010 na baadaye ongezeko la Sh.951,399,378,619 sawa na asilimia 34.5% kwa mwaka 2010/11

Deni la nje limeongezeka kwa kiasi ukilinganisha na deni la ndani kwa asilimia 44 mwaka 2009/2010 na asilima 38.5 mwaka 2010/2011 ikimaanisha kuwa serikali imekopa zaidi katika taasisisi za nje ikilinganishwa na taasisisi za ndani. Hii inamaanisha kuwa Serikali ina dhima kubwa katika kuwalipa wadai wa nje kuliko wadai wa ndani, na hii kiuchumi ina maana kuwa kiasi kikubwa cha mtaji katika fedha za kigeni kitalipwa nje ya nchi.

8.2.15 Taarifa ya mihadi Sh. 79,113,403,430

Taarifa Jumuifu ya Mihadi isiyoshughulikiwa inaonyesha kufikia Sh. 79,113,403,430 kama ilivyokuwa tarehe 30 Juni, 2011 ikiwa ni pungufu ya 14,747,403,560 sawa na asilimia 16 % ikilinganishwa na ile ya mwaka 2009/10 ya kiasi cha Sh. 93,860,806,990.

Ikihusishwa na hii, ninarudia kusisitiza ushauri wangu nilioutoa mwaka uliopita kwamba serikali inabidi iwe na tahadhari kubwa katika kujiingiza katika mihadi ambapo hakuna fedha ya kugharamia matumizi hayo. Hali kadhalika pale serikali inapokuwa na bakaa ya fedha ambazo hazina mihadi ni vyema zikarudishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

www.JamiiForums.com

8.2.16 Taarifa ya mikopo inayotolewa na Serikali Sh.480,229,660,682

Taarifa ya mikopo iliyotolewa na serikali inaonyesha mikopo isiyorejeshwa hadi tarehe 30 Juni 2011 ya Sh. 480,229,660,682. Hii inaonyesha ongezeko la Sh.20,786,565,296 sawa asilimia 5% ikilinganishwa na kiasi cha Sh.459,443,095,386 mwaka 2009/2010. Serikali inatakiwa kutengeneza mchanganuo ili kujua umri wa madeni hayo na uwezekano wa kulipwa.

8.2.17 Taarifa ya madeni yamkini Sh.30,408,060,580

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Serikali ilikuwa na madeni yamkini yaliyofikia kiasi Sh.30,408,060,580 ambayo asili yake haikuonyeshwa kwenye vitabu.

Hivyo ningependa kuishauri Serikali kujiepusha katika kufanya maamuzi ambayo yatasababisha kushamiri kwa madeni yasiyotarajiwa. Na endapo kuna kesi zinazoendelea mahakamani jitihada zifanyike za kukamilisha hukumu za kesi hizo.

8.2.18 Taarifa ya udhamini wa Serikali **Sh.579,280,687,763**

Makampuni sita ya maua na kampuni moja ya ufugaji zilipewa mkopo wa Sh.514,959,828,292 ambao kimakosa ulionyeshwa kama dhamana ya serikali. Kutokana na makosa haya, hesabu za dhamana ya serikali hazionyeshi hali halisi. Ninaishauri serikali kufanya marekebisho na kuthibitisha urejeshwaji ya mikopo hiyo.

8.2.19 Mfuko wa mpango wa kubadilisha madeni Sh.2,098 billion

Serikali inapashwa kufanya ufuatiliaji wa wakopaji ili kubaini uwepo wa wadaiwa na kama bado madeni yapo. Kwa zile fedha zilizo katika mfuko kwa mUda mrefu, iko haja ya kuzipeleka fedha hizo kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

www.JamiiForums.com

8.2.20 Kutoonyesha madai na amana za Serikali kwenye taarifa za fedha

Taarifa ya fedha iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2011 imeonyesha kiasi cha Sh.165.286 bilioni kama fedha zilizotazamiwa kupokelewa na benki kuu kutoka Serikalini. Hata hivyo, kiasi hiki hakikuonyeshwa kwenye Hesabu Jumuifu za Taifa kama madai ya benki kuu Serikalini. Ninaishauri Serikali kutambua na kuonyesha kwa uwazi amana na madeni/madai yote kwenye Hesabu Jumuifu za Taifa. Vile vile, madai yaliyolipwa baada ya kufunga hesabu za mwaka yaonyeshwe katika kidokezo cha taarifa za fedha.

8.2.21 Madeni ambayo hayakulipwa Sh.577,537,084,848

Mandeni yasiyolipwa ya Sh.577,537,084,848 ni sawa na ongezeko la asilimia 259 ililinganishwa na madenii ya Sh.160,756,067,190 niliyoyatolea taarifa mwaka uliopita. Ninasisitiza ushauri wangu nilioutoa mwaka uliopita kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kuonyesha madeni na amana zote katika taarifa za fedha jumuifu za taifa.

Pia, kwa kuwa serikali inafuata mwongozo wa kimataifa wa sekta ya umma katika kuandaa taarifa za fedha za mwaka unaozingatia malipo na mapokezi fedha taslimu katika kulipa na kupokea fedha sitegemei kuwe na madeni. Pia, manunuzi ya vifaa na huduma yafanyike kwa kufuata makisio yaliyoidhinishwa na Bunge.

8.2.22 Taarifa ya vifaa vya stoo na mali nyingine Sh.38,292,059,659

Taarifa Jumuifu ya Fedha ya tarehe 30 Juni 2011 inaonyesha uwepo vifaa na mali nyingine zenye thamani ya Sh.38,292,059,659. Hili ni ongezeko la asilimia 130 ikilinganishwa na Sh16,806,978,964 nilizotolea taarifa mwaka jana. Ninapendekeza Serikali kufanya manunuzi ya vifaa katika muda unaotakiwa na kuanza kutumika ili kuepuka bakaa kubwa mwishoni mwa mwaka, hali ambayo ni hatarishi, kwani vifaa vinaweza kupotea.

www.JamiiForums.com

8.2.23 Taarifa ya upotevu wa fedha na mali Sh.12,968,168,985

Taarifa Jumuifu ya Fedha inaonesha upovetu wa fedha na vifaa umeongezeka kutoka Sh.11,152,048,065 mwaka 2009/2010 hadi Sh.12,968,168,985 mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la Sh. 1,816,120,920 sawa na asilimia 16.

Ninaishauri serikali kuchukua hatua stahiki ili kuondoa au kupunguza potevu hizo. Vilevile hasara zote ambazo bado kufutwa na azimio la bunge zinapashwa kuendelea kuonyeshwa kwenye taarifa ya fedha, na Hazina wachukue hatua stahiki kuanza mchakato wa kufuta hasara hizi kwa azimio la bunge. Pia mchanganuo wa hasara hizo na kipindi zilipotokea inabidi kuandaliwa.

8.2.24 Mifuko maalumu ya fedha Sh.47,285,051,367

Taarifa Jumuifu ya Fedha inaonyesha Mifuko maalumu ya fedha inayosimamiwa na Wizara na Idara za serikali kulingana na kifungu namba 12 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ina jumla ya Sh.47,285,051,367. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 42 ikilinganishwa na Sh. 81,880,605,817 zilizotolewa taarifa mwaka 2009/2010

Hata hivyo, imebainika kwamba mifuko hiyo hesabu zake hazikuoneshwa na kilichoonyeshwa ni bakaa ya fedha hadi tarehe 30 Juni 2011 na kwa hali hiyo haijumuishi fedha nyingine zilizolipwa kama karadha au mikopo.

Ili kuongeza uwazi, ninapendekeza kuwa rasilimali zote za mifuko maalumu ya fedha zionyeshwe kwenye Hesabu badala ya kuonyesha bakaa tu.

Kwa mifuko endelevu rasilimali zote za mifuko lazima zionyeshwe mwisho wa mwaka na ziingizwe kwenye Taarifa Jumuifu ya Taifa.

8.2.25 Bakaa ya fedha ambayo haikurejeshwa kwa Mlipaji Mkuu Serikali Sh.11,921,864,616

Nashauri Hazina ifanye ufuatiliaji ili kuhakikisha Afisa Masuuli wote wanarudisha fedha zote ambazo hazikutumika kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili ziweze kuingizwa mfuko mkuu wa serikali.

www.JamiiForums.com

Kutokana na dosari hii, ninaishauri Serikali kupitia Hazina (Mhasibu Mkuu wa Serikali) kufuatilia fedha hizi ili zirejeshwe kwa Mlipaji Mkuu wa Seikali na kuingizwa katika mfuko mkuu wa serikali.

8.2.26 Kutofuata Sheria ya fedha ya umma (PFA) na viwango vya kimataifa vya uandishi vitabu vya sekta ya Umma (IPSAS)

Kifungu cha 25(1)(a) cha sheria ya fedha ya umma ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004, kinamtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kutayarisha na kupeleka kwa Waziri na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali mizania ya hesabu ikionyesha mali na madeni katika mfuko mkuu wa serikali.

Pia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS) namba 6 inataka Hesabu Jumuifu kuonyesha taasisi zote zinazomilikiwa kwa ujumla wake au kwa kushirikina na serikali ikiwa ni pamoja na mamlaka za serikali za mitaa, Wakala wa Serikali, Mifuko mbalimbali.

Viwango hivyo pia vinataka wakati wa kutayarisha hesabu hizo, taasisi mama kujumuisha taarifa za fedha kwa taasisi zote zilizo chini wa udhibiti wake na kuunganisha mali na madeni yanayofana. Hivyo nashauri kwamba:-

(i) Serikali kupitia Mhasibu Mkuu wa Serikali iangalie uwezekano wa kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia mfumo wa kutambua mapato hata pale ambapo hayajapokelewa au malipo hata pale ambapo hayajalipwa (accrual) ili kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa mali na madeni ya serikali, hii ikiwa ni pamoja na Hesabu za Deni la Taifa, Taarifa ya Msajili wa Hazina, na Taarifa ya Majumuifu ya Fedha ya Taifa.

(ii) Hazina pamoja na mambo mengine iandae mizania ya hesabu ya mali na madeni ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kama inavyotakiwa na kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha ya Umma.

www.JamiiForums.com

(iii) Hesabu zote za Taasisi za Umma zijumuishwe kwenye Taarifa Jumuifu ya Fedha ya Taifa.

8.2.27 Wajibu wa Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuishauri Serikali

Kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, nina jukumu la kuishauri Serikali kwa malengo yafuatayo:

(a) Kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyo na tija;
(b) Kuongeza ukusanyaji mapato ya Serikali; na
(c) Kuiepusha Serikali kupata hasara kutokana na dharau, uzembe, wizi, kukosa uaminifu, rushwa, ufisadi unaohusisha fedha za Umma na rasilimali nyinginezo.

Kutokana na wajibu huo wa kisheria, nimekuwa nikifanya kaguzi maalum na kuwa na vikao vya kubadilishana mawazo na wadau ili kuniwezesha kutoa ushauri na kuwasilisha mapendekezo kwa Waziri mhusika kadri ninavyoona inafaa kwa lengo la kuboresha usimamizi wa rasilimali za Umma. Kutokana na majadiliano na wadau na kaguzi maalum zilizofanyika, mapendekezo yafuatayo yalitolewa:

8.2.28 Kuboresha Mfumo wa Bajeti

Moja ya mambo muhimu katika kuhakikisha uwajibikaji ni utekelezaji wa bajeti. Moja ya hatua za mchakato wa kuandaa bajeti ni majadiliano baina ya maafisa wa bajeti katika ngazi ya Hazina na Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, pia Bunge baada ya masuala husika kupitiwa na Kamati za Kisekta, mchakato unaojulikana kama mjadala wa Umma na upitishaji wa bajeti.

Baada ya bajeti kupitishwa, utekelezaji wake hufuata ambapo ukusanyaji maduhuli na kutoa huduma kwa Umma huanza kufanyika. Kwa hiyo, utekelezaji wa

www.JamiiForums.com

bajeti unahusisha kukusanya maduhuli na kuyaingiza vitabuni, kutoa huduma kwa Umma kupitia bajeti ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mchakato wa bajeti umeonekana kuwa na changamoto kadhaa kama ifuatavyo:

8.2.29 Bajeti kuchelewa kuanza kutumika

Imekuwa ni kawaida kwamba, mjadala kwa ajili ya bajeti kupitishwa na Bunge unafanyika katika kipindi cha mwezi Juni hadi Agosti kila mwaka, wakati Sheria ya Matumizi inaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai kila mwaka. Hii ina maana kwamba, utekelezaji wa bajeti unaanza katikati ya mwezi Septemba ya kila mwaka na kwa hali hiyo, katika kipindi cha kati ya tarehe 1 Julai hadi katikati ya mwezi Septemba, majukumu muhimu ya Serikali hasa shughuli za maendeleo hazifanyiki kutokana na kutokuwepo bajeti iliyopitishwa.

Ni vyema ikaeleweka kuwa Rais anaweza kutoa idhini ya kutumia fedha kwa shughuli za Serikali kiasi ambacho ni sawa na theluthi moja (1/3) ya bajeti ya mwaka uliopita au bajeti ya sasa lakini kiasi hiki ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu, hakihusishi utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

